SIRI PART 2

MAISHA NA KIFO CHA MELANIE CHUMA

SEASON 10

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

1.MISS TANZANIA
2.I WAS WRONG
3.TEN CHAPTERS
4.I DO
5.SERENA
6.BEFORE I DIE
7.BEYOND PAIN
8.PENIELA
9.QUEEN MONICA
10.THE FOOTBALL
11.I DIED TO SAVE PRESIDENT
12.KIAPO CHA JASUSI
13.KIKOSI CHA SIRI
14.SIRI

MAWASILIANO
0764294499

“Peniela ametuma namba hizi za watu ambao wamekuwa wakiwasiliana na Devotha,tuanze kuzifuatilia kuwafahamu wenye namba hizi.” akasema Mathew kisha Ruby akaichukua kompyuta yake akaweka sawa program zake na kuanza kupiga zile namba.Namba tatu hazikuwa zinapatikana na alipoingiza namba ya nne kwa ajili ya kupiga akastuka kwani alikuwa nayo ile namba tikana.

“Edwin Mbeko ! akasema Ruby

“Edwin Mbeko?Mathew naye akauliza

“Ndiyo hii ni namba yake” akasema Ruby

“Sasa picha imeanza kujitengeneza Ruby.Hebu tazama huu mtiririko.Devotha ambaye ni mtu wa karibu na Melanie amekuwa na mawasiliano na Edwin Mbeko wa SNSA.Jana tumempoteza Khalid Sultan kwa kitendo kilichofanywa kwa makusudi na watu ndani ya SNSA aliko Edwin.Kwa Edwin kuwa na mawasiliano na Devotha ambaye ni mtu wa karibu na

Melanie nalazimika kuamini kwamba lazima Edwin atakuwa katika mtandao wa akina Melanie na ndiye anayewezesha mambo ya yote ya matandao huo kufanikiwa” akasema Mathew

“Mathew hapa nilipo ninahisi mwili wote unanitetemeka kwa woga.Sikutegemea kabisa kama Edwin angeweza kuwepo katika mtandao huu” akasema Ruby na Mathew akamtaka awashe gari

“Tunaelekea wapi?

“Tunakwenda nyumbani nikachukue silaha kisha tunamfuata Edwin ofisini kwake SNSA”

“Hawataturuhusu kuingia pale kwani mimi si mkurugenzi kwa sasa hadi suala langu litakapotatuliwa”

“Ndiyo maana ninakwenda kuchukua silaha zitakazotuwezesha kungia pale SNSA”

“Mathew huo ni mpango wa hatari kubwa.Ofisi ile ina ulinzi mkali na si rahisi kuivamia” akasema Ruby

“Tutaingia pale ndani na lazima tumpate Edwin.Usihofu Ruby uko na Mathew Mulumbi the unstoppable! akasema Mathew

“Mathew naomba nikushauri mpenzi wangu.Kwa mchana huu tulikuwa na mpango wa kumshughulikia Gosu Gosu.Tumuhamishe Gosu Gosu na kuhakikisha anakuwa sehemu salama halafu usiku wa leo ndipo tukavamie SNSA na kumchukua Edwin.Naamini mpaka muda huo hatakuwa anafahamu kama Devotha

ameuawa na wala hatakuwa akijua kama tumefahamu ana mawasiliano na Devotha” akashauri Ruby.Mathew akafikiri kisha akasema

“Ushauri mzuri.Tumuhamishe kwanza Gosu Gosu na kumpeleka sehemu salama halafu nitamonyesha Yule Edwin na mtandao wake mimi ni nani” akasema Mathew

ENDELEA.....

Geti la nyumba anayoishi Melanie Davis lilifunguliwa na

gari la Edwin Mbeko likaingia.Akashuka garini na kufungua buti akatoa maboksi matano watumishi wa ndani wa Melanie wakatoka na kumsaidia kubeba maboksi yale wakayaingiza ndani. Mtumishi akamuongoza Edwin kwenda bustanini walikokuwa wamekaa Melanie.James Kasai na Khalid Khalid.

“ Nimefurahi sana kuwaoneni tena mkifurahia hali ya hewa safi ya Dar es salaam” akasema Edwin

baada ya kusalimiana na akina Melanie

“Dar es salaam ni jiji zuri.Nitakuja tena kutembea siku nyingine.Nitakapokuja wakati mwingine Melanie naomba unitafutie mtoto mzuri wa kitanzania wa kustarehe naye.Nimepapenda sana Tanzania” akasema James Kasai huku akivuta sigara na mezani kukiwa na chupa kubwa ya pombe kali akinywa taratibu.

“Umekuja na vifaa vyote nilivyoelekeza?akauliza Khalid

“Ndiyo nimefanikiwa kupata kila kitu” akajibu Edwin

“Edwin ninafurahi sana kufanya kazi nawe.Nimependa namna ulivyo makini katika kazi yako natumai huko siku za usoni tutashirikiana katika kazi nyingi zaidi za hapa Tanzania” akasema Khalid

“Usijali Khalid mashirikiano haya yataendelea” akasema Edwin

“Kwa kuwa kila kitu tayari mimi ninakwenda kuanza kutengeneza bomu” akasema Khalid na wote wakainuka

wakaelekea ndani.Maboksi yale aliyokuja nayo Edwin yakaingizwa katika chumba maalum ambacho kiliandaliwa kwa ajili ya kutengenezea bomu vifaa vikatolewa katika maboksi,Khalid akavikagua kama vimetimia na bila kupoteza muda kazi ikaanza.

Wakati Khalid akianza kutengeneza bomu Edwin akamuomba Melanie watoke wakazungumze nje.

“Melanie kuna kitu kimetokea jana usiku sikukujulisha nilitaka

nikifanyie kazi kwanza ndipo nikujulishe” akasema Edwin.

“Nini kimetokea Edwin? Akauliza Melanie macho yake yakionyesha wasiwasi.

“Jana usiku baada ya kutoka huku nilirejea tena ofisini nikakuta kuna kitu kimetokea.Mkurugenzi wetu mpya alifahamu kwamba kuna mchezo ulifanyika wakati wa zoezi la kumfuatilia Khalid”

“Amegundua?akauliza Melanie

“Ndiyo amegundua”

“Amegundua vip?akauliza Melanie

“Kuna watu ndani ya idara ambao niliwatumia katika kuvuruga zoezi lile kwa kuwapa fedha kidogo.Baada ya zoezi kumalizika nilimuondoa mmoja na kwenda kumuua kwa ajili ya usalama wetu Yule mwingine nilitegemea baada ya kutoka huku ndipo ningeenda kummaliza lakini niliporejea ofisini nikakutana na taarifa kwamba mkurugenzi akishirikiana na mtu mwingine ambaye si mfanyakazi wa idara yetu walimpeleka huyo jamaa katika chumba cha mahojiano wakamuhoji kisha wakaanza

kumtesa hadi akapoteza fahamu.Nilipofika nilimkuta akiwa tayari amepata fahamu nikamuuliza nini sababu ya kuteswa vile akanieleza kwamba tayari Annabel anafahamu kuhusu kile kilichofanyika na alimtesa ili amueleze ukweli..”

“Alimueleza chochote ?akauliza Melanie kwa wasi wasi

“Hapana hakumueleza chochote” akajibu Edwin

“Ahsante.Tayari nilikwisha anza kuwa na wasi wasi kwamba mpango wetu

umeingia kirusi” akasema Melanie

“Nilikuwa nimempa onyo kwamba akithubutu kusema chochote ataikosa familia yake ndiyo maana hakusema chochote kwa ajili ya familia yake.Hata hivyo nililazimika kumuua pale pale katika chumba alichokuwa amelazwa”

“Ulifanya jambo zuri sana.Vipi kuhusu huyo mkurugenzi?Naye pia anatakiwa ashughulikiwe haraka sana kwani kuna kitu amekwisha anza kukihisi.Huyu

ni hatari mno kwetu” akasema Melanie

“Tayari nilikwisha anza kumshughulikia.Jana hiyo hiyo nililazimika kutumia kanuni zetu kumuondoa katika nafasi yake ya ukurugenzi.Pale idarani tunazo kanuni ambazo zinatuwezesha wafanyakazi kumuondoa kiongozi na niliwashawishi wenzangu tukazitumia kanuni hizo kumuondoa Annabel katika nafasi yake.Atakaa nje ya ofisi kwa muda wa siku saba.Nilifanya hivi kwa lengo la kumuweka nje ya ofisi ili

tuendelee na mipango yetu.Kwa sasa hakuna wasi wasi na kila kitu kitaendelea kama kawida” akasema Edwin

“Ahsante Edwin kwa hicho ulichokifanya hata hivyo bado haitoshi.Huyu mwanamke kama amefanikiwa kugundua jambo hilo hatakaa kimya lazima ataendelea kuchunguza hadi aufahamu ukweli.Kwanza amefahamuje jambo hilo?Au watu uliowatumia hawakuwa makini na wakasababisha akagundua walichokifanya?akauliza Melanie

“Niliowatumia ni watu makini sana na wanajua wanachokifanya.Niliyemtumia kuvuruga mawasiliano anaitwa Dina ndiye ambaye tunamtegemea sana katika masuala yote ya satelaiti.Kwa ujumla wote hawa wawili niliowatumia wametekeleza nilivyowaambia hata mimi nashindwa kuelewa imetokeaje hadi Annabel akagundua kuhusu mchezo ule.Nitaendelea kuchunguza kujua namna alivyofahamu” akasema Edwin

“Sawa Edwin lakini huyu mwanamke ni kama fisi.Tayari amenusa harufu ya nyama na ataendelea kuifuatilia kujua mahala alipo .Huyu Annabel tayari amekwisha hisi kuna kitu kinaendelea na hata kama akiwa nje ya ofisi ataendelea kufuatilia hadi aufahamu ukweli. Huyu ni mdudu ambaye anatakiwa kufinyangwa haraka .Nataka auawe haraka sana kabla hajaleta madhara” akasema Melanie

“Huo ndio mpango wangu lakini kwanza nilitaka

nimuondoe ofisini ili atupe nafasi ya kutekeleza mipango yetu na baada ya kutoka ofisini sasa ninaanza kuandaa mpango wa kumuua kumuondoa kabisa ili kuwa na uhakika kwamba hakuna kiumbe yeyote ambaye anaweza kuwa hatari kwetu”akasema Edwin

“Vipi kuhusu Gosu Gosu ? Kuna taarifa zozote umepata kutoka hospitali?akauliza Melanie

“Gosu Gosu sijapata bado taarifa zake zozote”

“Kill him today ! akasema Melanie

“Nataka hadi jua litakapochwea Gosu Gosu awe tayari ameuawa.Kwa namna yoyote ile hakikisha siku ya leo haipiti bila Gosu Gosu kuuawa.Yule ni mtu hatari sana kwani mipango yangu mingi anaifahamu na kwa mujibu wa Devotha,Gosu Gosu ana ukaribu na watu ambao wanaweza kuwa hatari kwetu.Endapo akifumbua macho anaweza akawaeleza watu hao kuhusu mimi na mambo yakaharibika.Make

sure you kill him today.Sitaki kuwe na uchafu wowote njiani tunamopita” akasema Melanie

“Usijali Melanie nitakapotoka hapa ninakwenda kushughulikia suala hilo.Devotha umewasiliana naye leo?akauliza Edwin

“Nilijaribu kumtafuta lakini hapatikani simuni.Nitamtafuta tena baadae” akasema Melanie

“Jenerali Akiki alinipigia simu asubuhi akanijulisha kwamba alizungumza na Dr

Fabian kuhusu kuandaa mkutano na amekubali”

“That’s good” akasema Edwin huku akitabasamu

“Lini wanakutana kwa mazungumzo?akauliza Edwin

“Jenerali Akiki alitaka iwe kesho lakini Dr Fabian ameahidi kumjulisha hapo baadae baada ya kuwasiliana kwanza na Rais Patrice Eyenga”

“Kama Dr Fabian amekubali basi hata Patrice hawezi kukataa na kama Jenerali Akiki ametaka kikao kifanyike kesho basi

kitafanyika hiyo kesho.Hii ni fursa ambayo wanaitafuta sana kukaa meza moja na Jenerali Akiki kuzungumza na hawataweza kuipuuzia hata kidogo.Melanie ninakusifu sana kwa uwezo mkubwa ulio nao hadi ukaweza kumshawishi Jenerali Akiki akakubaliana nawe”

“Kila penye nia pana njia Edwin.Ninataka kulipiza kisasi na lazima nifanye kila linalowezekana kuhakikisha mipango yangu inakamilika”

“Khalid amekwisha fanya mawasiliano na mtu aliyeahidi

kumleta kwa ajili ya kutekeleza shambulio la kujitoa mhanga?akauliza Edwin

“Ndiyo.Tayari amekwisha fanya mawasiliano na hivi tuzungumzavyo tayari mtu huyo amekwisha anza safari.Ni mtu kutoka katika kundi la Alshabaab la nchini Somalia ambaye makazi yake ni nchini Kenya.Tayari amekwisha vuka mpaka wa Namanga hivi sasa anaelekea Arusha.Kesho asubuhi tutampokea hapa Dar es salaam” akasema Melanie

“Huyu anatakiwa kufika Dar es salaam leo hii hii ili

tuwe na uhakika mkubwa kwamba tunaye mtu wa kutekeleza shambulio hilo.Hivi sasa bomu linatengenezwa na alitakiwa awepo hapa tayari kwa kazi hiyo.Khalid anatakiwa kuwasiliana na huyo mtu na kumtaka akifika Arusha asiendelee tena na safari.Mimi nitaruka na helkopta kwenda kumchukua.Kila kitu lazima kikamilike leo hii hii" akasema Edwin

"Hilo ni wazo zuri sana Edwin" akasema Melanie wakaelekea ndani ambako

Khalid alikuwa anaendelea na maandalizi ya kuunda bomu. Wakamueleza mapendekezo ya Edwin akakubaliana nayo kisha kwa kutumia simu ya Melanie akawasiliana na huyo mtu aliyekuwa njiani akielekea Dar es salaam kwenda kutekeleza shambulio la kujitoa mhanga akampa maelekezo ya kutoendelea na safari atakapofika Arusha na asubiri maelekezo mengine

“Kwa kuwa limejitokeza suala hili la huyu mtu nalazimika kuahirisha baadhi ya mambo ili nielekee Arusha

kumchukua kisha nirejee mapema Dar es salaam kuendelea na masuala mengine” akasema Edwin

“Sawa Edwin lakini hakikisha unapoondoka umeacha watu watakaolishughulikia suala la Gosu Gosu pamoja na mkurugenzi wako Annabel” akasema Melanie

“Sawa Melanie nitatoa maelekezo kwa vijana wafanye uchunguzi namna tukavyoweza kumuua Gosu Gosu.Lazima kwanza tufanye uchunguzi kwa kuwa naamini

umakini utakuwa mkubwa sana baada ya jaribio lile la kwanza la kumuua kushindwa kufanikiwa.Vijana wataniletea mapendekezo ya namna tutakavyoweza kutekeleza mpango huo wa kumuua Gosu Gosu halafu tutajipanga kwa usiku wa leo tuweze kumuonda.Kuhusu Annabel nitalazimika kumfanyia uchunguzi kwa kuwa mpaka sasa sifahamu mahala anakoishi.Kwa Rais kumpa nafasi kama ile ya ukurugenzi wa idara nyeti lazima amejiridhisha kuwa ana

sifa.Lazima atakuwa ni mtu mwenye mafunzo ya ujasusi na anafahamu mbinu nyingi hivyo kumuua inahitaji umakini mkubwa.Nitalishughulikia suala lake nitakaporejea kutoka Arusha.Msiwe na wasiwasi wowote kila kitu kitakwenda vizuri.” akasema Edwin kisha akaagana na Melanie akaondoka

“Melanie yuko sahihi kbaisa.Annabel anastahili kuuawa lakini kuuawa kwake kunapaswa kufanywa kiutaalamu mno.Nitalishughulikia hili

baada ya kurejea kutoka Arusha” akawaza Edwin akiwa garini baada ya kuondoka nyumbani kwa Melanie

PARIS – UFARANSA

Mlinzi aliyesimama katika mlano wa ofisi ya Rais wa Ufaransa aliufungua mlango watu wawili wakaingia na Rais Michael Weren akasimama akawakaribisha watu wale wakasalimiana kisha akawaelekeza waketi sofani.

“Nilitegemea Devotha awe amekwisha fika hapa hadi

mida hii lakini bado hajafika naomba dakika chache tumsubiri kwani yeye ni muhimu sana katika mazungumzo haya” akasema Michael Weren na kwenda mezani kwake akachukua simu akampigia Devotha lakini simu yake haikuwa inapatikana

“Simu ya Devotha haipatikani nadhani tuendelee na mazungumzo atakuta tukiendelea” akasema Michael Weren

“Mheshimiwa Rais kubwa ambalo limetuleta hapa ni kutaka kupata mrejesho

kuhusiana na ule mpango wetu wa Afrika.Nini kinaendelea hadi hivi sasa?akauliza mmoja wa wale jamaa aliyekuwa na suti ya rangi ya kijivu

“Kwa ujumla mpango wetu unakwenda vizuri sana mpaka sasa.Kama mnavyosikia katika vyombo vya habari ni kwamba hali ya kiusalama katika eneo la Afrika mashariki ni tete.Kumetokea mvurugano mkubwa sana na jumuiya kwa sasa iko hatarini kuvunjika.Rwanda na Uganda zinashambuliana mpakani.Jamhuri ya

kidemokrasia ya Congo nayo imepeleka vikosi vyake katika mpaka wake na Uganda.Nchi tatu za Tanzania,Rwanda na jamhuri ya kidemokrasia ya Congo zinaandaa kikosi cha pamoja kwa ajili ya kuvamia nchini Uganda kumsaka James Kasai ambaye alitekeleza shambulio lililopelekea mvurugano huu ukatokea.Tayari Uganda imetoa onyo kwamba endapo kikosi hicho kitathubutu kutia mguu wake nchini Uganda basi itatumia nguvu kubwa kukisambaza.Haya yoteni

matokeo ya mipango yetu na hakuna ubishi kwamba jumuia ya Afrika mashariki inakwenda kusambaratika” akasema Michale Weren

“Tunafuatilia sana hali ya mambo inavyokwenda Afrika mashariki na zipo dalili kwamba jumuiya hiyo inaweza ikasambaratika na sisi tukapata njia ya kupita kuelekea Congo lakini kuna jambo ambalo linaleta ukakasi kidogo njia iliyotumika katika kusababisha hali hii ikatokea.James Kasai anayeongoza kikundi cha

waasi pamoja na kikundi cha kigaidi cha IS walishirikishwa katika mpango huu.Hii imetia doa mpango wetu.Hatukupanga kuwatumia magaidi au James Kasai ambaye amekwisha ua mamia ya watu na anatafutwa na mahakama ya kimataifa ya uhalifu wa kivita kutokana na mauaji aliyoyafanya.Mtu kama James Kasai au kikundi cha IS kufahamu mipango yetu ni hatari kubwa sana kwetu" akasema Yule mzee

"Hata mimi nilipoelezwa mara ya kwanza kwamba

James Kasai na kikundi cha kigaidi cha IS wameshirikishwa katika mpango huu nilistuka na kutaka mpango huo wa kuwatumia watu hao usitishwe mara moja lakini nikapewa ufafanuzi na faida za kuwatumia James na IS nikaona ni mpango mzuri nikatoa maelekezo kwamba waendelee kushirikiana nao” akasema Michael

“Unaweza ukatueleza mheshimiwa Rais faida za kuwatumia hawa magaidi na James Kasai?

“Faida kubwa ni kwamba mpango huu hautajulikana kama sisi tunahusika utaonekana ni mpango wa IS na James Kasai.Mpaka sasa nchi za Afrika mashariki zinamsaka James kwa udi na uvumba na hii inatupa sisi nafasi ya kuendelea na mipango yetu bila ya kutambulika”akasema Rais Michael na kuwaeleza kuhusiana na mpango unaoendelea wa kuwaua marais wa Tanzania na Congo kuwafafanulia faida zake

“Kama mpango huo utafanikiwa basi itakuwa ni chanzo cha vita kati ya majeshi ya serikali ya Congo na kikundi cha James Kasai na vikundi vingine pia vitaibuka nchi ya Congo itarejea kuwa kama ilivyokuwa zamani.Patrice Eyenga amekuwa ni kikwazo kikubwa kwetu lakini kama jumuiya ya Afrika mashariki ikisambaratika na tukafanikiwa kumuua Patrice Eyenga basi njia itakuwa nyeupe ya kuingia Congo”akasema Michael

“Ni mpango mzuri sana huo lakini nina mapendekezo kwamba huyu mtu ambaye ametumwa kwenda kufanikisha mpango huu auawe mara tu atakapokamilisha mpango huo.Mtu huyo kuendelea kuwa hai ni hatari sana kwetu.Ni vipi kama siku moja James Kasai akakamatwa na kumtaja kuwa anashirikiana naye? Itakua ni aibu kubwa kwetu hivyo napendekeza mara tu atakapokuwa amemaliza kazi yake auawe mara moja na sisi tuendelee na mipango

mingine” akatoa ushauri mmoja wa wale jamaa

“Ushauri wako ni mzuri na nitauzingatia.Ni kweli huyu mtu akiendelea kuwepo hai itakuwa ni hatari kubwa kwetu.Wazo la kumuua ni zuri” akasema Rais Michael Weren na baada ya mazungumzo ya takribani saa mbili akaagana na wageni wake wakaondoka.Mara tu wageni wake walipoondoka Rais Michael akachukua tena simu na kumpigia Devotha lakini bado simu yake haikupatikana

“Devotha uko wapi? Ninahitaji sana kujua taarifa za kinachoendelea Tanzania” akawaza Michael na kuketi katika kiti chake akaweka miguu juu ya meza

“Kwa nini Melanie akaanzisha mashirikiano na magaidi wa IS? Naamini lazima atakuwa amewaeleza kuhusiana na mipango yetu na hiki ni kitu kibaya sana.Jambo hili si la kuchukulia kirahisi kwani magaidi hawa wanaweza wakatugeuka siku za usoni na kutuchafua.Nadhani pendekezo la kumuua Melanie

ni zuri.Mara tu atakapomaliza mpango wa kuwaua marais wa Tanzania na Congo lazima naye auawe.Nitajadiliana na Devotha kwa kina suala hili" akawaza Michael.

TANZANIA

Saa kumi bna mbili za jioni helkopta ya idara ya SNSA ilitua katika bohari kuu la idara hiyo.Edwin Mbeko alikuwa ametoka jijini Arusha kumchukua mtu ambaye angetekeleza shambulio la kujitoa mhanga lililolenga

kuwaua marais Dr Fabian na Patrice Eyenga.Tayari gari lake lilikwisha fika mahala pale akashuka katika helkopta pamoja na mtu wake aliyekwenda kumchukua Arusha wakaingia garini na kuondoka kuelekea nyumbani kwa Melanie Davis.

“Abdi karibu sana Dar es salaam” akasema Edwin lakini Abdi hakujibu kitu alikuwa ameelekeza macho yake nje akitazama pilika pilika za jioni za wakazi wa jiji la Dar es salaam.

Safari iliendelea kimya kimya hadi walipowasili nyumbani kwa Melanie akafunguliwa geti na kuingia ndani.Melanie aliwapokea na kuwakaribisha sebuleni ambako James Kasai alikuwa ametulia sofani akiwa na chupa kubwa ya mvinyo.

“Karibu sana Abdi.Huyu ni James Kasai naamini umewahbi kusikia taarifa zake” Melanie akafanya utambulisho na Abdi alionekana kustuka kidogo kumfahamu James Kasai. Melanie akamchukua na kumpeleka katika chumba

alichoandaliwa ili apumzike kabla ya mazungumzo hapo baadae.

“Mambo yanakwendaje hapa?akauliza Edwin

“Mambo yanakwenda vizuri.Khalid anaendelea na uundaji wa bomu na kwa maelezo yake anaelekea katika hatua za mwisho kulikamlisha”akajibu Melanie

“Vizuri sana.Mpaka hapa tuna uhakika kwamba bomu linaelekea kukamilika na mtu wa kulilipua tunaye.Umepata mrejesho wowote kutoka kwa Jenerali Akiki?Edwin akauliza

“Ndiyo.Amenipigia simu akanijulisha kwamba marais Dr Fabian na Patrice Eyenga wamekubali kukutana naye kesho jijini Dar es salaam.Mipango yetu yote inakwenda vizuri”

“Safi sana.Nitarejea hapa baadae natakiwa kurejea ofisini nikashughulikie suala la Gosu Gosu kwani niliwachia kazi vijana wachunguze namna tutakavyoweza kumuua.Kabla ya mapambazuko ya lazima Gosu Gosu awe ameuawa.Devotha

umewasiliana naye? Akauliza Edwin

“Hapana hajanipigia simu.Mara nyingi yeye hunitafuta kutaka kujua kila kinachoendelea huku lakini nashangaa mpaka muda huu hajanitafuta na siyo kawaida yake” akasema Melanie

“Sawa nitamtafuta nimjulishe kile kinachoendelea” akasema Edwin akaagana na Melanie akaingia garini na kabla ya kuondoka akachukua simu akazitafuta namba za Devotha

akampigia lakini simu yake haikupatikana.

“Where are you Devotha?Kwa nini leo hupatikani?akajiuliza Edwin akawasha gari na kuondoka

“Kila kitu kimekamilika kwa ajili ya tukio la kesho.Dr Fabian kama angejua kwamba kesho atakufa angeanza kutubu kuanzia sasa kumuomba Mumgu amsamehe makosa yake kwani sku ya kesho hataimaliza atakuwa amekufa.Nina hasira naye sana Yule jamaa ameniweka kukaimu nafasi kwa miaka

mitatu halafu anakuja kumpa ukurugenzi mtu mwingine kabisa na kuniacha mimi ambaye nimefanya kazi kwa ufanisi mkubwa kwa miaka mitatu.Baada ya kufariki mimi nitaendelea kuwa mkurugenzi kwani Annabel hatarejea tena.Hakuna wa kumrejesha" akawaza na kutabasamu

"Usiku huu nitamuondoa Gosu Gosu na baada ya hapo nitaanza kumsaka Annabel.Lazima naye afe.Kama alivyosema Melanie kwamba Annabel ni mdudu anayetakiwa kufinyangwa

haraka sana kabla hajaleta madhara makubwa”

Edwin aliendelea kuwaza mambo mengi hadi alipofika katika jengo la makao makuu ya SNSA akashuka garini na kuelekea ofisini kwake ambako alipewa taarifa kuhusiana na maandalizi ya mazishi ya Fidelis na vile vile akajulishwa kuhusu kifo cha Edina .Edwin akaonyesha masikitiko makubwa kwa taarifa ile mbaya.Hakupoteza muda akaenda kuzungumza na wafanyakazi

“Ndugu zangu habari za muda huu.Awali ya yote ninapenda kuwashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa mliouonyesha jana hadi tukafanikiwa kumuondoa Annabel ambaye alionekana kushindwa kumudu vyema majukumu yake na hata kupelekea kifo cha mwenzetu Fideli.Tayari suala lake liko kwa Rais analishughulikia na tunasubiri maamuzi yake.Nimetaarifiwa pia kwamba maandalizi ya mazishi ya Fidelis yanaendelea vizuri na kwa mujibu wa wanafamilia

atazikwa kesho kutwa na sisi tutashiriki kikamilifu.

Tukiachana na taarifa hizo za Fidelis,nimepewa tena taarifa nyingine mbaya za kuhuzunisha kwamba mwenzetu,kipenzi chetu,mdogo wetu dada yetu Edina amefariki dunia.Nimestushwa sana na taarifa hizo.Taarifa zinadai amepigwa risasi yeye na mdogo wake.Huu ni ukatili mkubwa sana amefanyiwa huyu mwenzetu.Japokuwa tayari jeshi la polisi linaendela na uchunguzi wa suala hili sisi

pia tunapaswa kufanya uchunguzi kujua nani hasa aliyemuua Edina? Binafsi ninaunganisha kifo cha Edina na kifo cha Fidelis.Nina uhakika vina muunganiko na aliyesababisha kifo cha Fidelis ndiye aliyemuua Edina.Tutaandaa timu ya kufanya uchunguzi wa kina kuhusu jambo hili.Hili ni pigo lingine kubwa tunalipata ndani ya kindi kifupi hta hivyo hatupaswi kukata tamaa.Tutaendelea na jukumu letu la ulinzi wa nchi na wale wote wenye lengo la

kutukwamisha hawatafanikiwa”Edwin akanyamaza kidogo halafu akaendelea

“Jambo la tatu ninalotaka kuwajulisheni ni kwamba ninaliondoa rasmi mezani suala la Khalid Sultan Khalid lililoletwa na Annabel.Mpaka sasa hatuna ushahidi wowote wa kutosha kuhusiana na huyu mtu ambaye tuliagizwa kumfuatilia.Annabel akipaswa kutupa uthibitsho usio na shaka kuhusiana na uhatari wa huyu mtu kwa nchi yetu.Hatutaendelea tena

kupoteza muda kumtafuta Khalid ambaye hatuna uhakika kama ni gaidi hadi hapo Annabel kama atabahatika kurejea atupe uthibitisho kwamba kweli mtu huyu ni gaidi kutoka IS hivyo kuanzia sasa hakuna mtu yeyote kuendelea na suala lile nimeliondoa rasmi" akasema Edwin na kutoa maelekezo kadhaa akarejea ofisini kwake ambako vijana wawili ambao aliwatuma kufanya uchunguzi hospitali kutafuta namna ya kumuua Gosu Gosu wakamfuata

“Victor naamini kazi niliyowatuma mmeikamilisha” akasema Edwin

“Mkuu ile kazi haijakamilika kw……..

“Kwa nini haijakamilika wakati niliwaambia kwamba ni kazi ya muhimu? Akauliza Edwin kwa ukali

“Mkuu kuna jambo limejitokeza ndiyo maana tulishindwa kuikamilisha kazi uliyotutuma” akasema Victor

“Nini kimetokea?akauliza Edwin

“Gosu Gosu hayupo hospitali amehamishwa”

“Amehamishwa?! Edwin akashangaa

“Ndiyo mkuu amehamishwa.Hayupo pale hospitali”

Edwin akavuta pumzi ndefu na kuwatazama vijana wake akauliza

“Amehamishiwa wapi?akauliza

“Hatujui mkuu”

Edwin akagonga meza kwa hasira

“Kwa nini msijue amehamishiwa wapi?

“Mkuu hilo jambo limefanywa kwa siri kubwa na

hata wafanyakazi wa hospitali hawajui mahala alikohamishiwa Gosu Gosu.Kwa mujibu wa watu tuliowahoji ni kwamba lilifika gari la wagonjwa ambalo si la hospitali ile na Gosu Gosu akatolewa katika wodi akaingiwa garini likaondoka bila taarifa kwamba linaelekea wapi lakini tulipata maelezo kwamba kabla ya kuondolewa hospitali daktari anayejulikana kama Dr Masawe alikuwa na mazungumzo na watu Fulani wawili ofisini kwake halafu baada ya muda likafika hilo

gari Gosu Gosu akahamishwa na huyo daktari na wengine wawili pamoja na wauguzi wawili waliondoka na gari lingine na tunadhani walilifuata lile gari lililombeba Gosu Gosu.Tumefuatilia hospitali mbali mbali kubwa lakini hajapelekwa huko” akasema Victor na Edwin akashika kichwa .

“Walifahamu Gosu Gosu yuko hatarini kuuawa ndiyo maana wameamua kumtoa pale hospitali na kumpeleka mafichoni.Wamempeleka wapi? Akajiuliza Edwin

“Mkuu kutokana na uchunguzi wetu inaonekana huyo Dr Masawe kuna kitu anakifahamu kuhusu kuhamishwa kwa Gosu Gosu na kama tukimpata tunaweza kufahamu alikopelekwa mgonjwa.Tulikwenda mbali zaidi na kufahamu hadi mahala anakoishi huyo Dr Masawe lakini hatukuweza kufanya chochote tukisubiri maelekezo yako”akasema Victor

“Good.Kazi nzuri sana mmeifanya.Kama tayari mmefanikiwa kufahamu

mahala anakosihi Dr Masawe itakuwa rahisi sana kwetu kufahamu mahala alipo Gosu Gosu" akasema Edwin na kuwaelekeza wale vijana kwenda kujiandaa

"Kwa namna yoyote ile lazima Gosu Gosu apatikane na auawe.Lile tayari ni bomu na linaweza kulipuka muda wowote hivyo lazima tulitegue haraka sana.Melanie alifanya kosa kubwa kuanzisha mahusiano na mtu kama Yule na sasa inatugharimu kuanza kumuwinda" akawaza Edwin

na kumuita dereva wake ambaye alifika mara moja

“Jackson kuna kazi ambayo nataka nikupe ikaisimamie na kuhakikisha inakamilika” akasema Edwin na kumuelekeza Jackson kuhusiana na zoezi lile la kumuua Gosu Gosu na akamtaka ahakikishe anaipata familia nzima ya Dr Masawe.Baada ya maelekezo yale Jackson na vijana wengine watatu wakaondoka kuelekea nyumbani kwa Dr Masawe.

****

Tangu alipotolewa hospitali na kuletwa katika nyumba ambayo Mathew aliiandaa,hali ya Gosu Gosu bado iliendelea kuwa mbaya.Alipoteza fahamu wakati wa zoezi la kumuhamisha kumtoa hospitali na hadi giza linangia hakuwa amerejewa na fahamu.

“Mathew lengo lako la kumtoa Gosu Gosu kule hospitali na kumleta hapa ni zuri sana kwa ajili ya usalama wake lakini kwa hali hii

aliyonayo nasikitika kusema kwamba tutalazimika kumrejesha tena hospitali akafanyiwe uchunguzi zaidi.Hapa hatuna vifaa vya kuweza kumfanyia uchunguzi kufahamu nini hasa tatizo lake” Dr Masawe akamueleza Mathew.

“Dr Masawe naomba unieleze ukweli kuhusu Gosu Gosu.Is he going to make it?akauliza Mathew

“I don’t know Mathew.Hali ya Gosu Gosu inatuchanganya sana ndiyo maana ninashauri tumrejeshe tena hospitali kwa

ajili ya uchunguzi zaidi.Kwa hali yake ilivyokuwa hakupaswa kuhamishwa kuletwa hapa.Kama ni usalama wake tutatumia walinzi au tutaomba msaada wa jeshi la polisi kumlinda isitoshe ana mahusiano na Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania tukimueleza hali halisi anaweza akatupa msaada.Kuendelea kumuweka hapa Gosu Gosu ni kuhatarisha maisha yake" akasema Dr Masawe.Mathew akainamisha kichwa akazama mawazoni.

“Mathew umejitahidi sana kuhakikisha mwenzako anakuwa salama lakini kwa hapa ilipofika hakuna namna lazima arudi hospitali” akaendelea kusisitiza Dr Masawe.

“Ahsante kwa ushauri wako Dr Masawe lakini hapana.Gosu Gosu ataendelea kukaa hapa hapa.Hatarejea tena hospitali.Endeleeni kumuhudumia hapa hapa na kama ni kupoteza maisha apoteze maisha akiwa hapa ndani kwa amri ya Mungu na

si binadamu mwingine kuitoa roho yake” akasema Mathew

“Mathew mimi ni daktari na ninashauri Gosu Gosu arejeshwe hospitali ili tuweze kuokao maisha yake.Tafadhali sana” akasema Dr Masawe

“Dr Masawe nimeigeuza nyumba hii hospitali kwa ajili ya Gosu Gosu.Nimenunua kila kifaa ulichokiorodhesha kwa ajili ya kumsaidia Gosu Gosu akiwa hapa hivyo ataendelea kupatiwa matibabu hapa hapa na hatakwenda tena sehemu yoyote.Endeleeni kumuhudumia kwa kila uwezo

mlio nao na kama akipoteza maisha itakuwa ni amri ya Mungu.Hakuna tena mjadala katika hilo Dr Masawe ! akasema Mathew

“Mathew nafahamu umetumia gharama kubwa sana kununua mashine na vifaa mbali mbali kwa ajili ya kumsaidia Gosu Gosu lakini bado ushauri wangu uko pale pale kwamba tunatakiwa kumrejesha hospitali.Yawezekana waliokuwa wanataka kumuua wamekwisha fika hospitali na kugundua amehamishwa na

hawajui mahala alipo hivyo wataachana na zoezi hilo”

“You don’t know anything Dr Masawe” akasema Mathew na kutoka sebuleni akaenda katika chumba alimokuwa amelazwa Gosu Gosu akawakuta madaktari wengine wawili na wauguzi wakiwa wamesimama wanamtazama Gosu Gosu.Akamsogelea karibu

“Gosu Gosu nimefanya maamuzi magumu kukuhamisha kutoka hospitali kukuleta hapa ambako naamini ni sehemu

salama.Siogopi kutumia hadi shilingi ya mwisho kuhakikisha unakuwa salama.I hope you are going to wake up soon brother ” akawaza Mathew huku akimtazama GosuGosu halafu akatoka mle chumbani akaenda katika chumba alimolazwa Austin ambaye naye alihamishwa hospitali na hali yake ilikuwa inaendelea vizuri akamueleza kile kinachoendelea

“It’s a taugh call Mathew but it’s the right one.Mathew ahsante sana kwa maamuzi haya uliyoyafanya ya

kuhakikisha tunakuwa salama kwa kutuleta hapa.Pale hospitali chochote kingeweza kutokea.Hawa watu lazima wangefanya kila juhudi kuhakikisha tunauawa.Mathew wewe ni kaka yet…….” Austin akanyamaza baada ya Ruby kuingia mle ndani kwa kasi na kuwastua sana

“Kuna nini Ruby?akauliza Mathew

“Dr Masawe” akasema Ruby

“Kafanya nini?Mathew akauliza

“Wakati tunaendelea na maongezi amepigiwa simu na mtu halafua kafungua kitu kama video katika simu yake na sura yake ikabadilika ghafla kisha akanitaka nikamfungulie geti kuna mahala anaelekea.Ameondoka kwa kasi ya ajabu” akasema Melanie

“What’s going on?Hajakueleza chochote?akauliza Mathew

“Hapana hajaniuliza chochote” akajibu Ruby.Mathew akajaribu

kumpigia lakini hakupokea simu.

“Hapokei simu yawezekana amepata taarifa mbaya za mgonjwa na anamuwahi” akasema Mathew

“Kwa mstuko alioupata baada ya kutazama ile video katika simu yake pokea ile simu na kwa namna alivyoondoka sina hakika kama anamuwahi mgonjwa.Halafu hata kama angekuwa anamuwahi mgonjwa lazima angetueleza lakini ameondoka kimya kimya bila kusema

chochote.Something is not right” akasema Ruby

“Usihofu Ruby kama kuna kitu kibaya Dr Masawe atatueleza” akasema Mathew huku akitazama saa yake

“Austin sisi tunaondoka.Usiku wa leo tunavamia ofisi za SNSA.Ninahitaji kumpata Edwin Mbeko usiku wa leo.Madaktari wako hapa na wauguzi wanaendelea kumtazama Gosu Gosu.Natamani tungekuwepo na sisi pamoja nanyi lakini tuna kazi nyingine kubwa ya

kufanya.Ni kazi ngumu na ya hatari kutokana na ulinzi mkali uliopo SNSA lakini nakuahidi tutarejea salama" akasema Mathew

"Ninaelewa Mathew.Ninawatakia kila la heri.Hakikisheni mnampata huyo Edwin" akasema Austin.Mathew akachomoa bastora na kumpa.

"Kama likitokea tatizo lolote kabla hatujarejea please save yourself and Gosu Gosu too" akasema Mathew kisha wakatoka na kwenda kuwaaga wale madaktari

wanaomuhudumia Gosu Gosu na kuwakuta wakijadiliana kuhusiana na namna Dr Masawe alivyoondoka.Mathew akawaaga kwamba wanaondoka na watarejea baadae wakaingia garini na kuondoka.

“Mathew I’m scared.Tunaondoka wakati hali ya Gosu Gosu ni mbaya”akasema Ruby

“Tunahitaji kuwa majasiri sana wakati huu.Kama hali ya Gosu Gosu ingekuwa inaruhusu kusafirishwa kwenda nje ya nchi tungefanya

hivyo lakini kwa hali yake hatuwezi kumsafirisha na kule hospitali hatuwezi kumrejesha tena kwa sababu za kiusalama.Kilichobaki hapa ni kumkabidhi Mungu suala hili yeye ndiye mwamuzi wa yote akiamua kumchukua Gosu Gosu sisi hatupaswi kulalamika.Naamini Mungu anaona mawazo yetu na anasikia maombi yetu hivyo atamponya Gosu Gosu” akasema Mathew

****

“Ruby hii ni misheni ya hatari sana hivyo hatutaongozana wote.Nitakwenda peke yangu wewe utabaki hapa ukiniongoza” akasema Mathew wakiwa katika ofisi ya nyumbani kwake

“Sawa Mathew nitajiunga na SNSA nitakuongoza hadi kufika katika ofisi ya Edwin.Hata kama hatakuwepo ofisini lakini unaweza ukafanikiwa kupata kitu ambacho kinaweza kutusaidia

kufahamu kwa kina mahusiano yake na Devotha na vile vile tujue kama ana mahusiano na Melanie Davis” akasema Ruby

“Kitu cha kwanza ninachokitaka baada ya kuvuka geti kuu ni kuzima umeme.Kukiwa giza nitaweza kuingia kwa urahisi zaidi ndani”

“Kuna chumba maalum ambacho kina kila kitu kinachohusiana na umeme wa jengo lile na ndani ya chumba hicho kuna jenereta la dharura pindi umeme

ukikatika.Unapoingia katika maegesho ya viongozi mkono wako wa kulia utaiona nyumba ina madirisha makubwa na nyumba hiyo ndiyo ina jenereta na vifaa vyote vya umeme wa jengo” akasema Ruby huku akiendelea kubofya kompyuta yake

“I’m in” akasema Ruby kisha ramani ya jengo la makao makuu ya SNSA ikaonekana katika kompyuta yake akaihamishia katika runinga kubwa ukutani

“Hii ndiyo ramani ya jengo la makao makuu ya SNSA.Ile

nyumba ninayokwambia ilimo jenereta ya umeme haiko katika ramani hii kwa sababu haina muda mrefu toka imejengwa.Utakapozima umeme utaelekea katika maegesho ya viongozi na utatumia mlango huu wa maegesho ya viongozi kuingia ndani ya jengo. Umeme unapokatika jenereta huwaka baada ya dakika moja lakini nitabadilisha katika mfumo ili liwake baada ya dakika tatu.Nitafanya hivi ili uweze kutumia muda huo kuufungua mlango wa kuingilia ndani

kupitia maegesho ambao hufunguliwa kwa kadi maalum lakini wewe utatumia vifaa vyako kuufungua mlango huo . Ukishaingia ndani ya jengo hilo umeme utawaka na utapita njia hii hapa ambayo ni njia ya dharura ya kupita viongozi endapo kutatokea dharura yoyote aidha ya moto au kitu chochote cha hatari.Utakutana na mlango ambao namba zake za kufungulia ni KW23T860.Ukifungua huo mlango itaonekana katika mfumo wao hivyo ukiufungua

na kuingia ndani utabonyeza namba TTY79 na itajulikana ni mmoja wa watu wa idara ya SNSA.Utaelekea hadi ghorofa ya tano ambako ndiko ziliko ofisi zetu.Nitakuunganisha na kompyuta hii ili niwe nakuona na kukupa maelekezo njia ya kupita kuelekea katika ofisi ya Edwin” akasema Ruby.

Mathew akatoka na kuelekea katika chumba chake ambacho kulikuwa na silaha na vifaa vingine mbali mbali akaanza kujiandaa.Alipokuwa tayari akarejea ofisini alikomuacha Ruby.

“Mathew umevaa kikomando hasa” akasema Ruby

“Ni kutokana na ulinzi uliopo mahala hapo ninakoelekea ndiyo maana nimejiandaa kiasi hiki”akasema Mathew na kuweka mezani kifaa Fulani kama boksi akakifungua na kukiwasha halafu akachukua kidude kidogo na kukiweka sikioni

“Huu ni mtambo mdogo kwa ajili ya mawasiliano.Kuna dishi kubwa la satelaiti liko nje ya nyumba ambalo ni maalum

kwa ajili ya kifaa hiki ambacho ndicho tutatumia kwa mawasiliano.” akasema Mathew na kufanya majaribio na kifaa kile kilifanya kazi vizuri

“Mathew hakikisha unafanikiwa kumpata Edwin.Ni mtu ambaye tunamuhitaji sana”akasema Ruby

“Usijali Ruby nitatumia kila uwezo nilio nao kuhakikisha Edwin anapatikana usiku huu” akasema Mathew wakakumbatiana

“Mathew please be safe ! akasema Ruby na Mathew akachukua begi lake akalivaa mgongoni akaelekea katika gari na kuondoka.

****

“Ee Mungu naomba usimame na familia yangu ili hao waliowateka wasiwafanyie kitu chochote kibaya” Dr Godwin Masawe alimuomba Mungu.

Alipokuwa nyumbani kwa Mathew akizungumza na Ruby alipigiwa simu na mtu

asiyemfahamu akamtaka atazame video atakayomtumia na alipoitazama video aliyotumiwa aliwaona mke na watoto wake wakiwa wamefungwa mikono huku wamepigishwa magoti na watu wawili waliofunika nyuso zao wakiwa na bunduki wakiwalinda.Mtu Yule aliyempigia simu alimtaka awashe gari na aondoke mahala alipo aende nyumbani kwake na asithubutu kuwajulisha polisi au mtu yeyote kuhusu tukio lile.Hii ndiyo sababu iliyomfanya Dr

Masawe kuondoka kimya kimya nyumbani kwa Mathew bila kuaga mtu yeyote.

“Nani hawa walioteka familia yangu? Nini wanakitaka hadi wakafanya hivi?akajiuliza maswali mengi

Dr Masawe alifika nyumbani kwake akapiga honi lakini hakuna aliyetoka kumfungulia geti akalazimka kushuka garini akaenda taratibu na kulisukuma geti halikuwa limefungwa akaingiza gari ndani.Akashuka kwa tahadhari na kuingia ndani akamuita mke wake

lakini hakukuwa na dalili zozote za kuwepo mtu mle ndani.Ni sauti ya runinga ndiyo iliyosikika sebuleni.Akaizima na kisha akaanza kuingia chumba kimoja baada ya kingine lakini hakukuwa na mtu yeyote mle ndani.Dr Masawe akachanganyikiwa.

“Hawa watu wanataka nini kwangu?Wamewapeleka wapi familia yangu? Akajuliza akiwa amesimama ameegemea mlango wa chumba chake cha kulala

“Natamani niwajulishe polisi lakini naogopa wale jamaa wanaweza wakaidhuru familia yangu kwani walinionya nisithubutu kuwaambia chochote polisi” akawaza na kuelekea chumbani kwake akafungua kasiki lake akaanza kuhesabu fedha zilizopo.

“Nahisi hawa jamaa wanahitaji fedha ndiyo maana wakateka familia yangu.Hapa nina jumla ya shilingi milioni thelathini na saba na kama wakihitaji zaidi nitajitahidi kukopa sehemu yoyote kwa

ajili ya kuikomboa familia yangu” akawaza Dr Masawe na mara simu yake ikaita.Akatazama mpigaji akahisi mwili unamtetemeka kwani zilikuwa ni namba za Yule jamaa mtekaji

“Hallow” akasema kwa woga

“Dr masawe kuna mtu anakuja hapo nyumbani kwako kukuchukua. Ndani ya dakika tano mtu huyo atakuwa amefika. Ninapokata simu hii zima simu yako tafadhali.” akasema Yule jamaa

“Nini unakitak…..” akasema Dr Masawe lakini Yule mtekaji alikata simu.Kijasho kilimtoka Dr Masawe usoni.Akaizima simu yake kama alivyoelekezwa akaelekea sebuleni.Baada ya dakika tano kama alivyokuwa ameelekezwa mlango wa sebuleni ukagongwa

“Nahisi huyo ndiye mtu aliyetumwa kuja kunichukua” akawaza na kutoka akakutana na mtu mmoja aliyevaa suti nyeusi na mkononi akiwa na bastora .Dr Masawe akatetemeka

“Funga nyumba yako ! akaelekeza Yule jamaa na Dr Masawe akafunga nyumba Yule jamaa akamtaka amfuate wakatoka nje ya geti ambako Yule jamaa alikuwa ameegesha gari lake.Akamfungulia mlango Dr Masawe akaingia garini halafu akamfunga kitambaa usoni na safari ikaanza

Dr Masawe hakujua mahala anakopelekwa.Baada ya mzunguko wa dakika kadhaa gari lile likasimama na mlango ukafunguliwa Dr Masawe akashushwa garini

akashikwa mkono akaongozwa kuelekea ndani ya jengo kisha wakaingia katika lifti baada ya muda milango ya lifti ikafunguka wakatoka wakatembea kwa muda mfupi mlango wa chumba ukafunguliwa Dr Masawe akaingizwa ndani akakalishwa katika kiti akafungwa mikono kwa pingu zilizokuwa katika meza halafu mlango ukafungwa akabaki peke yake

“Ee Mungu naomba unisaidie mimi na familia yangu tuwe salama.Watu hawa hawaonekani kuwa watu

wazuri na wana lengo baya nasi” akaomba Dr Masawe

Zilipita dakika kadhaa mlango ukafunguliwa tena na watu wakaingia ndani ya kile chumba Dr Masawe akavuliwa kitambaa usoni .Mle ndani ya chumba kulikuwa na watu wanne mmoja ndiye aliyekuwa amekaa kitini wengine wamesimama.

“Hallow Dr Masawe pole sana kwa mstuko ulioupata.Mimi naitwa Edwin Mbeko ni mkurugenzi wa idara ya SNSA yaani idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi”

akasema Yule jamaa aliyekuwa amekaa kitini.DrMasawe hakuweza kujibu chochote alikuwa anatetemeka

“Relax Dr Masawe.Take a deep breath” akasema Edwin kisha akaamuru Dr Masawe afunguliwe zile pingu mikononi.

“Usiogope Dr Masawe uko hapa kwa jambo dogo tu kisha utaondoka na familia yako” akasema Edwin

“Familia yangu wako wapi? Akauliza Dr Masawe

“Usihofu Dr Masawe.Familia yako iko

salama ! akasema Edwin akachukua kitanza mbali akakielekeza katika ukuta wa kioo akakibonyeza na rangi ya kioo ikabadilika na upande wa pili familia ya Dr Masawe wakaonekana wakiwa wamekaa sofani.Mke wake akiwa amewakumbatia watoto wake.Yule jamaa akabonyeza tena kitanza mbali na rangi ya kioo ikabadilika na kuzuia watu waliokuwa upande wa pili kuonekana.

“Ahsante Mungu familia yangu wako salama” Dr

Masawe akashukuru kimya kimya

“Tayari umewaona familia yako wote wako salama na muda mfupi ujao utaondoka nao” akasema Edwin

“Nini mnakitaka kutoka kwangu?akauliza Dr Masawe

“Kuna kitu kidogo sana Dr Masawe ninachokihitaji kutoka kwako.Ni taarifa ndogo tu na ukinipatia hiyo basi familia yako watakuwa salama na utaondoka nao sasa hivi” akasema Edwin

“Niambieni tafadhali mnachokihitaji niwapatie

kama ni fedha niko tayari kuwapa kiasi chochote kile mnachokihitaji ili mradi msiidhuru familia yangu” akaomba Dr Masawe.

“Kuna mgonjwa mmoja anaitwa Papi Gosu Gosu alikuwa amelazwa katika hospitali ya Mtodora akipatiwa matibabu baada ya kushambuliwa kwa risasi na watu wasiojulikana.Mgonjwa huyo amehamishwa leo kutoka hospitalini hapo na kupelekwa kusikojulikana.Ninachokihaji kutoka kwako ni kunieleza mahala aliko Gosu

Gosu.Ukijibu hilo ninakuhakikishia wewe na familia yako mtaondoka hapa salama” Edwin akanyamaza na kumtazama Dr Masawe

“Wapi alipo Gosu Gosu?akauliza Edwin

“Hili ni jaribu kubwa sana.Yawezekana hawa jamaa ndio wanaotaka kumuua Gosu Gosu” akawaza Dr Masawe

“Dr Masawe wapi alipo Gosu Gosu?Nieleze tafadhali ili tuokoe muda na uondoke hapa na familia yako”

“Sifahamu mahala aliko huyo mgonjwa” akajibu Dr

Masawe na Edwin akamtazama halafu akatabasamu

“Una uhakika Dr Masawe hufahamu mahala alipo Gosu Gosu?akauliza Edwin

“Ni kweli sifahamu mahala alipo Gosu Gosu.Kama ningejua mahala alipo ningewaeleza” akajibu Dr Masawe

“Dr Masawe tunafahamu Gosu Gosu amehamishwa leo kutoka hospitali ya Mtodora na wewe ukiwa na madaktari wengine wawili na wauguzi wawili mliongozana naye

kwenda mahala alikohamishiwa ili kuendelea kumpatia matibabu.Nataka unieleze mahala alikopelekwa Gosu Gosu.Yule mtu ni hatari sana kwa usalama wa nchi”

“Sifahamu alikohamishiwa Gosu Gosu na wala sikuongozana na waliomuhamisha” akasema Dr Masawe

“Dr Masawe ninakuheshimu sana mzee wangu na sitaki kukufanyia jambo lolote baya.Ninakuuliza kwa upole kabisa wapi alipo Gosu Gosu?Nieleze tafadhali

uondoke haraka na familia yako”

“Sifahamu kwa kweli alipo huyo Gosu Gosu” akajibu Dr Masawe.Edwin akamtazama kisha akawasha sigara akavuta na kupuliza moshi halafu akasema

“Kwa nini unaficha mahala alipo Gosu Gosu.Ana umuhimu gani kwako?

“Simfichi ila sifahamu mahala alipo.Mnataka kumuua amewakosea nini? Akauliza Dr Masawe na kwa kasi ya umeme Edwin akainuka na kumlamba kofi zito Dr Masawe

“Huna ruhusa ya kuuliza swali lolote hapa.Nimekuuliza swali jibu haraka sana na si kuniuliza swali.Nakuuliza kwa mara ya mwisho wapi alipo Gosu Gosu? Ukishindwa kunijibu nitaanza kuitesa familia yako huku ukishuhudia ! akasema kwa ukali Edwin ambaye sura yake ilikuwa imebadilika na kuonyesha ukatili mkubwa

“Wapi alipo Gosu Gosu?akauliza lakini Dr Masawe hakujibu kitu.Edwin akasimama

“Dr Masawe hujanifahamu vyema mimi ni nani.Sasa umenilazimisha nifanye kitu ambacho sikuwa nimetarajia kukifanya ! akasema na kuelekeza kitanza mbali katika kioo akabonyeza na familia ya Dr Masawe ikaonekana.

“Binti yako ana umri wa miaka mingapi? Akauliza

“Tafadhali naomba msiwaguse familia yangu ! Kama ni kunitesa niteseni mimi ! akasema Dr Masawe na kulambwa tena kofi zito

“Niambie binti yako ana miaka mingapi? Akauliza

“Ana miaka kumi na mbili”

“Sawa.Leo hii tunampatia mchumba hapa na kwa mara ya kwanza ataingiliwa kimwili huku ukishuhudia” akasema Edwin na Dr Masawe akasimama

“Nasema msimguse binti yangu tafadh…” hakumaliza sentensi yake akapigwa ngumi iliyompeleka chini.Damu zilianza kumtoka mdomoni.Akainuliwa akatolewa mle ndani na kuingizwa katika chumba walichokuwamo familia yake ambao waliangua kilio

walipomuona baba yao.Edwin akawanyamazisha halafu akamfuata binti wa Dr Masawe

“Binti unaitwa nani?akauliza Edwin

“Naitwa Paulina” akajibu Yule binti huku akitetemeka.Edwin akamshika mkono na kumtaka ainuke akampeleka katika kiti akamtaka aketi

“DrMasawe hii ni mara ya mwisho ninakuuliza wapi alipo Gosu Gosu?

“Tafadhalini jamani naomba binti yangu mumuache kwani hahusiki

kwa namna yoyote na suala hili.Nitawasaidia kutafuta taarifa za mahala aliko huyo mtu mnayemtafuta lakini nawaomba msimguse binti yangu ! akasema Dr Masawe

“Dr Masawe wapi alipo Gosu Gosu? Akauliza Edwin

“Naombeni mniamini vijana wagu sifahamu mahala alipo Gosu Gosu.Kama ningefahamu ningewaeleza lakini sijui chochote ! akasema Dr Masawe

“Unatulazimisha tufanye ukatili ambao hatukuwa tumetegemea kuufanya !

akasema Edwin na kuwapa ishara watu wake.Jamaa wawili waliojazia miili yao wakamshika Paulina binti wa Dr Masawe na kumpandisha juu ya meza.Alikuwa analia.

“Dr Masawe fursa ya mwisho wapi alipo Gosu Gosu?

“Naombeni jamani muacheni binti yangu hana mahusiano yoyote na suala hili.Ninawaahidi nitawasaidia kutafuta mahala alipo Gosu Gosu ! akasema Masawe aliyekuwa amefungwa pingu mikononi

“Mume wangu kama unafahamu hicho wanachokuuliza wajibu tafadhali ili kumuepusha binti yetu na ukatili ambao anakwenda kufanyiwa na hawa watu! akasema mke wa Dr Masawe huku akitokwa na machozi

“Sifahamu mke wangu mahala alipo huyo mtu wanayemtaka.Kama ningejua mahala alipo ningewaeleza ! akasema Dr Masawe.Edwin akawaelekeza watu wake kuendelea na zoezi.Kwa kutumia nguvu Paulina

akavuliwa gauni alilokuwa amevaa akabaki mtupu.Alikuwa anapiga kelele kubwa.Dr Masawe na mke wake walikuwa wamedhibitiwa na watu wenye silaha ili wasiweze kufanya chochote.Mmoja wa wale jamaa waliojazia miili yao akavua suruali yake bila aibu na kuutoa uume wake uliosimama.

“Nitawaeleza ! Nitawaeleza ! Nitawaeleza ! akasema Dr Masawe

“Unasemaje Dr Masawe ? akauliza Edwin

“Nitawaeleza mahala alipo Gosu Gosu.Tafadhali naombeni msimfanye chochote binti yangu” akasema Dr Masawe na Edwin akaelekeza wale jamaa wamuache Paulina kisha Dr Masawe akatolewa ndani ya kile chumba akarejeshwa katika chumba alichokuwamo awali.

****

Mathew Mulumbi alikaribia kufika katika geti kuu la kuingilia ofisi za SNSA.

“Ruby tayari ninalitazama geti kuu la SNSA” Mathew akamwambia Ruby

“Good.Ninakuona na tayari nimekwisha cheza na kamera zote zilizoelekezwa eneo la geti kuu.You have two minutes to finish the main gate” akasema Ruby

“Thank you Ruby” akajibu Mathew na kupunguza mwendo baada ya kukutana na kibao kilichomuelekeza afanye hivyo.Alipolikaribia geti kuu akakutana na kibao kingine kilichomtaka asimame kwa ajili ya ukaguzi.Jamaa mmoja

aliyevaa sare za ulinzi za rangi nyeusi akasogelea kioo Mathew akakishusha

“Habari yako ndugu” akasalimu Yule mlinzi

“Nzuri ndugu yangu”

“Nikusaidie nini?

“Mimi ni mgeni wa Edwin Mbeko yuko ndani? Akauliza Mathew

“Mathew kuna walinzi wengine watatu wako hapo getini” Ruby akamwambia Mathew kupitia kile kifaa alichokiweka sikioni

Yule mlinzi akamtaka Mathew asubiri kidogo ili

akawasiliane na Edwin Mbeko alipogeuka tu mkono wa Mathew ulikuwa mwepesi ukanyanyuka kwa kasi ya aina yake na kwa kutumia bastora yenye kiwambo cha sauti akamlenga Yule jamaa risasi akaanguka chini kisha kama nyani akashuka kutoka ndani ya gari lile na kuelekea katika nyumba ya walinzi na kama alivyoelekezwa na Ruby kulikuwa na walinzi watatu.Mathew alicheza na bastora yake kama vile ana mikono minne na ndani ya sekunde chache wale walinzi

wote wakawa sakafuni wakivuja damu

“I’m sorry guys wakubwa wenu ambao wanashirikiana na magaidi wamesababisha mkafikwa na masahibu haya” akasema Mathew huku akiwavuta walinzi wale na kuwaingiza katika chumba kidogo cha mapumziko

“Mathew you have 10 seconds to get out of there ! Ruby akamuelekeza Mathew ambaye aliingia katika gari lake na kutoka mahala alipo Ruby akalifungua geti na Mathew akapita.Moja kwa

moja akaelekea sehemu ya maegesho ya viongozi wa idara.Kabla hajashuka garini akalitazama eneo lile kama lina mlinzi yeyote halafu akawasiliana na Ruby

“Tayari niko eneo la maegesho ninataka kutoka garini”

“Sawa Mathew unaweza kutoka.Hakuna hatari yoyote eneo hilo” akasema Ruby na Mathew akafungua mlango wa gari akashuka akachukua begi lake akalivaa mgongoni bila kusahau kofia yake ngumu ambayo ilifungwa miwani ya

kumuwezesha kuona sehemu yenye giza.Moja kwa moja akaelekea katika jengo ambalo ndimo mna vifaa vyote vya umeme pamoja na jenereta la dharura pale umeme unapokatika.Akalizunguka kwa nyuma jengo lile halafu akatoa mkasi mgumu akakata kipande cha wavu akapenya na kuingia ndani.Akaelekea moja kwa moja katika sehemu ya kukatia umeme akachukua kifaa Fulani kutoka katika begi lake akakiweka katika sanduku kubwa la umeme na baada ya sekunde chache kukatokea

cheche kubwa na jengo zima umeme ukakatika kisha akatoka kwa kasi kupitia mahala alikoingilia akaelekea upande ule wa maegesho ya magari akachomoa vifaa kutoka mfukoni na kuuchokonoa mlango ukafunguka akaingia ndani.Kulikuwa na giza lakini aliweza kuona kutokana na ile miwani ya kuonea usiku.

“I’m in”Mathew akamwambia Ruby

“Good.Sekunde ishirini na nne umeme utawaka hivyo elekea njia ya kushoto kwako

yenye kibao emergency exit.” Akaelekeza Ruby na Mathew akaanza kupanda ngazi taratibu na kwa tahadhari kubwa.Alisikia kwa mbali watu wakizungumza kutokea nje

Ndani ya chumba alichokuwa anahojiwa Dr Masawe mahojiano yalisimama baada ya umeme kukatika na umeme uliporejea Edwin akatoa simu yake akapiga kwa fundi mkuu

“Masoud kuna nini kimetokea hadi umeme ukakatika na kuchelewa kuwaka?

“Mkuu imetokea hitilafu katika boksi kubwa na kutulazimu kuchepua umeme katika njia nyingine hadi hapo tutakapofahamu chanzo cha hitilafu iliyojitokeza”

“Nakuhitaji ofisini kwangu haraka sana unieleze kwa kina kilichotokea kwani jengo hili halipaswi kukosa umeme zaidi ya dakika mbili kutokana na unyeti wake lakini imechukua zaidi ya dakika tano umeme kurejea” akasema Edwin na kuwaelekeza vijana wake waendelee kumchunga Dr Masawe ili akafahamu

kilichokuwa kimetokea na kusababisha hitilafu ile

Mathew aliufikia mlango alioelekezwa na Ruby akabonyeza namba huku akielekezwa na Ruby lakini zikagoma

“Yawezekana wamebadili namba ! akasema Ruby

“Ruby find me another way ! akasema Mathew

“Nipe sekunde chache Mathew nione kitu cha kufanya” akasema Ruby na kushusha pumzi akaanza kubofya kompyuta yake haraka

haraka na mara simu yake ikaita alikuwa ni Rais

“Oh no ! kwa nini anapiga wakati huu?akasema Ruby kisha akaichukua ile simu na kutoka nje ya kile chumba akaipokea

“Hallo mheshimiwa Rais” akasema Ruby

“Ruby uko wapi ninahitaji kuzungumza nawe usiku wa leo kuhusiana na kile kilichotokea jana kule SNSA.Nielekeze mahala ulipo tafadhali ili nitume watu wangu waje kukuchukua” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais utanisamehe kwani kwa usiku huu haitawezekana.Naomba kama itawezekana tuonane kesho”

“Kesho haitakuwa rahisi kwa upande wangu kwani nitakuwa na kikao muhimu sana na marais wenzangu.Naomba tafadhali tuzungumze usiku huu ili niweze kulimaliza hili swala nahitaji urejee haraka sana SNSA kabla ya hizo siku saba” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais kwa usiku huu haitawezekana kwa

sababu ninamsaidia Mathew Mulumbi kufanikisha misheni ya muhimu sana” akasema Ruby

“Misheni ipi? Naomba unieleze tafadhali.Nataka kufahamu anachokifanya Mathew” akasema Dr Fabian

“Kuna uchunguzi anakwenda kuufanya ndani ya SNSA na mimi ndiye ninayemsaidia ili aweze kufanikisha hilo jambo”

“Umesema Mathew anakwenda kufanya uchunguzi SNSA?

“Ndiyo mheshimiwa Rais”akajibu Ruby

“Anakwenda kuchunguza nini?akauliza Dr Fabian

“Kwa sasa naomba nisikueleze mheshimiwa Rais lakini pale uchunguzi utakapokamilika tutakujulisha” akasema Ruby

“Ruby you have to tell me everything.SNSA ni ofisi iliyo chini yangu natakiwa kujua kila kinachoendelea pale.Nataka kufahamu kitu gani anachokwenda kukichunguza Mathew?Mle kuna siri nyingi za usalama wa

nchi ambazo mtu kama Mathew ambaye si mfanyakazi hapaswi kuzifahamu.Ruby nini kinaendelea?Mara ya kwanza umemuingiza ndani ya SNSA na akashiriki katika tukio la kusababisha kifo cha mmoja wa wafanyakazi na leo anarejea tena kufanya uchunguzi ..!

“Mheshimiwa Rais tafadhali naomba umuamini Mathew.Kuna jambo kubwa linaendelea hapa nchini hivi sasa na pale tukikamilisha uchunguzi tutakujulisha”

“So you are with him !

“Yes Mr President.I’m with him” akajibu Ruby na Dr Fabian akavuta pumzi ndefu

“Ruby ninakuamini sana na ndiyo maana nikakuomba uje uongoze idara nyeti kama ile lakini kwa mambo haya unayoyafanya unanipa wasiwasi wa kuendelea kukuamini.Mathew Mulumbi si mtu wa kumuamini hata kidogo.Hakuna anayejua alikuwa wapi na kwa nini ametokea katika wakati huu.Huyu ni mtu wa kuogopwa sana na kwa namna yoyote ile hukupaswa

kumsaidia kuingia ndani ya ofisi nyeti kama SNSA!

“Mheshimiwa Rais nitazungumza nawe kesho.Sorry ! akasema Ruby na kukata simu akakimbilia ndani akavaa spika za masikioni na kumuita Mathew

“Mathew unanisoma?akauliza Ruby

“Ulikuwa wapi Ruby?! Tayari nimekwisha anza kuingiwa na wasi wasi labda kuna kitu kimekutokea” akasema Mathew

“I’m sorry” akasema Ruby na kuendelea kubonyeza

kompyuta yake kwa kasi kubwa

“Umefikia wapi kunitafutia njia nyingine?

“I’m changing the codes.Ndani ya sekunde chache nitakupa namba mpya za kufungulia huo mlango” akasema Ruby

“Fanya haraka Ruby ! akasema Mathew

Mara tu baada ya Ruby kukata simu Dr Fabian akampigia Edwin Mbeko

“Mheshimiwa Rais ! akasema Edwin

“Edwin uko wapi?akauliza Dr Faban

“Niko ofisini mheshimiwa Rais”

“Kila kitu kiko sawa hapo ofisini?

“Ndiyo mheshimiwa Rais kila kitu kiko sawa kabisa”

“Are you sure?

“Ndiyo mheshimiwa Rais kila kitu kiko sawa kabisa ukiacha yale matukio mawili ya kuwapoteza wafanyakazi wetu ambayo nimekwisha kufahamisha lakini hakuna tena tatizo lingine lolote” akasema Edwin

“Hakuna tukio lolote limetokea hapo ofisini ambalo si la kawaida usiku huu?akauliza Dr Fabian

‘Kilichotokea muda mfupi uliopita ni umeme kukatika na niko hapa na mhandisi wetu wa umeme akinieleza namna tukio lilivyotokea”

“Oh my God ! akasema Dr Fabian

“Kuna nini mheshimiwa Rais?akauliza Edwin

“Edwin kuna mtu tayari yuko ndani ya jengo lenu.Amesaidiwa kuuingia ndani na mtu aliyeko nje

anayelifahamu vizuri jengo hilo na mifumo yake.Sifahamu mtu huyo anakuja kutafuta nini lakini nahisi kuna siri anazitafuta.Tafadhali zima kabisa kila kitu ili mtu huyo asifanikiwe lengo lake na hakikisha anatiwa mikononi na ahojiwe kitu anachokuja kukifanya hapo SNSA” akasema Dr Fabian na Edwin akaonyesha mstuko mkubwa

“Edwin umenisikia?

“Nimekusikia mheshimiwa Rais” akasema Edwin na Rais akakata simu.Edwin akatoka mbio na kuelekea ghorofa ya

tatu ambako kulikuwa na watu wakiendelea na kazi akawataka wazime kila kitu kwa haraka pamoja na kufunga milango yote ya usalama.

Ruby aliyaelekeza macho katika kompyuta yake ambayo iliendelea kuzunguka ikionyesha asilimia themanini na nane ili namba mpya alizoziweka ziweze kutambuliwa na mfumo wa SNSA na Mathew aweze kuufungua mlango.Ilipofika asilimia tisini na saba mara mawasiliano yakakatika ghafla.Ruby akapiga meza kwa

hasira akaendelea kubonyeza kompyuta yake haraka haraka lakini hakuweza kujiunganisha na mfumo wa SNSA

“Bastard ! akasema kwa hasira kisha akavaa spika zake za masikioni

“Mathew we have a problem” akasema

“Nini kimetokea tena Ruby?akauliza Mathew

“Mawasiliano yamekatika ghafla inaonekana wamezima kila kitu.I can’t access anything ! akasema Ruby

“They know I’m here ! akasema Mathew

“Mathew please get out of there ! akasema Ruby

“Hapana Ruby siwezi kurudi.Lazima nimpate Edwin Mbeko.Ninayo ile ramani ya jengo zima uliyonitumia katika simu yangu.I have to do it on my own.Usiendelee kuwasiliana nami kwani wanaweza wakafuatilia mawimbi na wakagundua mahala ulipo ukawa katika hatari.Thank you Ruby let me do this on my own” akasema Mathew na kuchomoa kifaa kile alichokuwa amekivaa sikioni akakikanyaga kanyaga

na kukata kabisa mawasiliano na Ruby

“Wamegunduaje kama niko hapa? Nitafahamu baadae kwa sasa natakiwa kuhakikisha ninafika katika ofisi ya Edwin Mbeko kwa namna yoyote ile” akawaza Mathew na kutoa bomu dogo katika begi lake akaenda kuliweka katika kitasa cha mlango halafu akarudi nyuma hatua tano na kulilenga bomu lile kwa kutumia bastora yake yenye kiwambo cha sauti ukatokea mlipuko na mlango ukasambaratika.Akajibanza katika kona kusikilizia kama

kuna mtu yeyote atajitokeza lakini hakukuwa na mtu yeyote akaanza kupanda ngazi haraka haraka kwa tahadhari kubwa.

Milango yote ya kuingia na kutoka ndani ya jengo la SNSA ilikuwa imezingirwa na walinzi wenye silaha ili kuzuia Mathew asiweze kutoka nje na kutoroka. Wafanyakazi wote wakakusanywa katika chumba kilichotengenezwa maalum kwa nyakati kama hizi kama kutatoea hatari yoyote ya kushambuliwa.Ni chumba kilichotengenewa maalum ambacho kina milango

isiyopenya risasi na kina uwezo wa kuwakinga wafanyakazi dhidi ya shambulio lolote la kibaolojia.

Edwin Mbeko akiwa ameongozana na walinzi wawili wakainga katika chumba kile ambacho wafanyakazi wote walikuwa wamekusanywa.Mara tu alipoingia wafanyakazi wakataka kufahamishwa kile kinachoendelea

“Poleni sana ndugu zangu kwa mstuko mlioupata.Halijawahi kutokea tukio kama hili hapa katika

idara yetu.Kilichotokea ni kwamba nimepokea taarifa muda mfupi uliopita kwamba ndani ya jengo letu kuna mtu amevamia na lengo lake ni kutafuta siri za usalama wa nchi.Baada ya kupata taarifa hiyo ya kustusha hatua ya kwanza ilikuwa ni kuzima kila kitu ili lengo la mtu au watu hao lisifanikiwe.Kama mnavyofahamu humu ndani kuna siri nyingi kuhusiana na usalama wa nchi hivyo basi hatuwezi kuwapa nafasi watu hao ya kufanikisha mipango yao.Ninachowaomba kwa sasa

tuendelee kutulia humu ndani wakati suala hili linashughulikiwa.Tayari kikosi cha makomando wa idara yetu kiko njiani kutoka katika kambi yao wanakuja hapa kwa ajili ya kuhakikisha mtu au watu hao wanadhibitiwa haraka sana" akasema Edwin na simu yake ikaita akaipokea akazungumza na aliyempigia halafu akasema

"Nimetaarifiwa kwamba walinzi wote waliokuwa geti kuu usikuhuu wameuawa na hao watu ndipo wakapata nafasi ya kupita kuingia ndani

ya jengo.Milango yote kwa sasa imefungwa na kuna ulinzi hivyo hawawezi kutoka nje.Ninawahakikishia kwamba tutawapata wote” akasema Edwin

“Mkuu inawezekanaje mtu au watu hao wakaweza kuvamia ofisi zetu bila kujulikana?Kuna kamera kila mahala na kila mtu au gari linalokaribia eneo hili linaonekana na kukaguliwa imezekanaje mtu au watu hao wakaweza kufika hadi geti kuu bila kujulikana? Mmoja wa wafanyakazi akauliza

“Tutalifanyia uchunguzi suala hilo kujua namna mtu huyo alivyoweza kufika hadi geti kuu akaua walinzi na kuingia ndani bila kunaswa na kamera zetu.Tuna mfumo wa kisasa mno na hata mimi ninashangaa kwa nini kamera zetu zimeshindwa kunasa tukio hilo .Tutafanya uchunguzi na kuufahamu ukweli na wote walioshiriki katika suala hili watajulikana na kuchukuliwa hatua kali lakini kwa muda huu kipaumbele kikubwa ni kuhakisha mvamizi au

wavamizi hao wanakamatwa” akasema Edwin

“Mkuu taarifa hii ya kuwapo kwa mvamizi umeipata wapi? Mtu huyo aliyekupa taarifa hii amejuaje kama kuna mtu kavamia jengo letu wakati sisi tuliopo ndani hatufahamu chochote?akauliza mfanyakazi mwingine.

“Si jambo zuri kuweka wazi chanzo cha taarifa lakini katika hili napenda kuweka wazi kuwa taarifa hii nimeipata kutoka wa mheshimiwa Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania

ambaye ofisi hii iko chini yake” akasema Edwin na wote wakabaki na mshangao minong’ono ikaanza kusikika

“Mingong’ono hiyo ni ya kujiuliza Rais amefahamuje kama kuna mtu katuvamia kabla yetu sisi? Hata mimi sifahamu Rais amejuaje lakini baada ya kumtia nguvuni huyo mvamizi wetu nitazungumza na Rais naamini atanipa taarifa kamili ya namna alivyoweza kupata taarifa za huyo mtu” akasema Edwin na ujumbe ukaingia katika simu

yake akausoma halafu akasema

“Ndugu zangu nimetaarifiwa kwamba kikosi cha makomando wetu kinakaribia kufika.Ninakwenda kuwapokea .Kila kitakachoendelea mtajulishwa” akasema Edwin na kutoka mle ndani akawakuta watu wanne nje ya kile chumba wakimsubiri

“Mkuu kumegundulika uwazi mkubwa katika nyumba ya jenereta tunaamini huyo mvamizi alikata wavu na

kuingia ndani kisha akakata umeme.Vile vile tumekuta gari katika maegesho ya wakuu wa idara na tunahisi ni gari lake" akasema mmoja wa wale jamaa.

"Kama gari lake limeonekana upande huo yawezekana ameingia ndani kupitia njia ya dharura ya vongozi wa idara ambayo watu wengi hata walio ndani ya idara hawaifahamu.Huyu mtu anaonekana kulifahamu sana jengo hili ama kuna mtu ambaye anashirikiana naye"

akasema Edwin na mlio wa helkopta ukasikika

“Makomando wamefika nahitaji kuwapokea” akasema Edwin kisha akaongozana na walinzi wawili wakaelekea ghorofani kwa ajili ya kuwapokea makomando hao ambao hutumiwa na SNSA katika operesheni kubwa na za hatari kwa usalama wa nchi.

“Ni nani huyu mtu aliyethubutu kuvamia ofisi zetu.Kitu gani anakitafuta?Halafu anaonekana kulifahamu vyema jengo hili je kuna watu wa

humu ndani ya idara anashirikiana nao? Akajiuliza Edwin huku wakipanda ngazi haraka haraka kuelekea juu ya jengo.

Helkopta iliyowaleta makomando ilisimama juu ya jengo la SNSA makomando wakaanza kushuka kwa kutumia kamba.Jumla ya makomando nane waliojihami vilivyo wakashuka kiongozi wao akasalimiana na Edwin kisha wakaelekea katika ofisi na Edwin akawaeleza kile kilichotokea na kupelekea kuwaita pale.Akawafahamisha

kwamba wanahisi mvamizi huyo anaweza kuwa amejificha katika njia ya dharura

Makomando waligawanyika katika vikosi viwili vya watu wanne kikosi kimoja kikashuka chini katika mlango wa kuingilia wakuu wa idara ambako ndiko gari la Mathew lilikoonekana kikosi cha pili kikaenda ghorofa ya tano ambako ndiko njia ile ilikuwa inaelekea zilipo ofisi za wakuu wa idara.Kikosi cha makomando wanne walioshuka chini wakiwa na mbwa mkubwa kiliingia katika

njia ile ya dharura na kuanza kupanda juu kwa tahadhari kubwa.Walikuta mlango mkubwa ukiwa umefumuliwa kwa bomu wakawasiliana na wenzao wakawajulisha kisha wakaendelea kupandisha taratibu huku mbwa mkubwa wa kijeshi waliyekuwa naye akiwaongoza kuelekea katika mlango mmoja uliokuwa umefungwa.Kulionekana mchirizi wa damu chini ya mlango.Mbwa Yule akawaongoza kuelekea katika mlango ule ulikotokea mchirizi ule wa damu.Kiongozi wa kile

kikosi akawataka wasimame kisha akatangulia mbele taratibu akiwa katika tahadhari kubwa.Ghafla mbwa akaruka juu na mkanda ukamponyoka yule jamaa aliyekuwa amemshika akakimbia mbio akaurukia mlango ambao haukuwa umefungwa na mara tu mlango ule ulipofunguliwa kukatokea kishindo kidogo na wale makomando wakalala chini.Ndani ya sekunde chache eneo lote likajaa moshi mzito na wale makomando wakaanza kuhisi kuishiwa nguvu na

kushindwa kupumua.Wakati wakihangaika kuvuta pumzi Mathew Mulumbi akajitokeza akiwa amevaa maski usoni ya kumkinga dhidi ya hewa chafu. Mkono wake wa kulia alikuwa ameshika bunduki ndogo na mkono wa kushoto alikuwa na kopo.Alibonyeza lile kopo na kupulizia hewa eneo lile moshi ukatoweka na hewa safi ikapatikana akavua maski yake na akaweza kuwaona vizuri wale makomando waliokuwa wakihangaika kutafuta hewa huku wakiwa hawana nguvu.Haraka haraka

akazikusanya bunduki zao na kuziweka sehemu moja halafu akachukua pingu za plastiki akawafunga kisha akatoa kitu Fulani katika begi lake akaanza kuwapulizia puani na baada ya muda mfupi wakaanza kujihisi vizuri na ndipo walipojikuta wakitazamana na mtu aliyekuwa amewaelekezea bunduki.

“Poleni sana ndugu zangu” akasema Mathew

“Aaaaghh ! akatoa ukelele kiongozi wa kikosi kile akitaka kukata pingu zile za plastiki walizokuwa wamefungwa

“Please don’t do that or I’ll shoot you ! akasema Mathew kwa sauti isiyo na masihara Yule komandoo akamtazama kwa dharau na kutunisha misuli akitaka kukata ile pingu mara risasi mbili zikapita pembeni ya kichwa chake na kupiga ukuta.

“Next time nitakifumua kichwa chako kama utaendelea kuwa mkaidi ! akasema Mathew na Yule jamaa akawa mpole.Mathew akawatazama kwa muda halafu akasema

“Listen to me brothers ! akanyamaza na kuwatazama tena wale jamaa

“Mimi ndiye mnayenitafuta.Naitwa Mathew Mulumbi ni…”

“Mathew Mulumbi ?! Kiongozi wa kile kikosi akastuka

“Ndiyo mimi ni Mathew Mulumbi”

“Unafanya nini hapa Mathew?akauliza Yule jamaa

“Unanifahamu? Mathew akauliza

“Nimezisikia sana habari zako.Ninaye ndugu yangu

anafanya kazi katika idara ya ujasusi ndiye ambaye amenieleza mambo yako mengi.Sikujua kama ni wewe ambaye tumekuja kukutafuta” akasema Yule jamaa huku wenzake wakimshangaa.

“Huyu anaitwa Mathew Mulumbi amewahi kufanya kazi katika idara ya ujasusi Tanzania na mambo aliyoyafanya ni makubwa sana.Ni mmoja kati ya manguli wa ujasusi hapa nchini” Yule kiongozi wa makomando akawafahamisha wenzake

“Aliyosema mwenzenu ni kweli kabisa” Mathew akaongeza

“Kwa nini umevamia jengo hili na kuua watu?Hujui kwamba hilo ni kosa? Tumeambiwa kwamba umeua walinzi wa geti kuu huo tayari ni uhalifu ! akasema mwingine

“Ni kweli niliwaua wale walinzi geti kuu ili nipate nafasi ya kuingia humu ndani kwani bila kufanya vile nisingeweza kuingia humu.Hata ninyi ningeweza kuwamaliza lakini sikufanya hivyo kwa kuwa ninyi ni

wenzangu na mnaweza mkanielewa nikiwaeleza kile kilichonileta hapa”akasema Mathew

“Nini kimekuleta hapa? Unatafuta siri za serikali? akauliza komando mwingine

“Sijaja hapa kuiba siri za serikali na siwezi kufanya hivyo.Niko hapa kwa sababu nyingine ya usalama wa nchi”akasema Mathew

“Usalama wa nchi ndio uvamie ofisi ya serikali na kuua watu?

“Labda niwaeleze kwa ufupi tu pengine mnaweza

mkanielewa.Si muda mrefu sana IS walifanya shambulio hapa Dar es salaam ambalo liliua wake za marais na mpaka sasa watu waliohusika katika shambulio hilo hawajakamatwa.Nilipata taarifa kutoka katika vyanzo vyangu vya habari kwamba kuna mtu anaitwa Khalid Sultan Khalid kutoka katika kundi la kigaidi al IS anakuja hapa nchini.Huyu ni mtu anayejishughulisha na milipuko mikubwa.Mkurugenzi mpya wa idara hii anaitwa Annabel

ni rafiki yangu na nilimuomba tuitumie idara yake kumfuatilia Khalid na kufahamu kile alichokuja kukifanya hapa Tanzania pamoja na washirika wake.Zoezi lilifanyika vizuri lakini katikati ya zoezi hilo mawasiliano yakakatika na timu iliyokuwa ikimfuatilia Khalid ikashindwa kufanya kazi yake na Khalid akapotea hadi sasa hatujui mahala alipo.Baada ya kufanya uchunguzi tukagundua kwamba mawasiliano hayo yalikatwa kwa makusudi na

mfanyakazi anaitwa Edina .Tulimfuatilia huyo Edina na kukuta ameuawa nyumbani kwake.Baada ya Edina kuuawa tukalazimika kumuhoji mhandisi mkuu ambaye alisema uongo kwamba mawasiliano yale yalikatika kutokana na hali ya hewa.Ilitumika nguvu kidogo kumuhoji kwani aligoma kusema chochote na alipelekwa katika chumba cha matibabu baada ya kupoteza fahamu.Baadae tukaambiwa amefariki dunia na kitu cha kushangaza ni kwamba

mkurugenzi huyo mpya ambaye aligundua kuhusiana na sababu ya kukatika kwa mawasiliano yale akaondolewa katika nafasi yake kwa kutumia kanuni za idara na aliyeongoza zoezi hilo ni Edwin Mbeko.Huo ni upande mmoja.Upande wa pili kuna mtu anaitwa Melanie Davis huyu anaishi hapa nchini na anashirikiana na James Kasai ambaye kwa kushirikiana na IS walitekeleza shambulio lile lililoua wake za marais.Huyu Melanie mpaka sasa tunamsaka na hatujafanikiwa

kumpata lakini kuna mtu wa karibu na Melanie ambaye anaishi Ufaransa na baada ya kumchunguza huyo mtu tukagundua ana mawasiliano ya karibu na Edwin Mbeko na hiyo ndiyo sababu niko hapa.I’m here for EdwinMbeko.Nimekuja kumchunguza kwani ninahisi anaweza kuwa na mahusiano na Melanie Davis ambaye anashirikiana na magaidi wa IS.Nina uhakika hata tukio lile la kumpoteza Khalid Sultan Khalid anahusika.Hivyo ndugu zangu nadhani kwa hayo

machache mmenielewa” akasema Mathew

“Kama unamtafuta Edwin kwa nini ukamfuata hapa?Kwa usingemtafuta sehemu nyingine nje ya hapa?

“Edwin Mbeko anatumia ofisi hii kama mwavuli wa kufichia mambo yake na ndiyo maana nimekuja hapa kufanya uchunguzi katika ofisi yake.Ndugu zangu nisingeweza kuja sehemu hii ya hatari kama nisingekuwa na sababu ya msingi niliyowaeleza.Kuna hatari kubwa ya kufanyika kwa shambulio lingine kubwa hapa

nchini hivyo kila juhudi lazima zifanyike kuhakikisha tunalizuia hilo lisitokee”akasema Mathew

“Kwa nini usiwasilishe suala hili katika vyombo husika vilishughulikie?

“Nisingeshindwa kufanya hivyo lakini hawa jamaa wana mizizi mirefu hadi katika taasisi za serikali kama hii.Ninawaomba ndugu zangu mnisaidie ili niweze kufanikisha jukumu lililonileta hapa.Kama msiponisaidia nikafanikisha kile kilichonileta hapa hamtakuwa mnatekeleza

wajibu wenu wa ulinzi wa nchi na nina uhakika mtaona aibu pale mtakaposikia magaidi wametekeleza shambulio lingine hapa nchini" akasema Mathew kisha akachukua kisu na kukata zile pingu za plastiki halafu akawarejeshea silaha zao.

"The choice is yours.Take me down or save the country ! akasema Mathew.Kiongozi wa kikosi kile akawatazama wenzake halafu akauliza

"What do you want?akamuuliza Mathew

“Nataka nifike katika ofisi ya Edwin.I need your help” akasema Mathew

“Kama nisingekuwa nimesikia habari zako nisingekuamini lakini nimesikia mambo makubwa uliyoyafanya kwa ajili ya nchi hii na ninakuamini.Mimi na wenzangu tutakusaidia kufanikisha kile kilichokuleta hapa japokuwa ni hatari kwetu lakini ni jambo sahihi kulifanya kwa ajili ya ulinzi wa nchi”

“Ahsanteni sana ndugu zangu” akasema Mathew

“Kwa sasa wafanyakazi wote walioko ndani ya jengo hili wamekusanywa ndani ya chumba maalum na kila kitu kimezimwa.Milango yote ya kuingiana kutoka imewekwa walinzi hivyo si rahisi kwa wewe kuweza kufika huko unakotaka kwenda.Sisi tumekuja jumla nane na tumegawanyika makundi mawili.Kundi moja ni sisi tuliokuja huku chini na kundi la pili liko juu.Tutakachokifanya utavaa mavazi ya mmoja wetu ili uonekane kama mwenzetu

kisha utaongozana na mmoja wetu kuelekea katika ofisi ya Edwin na wakati huo sisi tutaendelea kuwepo huku tutawaeleza wenzetu kwamba tunaendelea kukutafuta.Naomba ndani ya dakika kumi uwe umemaliza kazi yako katika ofisi hiyo kwani walioko juu wanaweza wakaingiwa na wasiwasi tumechukua muda mrefu huku chini" akasema Yule mkuu wa ile timu

"Ahsante sana nashukuru kwa msaada wenu.You are doing the right thing for the

country” akasema Mathew huku akianza kuvua mavazi yake na kubadilishana mavazi na mmoja wa makomando wale kisha akaongozana na komando mwingine wakashuka ili kwenda kupita katika mlango mkubwa.

Katika sehemu ya juu ya njia ile ya dharura,makomando wanne wakiwa na Edwin Mbeko na walinzi wengine wawili waliendelea kusubiri taarifa kutoka kwa wenzao waliokuwa wamepita chini.

“Hakuna njia nyingine ambayo huyo mvamizi anaweza akapita na kutokomea zake?akauliza mkuu wa kikosi kile.

“Hakuna sehemu anayoweza kutoka.Ukiacha mlango huu hapa juu,upo mlango mwingine ghorofa ya pili ambao hufunguliwa kwa namba maalum ambazo walizo nazo ni viongozi pekee hakuna tena mlango mwingine zaidi ya hii miwili” akajibu Edwin

“C2 nini kinaendelea huko chini?Mmechukua muda mrefu mko kimya.Tujulisheni

kinachoendelea ova ! akasema Yule mkuu akiwasiliana na kikosi kilichokwenda chini akajulishwa kwamba wanaendelea na upekuzi wa kina

Mathew akiwa katika mavazi waliyovaa wale makomando akiwa ameongozana na komando mwingine wakaelekea upande wa ofisi za wakuu wa idara.Anaifahamu ofisi ya Edwin Mbeko akausogelea mlango haukuwa umefungwa kwani Edwin alitoka kwa haraka na kusahau kufunga

ofisi yake.Mathew akamtaka Yule komando kumsubiri nje akausukuma mlango akaingia ndani moja kwa moja akaelekea katika meza ya Edwin.Makaratasi mengi yalikuwepo mezani na hakujua aanzie wapi mara akauona mkoba wa kompyuta ukiwa pembeni akaushika kwa umakini huku mkononi akiwa amevaa glovu akaufungua na kutoa kompyuta ndogo na makaratasi kadhaa akayapitia na kustuka baada ya kuiona karatasi moja ikiwa

imeandikwa kwa mkono ikiwa na orodha ya vitu mbali mbali

“Hivi ni vifaa vya kutengeneza mlipuko.Ahsante Mungu” akawaza Mathew kisha akapiga picha karatasi zile kwa kutumia simu yake

“Ningeondoka na kompyuta ya Edwin lakini akiikosa atajua nimefika ofisini kwake.Ngoja nimpigie Ruby anipe maelekezo kuhus……”akawaza Mathew na kutolewa mawazoni na Yule komando aliyekuwa nje ya mlango aliyemjulisha kwamba anasikia

vishindo vya watu wanakuja.Haraka haraka Mathew akarudisha kila kitu katika mkoba namna kilivyokuwa akatoka wakaondoka eneo lile wakarejea kule walikowaacha wenzao.

“Umefanikiwa kupata kile ulichokuwa unakitafuta?akauliza kiongozi wa ile timu ya chini

“Nimepata kitu kidogo lakini naamini kitakuwa na msaada mkubwa.Please help me get out of here” akasema Mathew

“Kila kitu kimezimwa sasa hivi hakuna kamera yoyote inayofanya kazi.Utatokea upande wa magharibi kwani geti kuu kuna walinzi.Utapanda ukuta utaruka nje kisha utawasiliana na wenzako watakufuata”

“Ninashukuru sana ndugu zangu kwa msaada huu mkubwa mlionisaidia.Mungu atawajalia kwa hili mlilolifanya kwa nchi yenu” akasema Mathew kisha akavaa mavazi yake akaongozana na makomando wawili wakatoka mle ndani.Kulikuwa na walinzi

katika mlango wa kutokea nje lakini hawakuwauliza chochote.Mathew na wale makomando wakaelekea upande wa magharibi na Mathew akapanda ukuta akaruka nje wale makomando wakarejea ndani kisha wakawajulisha wenzao kwamba wametafuta kila sehemu Mathew hakuwepo.

“Haiwezekani ! akasema Edwin kwa hasira

“Mtu huyo alikuwemo humu ndani.Ametoka vipi?

“Yawezekana aliwahi kutoka kabla hatujafika”

akajibu mkuu wa kile kikosi cha makomando na Edwin akawataka waiingie wote kwa mara nyingine kupekua ili kujiridhisha kwamba kweli hakukuwa na mtu.Baada ya kupekua kona zote hakuonekana mvamizi yeyote.Edwin akaelekeza makomando wale kupekua sehemu nyingine zote za jengo lakini Mathew hakuonekana .

****

Ruby akiwa katika ofisi ya Mathew alihisi

kuchanganyikiwa.Alikuwa akiingia na kutoka ndani ya ofisi ile huku akizungumza mwenyewe

“What am I going to do to save Mathew?akajiuliza

“Ee Mungu naomba umsaidie Mathew aweze kutoka salama ndani ya lile jengo.Maisha yake yako hatarini.Endapo akikamatwa mambo yote yataharibika” akaomba Ruby na kukaa juu ya meza akiwaza

“Ngoja nipigie simu Austin yawezekana akawa na msaada japo anaumwa” akawaza Ruby

na kumpigia simu mmoja wa madaktari anayewauguza Austin na Gosu Gosu na kumuomba azungumze na Austin

“Hallow Ruby ! Sauti ya Austin ikasikika baada ya muda mfupi.

“Austin samahani kwa usumbufu najua una umwa lakini sina mwingine ninayeweza kumkimbilia kuomba msaada” akasema Ruby

“Kuna nini Ruby?akauliza Austin na Ruby akamueleza kile kilichotokea

“We need to save Mathew.Please help me” akasema Ruby

“Ruby please relax ! Nipe dakika tano nipige simu niombe msaada wa vijana wangu waende wakamkomboe Mathew” akasema Autin

“Thank you Austin” akasema Ruby

Dakika mbili toka awasiliane na Austin simu yake ikaita akaitoa mfukoni haraka haraka na kustuka baada ya kukuta mpigaji ni Mathew hakupoteza hata sekunde akaipokea

“Mathew are you okay?akauliza Ruby

“Niko salama Ruby.Tayari nimetoka ndani ya jengo”

“Ouh thank you Lord.Umewezaje kutoka?

“Ruby tutazungumza baadae lakini kwa sasa nahitaji msaada.Nataka uje unichukue hapa mahala nilipo.Gari langu nimeliacha SNSA” akasema Mathew na kumuelekeza Ruby mahala alipokuwa.Ruby akakimbia nje akaingia garini na kuondoka kwa kasi.Mara tu alipotoka getini akampigia simu Austin na kumjulisha

kwamba tayari amewasiliana na Mathew amekwisha toka ndani ya lile jengo la SNSA.

****

Upekuzi katika jengo la SNSA ulikamilika bila ya kumpata mvamizi aliyetajwa kuvamia jengo lile.Kikosi cha makomando wa SNSA kilichokuja kupambana na wavamizi kikaondoka kurejea katika kambi yao.Edwin Mbeko akaamuru shughuli ziendelee kama kawaida huku

ulinzi ukiimarishwa kila kona ya jengo lile.

“Rais hawezi akanidanganya lazima mvamizi alikuwemo humu ndani.Amewezaje kutoka ndani wakati milango yote ilikuwa na walinzi?Inanishangaza sana.Au yawezekana wakati Rais ananipa taarifa tayari huyo mvamizi alikwisha toka.Nitazungumza na Rais na kumfahamisha kila kitu,kwa sasa ni wakati wa kulimaliza lile suala la Gosu Gosu kisha nitakuja kuendelea na hili

suala la huyu mvamizi” akawaza Edwin na kuelekea katika chumba alichokuwamo Dr Masawe

“Dr Masawe nimerejea tena.Safari hii sitaki mzaha nataka unieleze mahala alikopelekwa Gosu Gosu .Nakuhakikishia ukinieleza ukweli utaondoka salama na familia yako” akasema Edwin

“Nitakueleza ukweli lakini naomba familia yangu wasiguswe” akasema Dr Masawe

“Nimekwisha kwambia kwamba utakaponieleza ukweli

familia yako itakuwa salama na utaondoka nao” akasema Edwin na Dr Masawe akavuta pumzi ndefu halafu akamueleza Edwin mahala alipo Gosu Gosu.

“Ahsante kwa kunieleza ukweli lakini utaondoka hapa na familia yako baada ya kujiridhisha kwamba ulichoniambia ni cha kweli” akasema Edwin na kutoka akarejea ofisini kwake akawaita vijana wake wanne wakiongozwa na dereva wake Jackson akawapa maelekezo

ya kwenda mahala aliko Gosu Gosu kumuua.

“Hakikisheni hakuna mtu mnayemuacha hai mahala hapo ! akasisitiza Edwin na wale vijana wakaondoka kisha akampigia simu Rais

“Edwin mmempata Mathew Mulumbi? Akauliza Dr Fabian

“Mathew Mulumbi ni nani mheshimiwa Rais?akauliza Edwin

“Ndiye aliyevamia hapo”

“Mheshimiwa Rais hatujafanikiwa kumpata huyo mtu”

“Hamjampata?! Dr Fabian akashangaa

“Ndiyo mheshimiwa Rais hatujampata”

“That’s impossible”

“Kweli mheshimiwa Rais”

“Amewezaje kutoka humo ndani bila kukamatwa?

“Mheshimiw Rais mara tu uliponipa taarifa ile kila kitu hapa kilisimama na tukaanza msako haraka sana na pia makomando wa idara yetu walifika wakaendelea na zoezi la kumtafuta bila mafanikio”

“This man is not a real human.He’s a ghost ! akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa rais huyu Mathew Mulumbi ni nani?Edwin akauliza

“I don’t know much about him.Inasemekana alifariki miaka mitatu iliyopita lakini ameibuka hivi karibuni kutoka mahala kusikojulikana na ameanza kuleta matatizo.Sina hakika kama ni binadamu wa kawaida.Hakuna chochote ambacho amechukua hapo?

“Hakuna mheshimiwa Rais tuliwahi kuzima kila kitu

isipokuwa ameua walinzi wetu watatu waliokuwa geti kuu”

“Dah ! akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais huyuo mtu ni nani tuweze kumfuatilia?akauliza Edwin

“Nitakutafuta baadae Edwin lakini kwa sasa hakikisheni ulinzi unaimarishwa sana hapo katika idara” akasema Dr Fabian na kukata simu

“Mathew Mulumbi ni nani?akajiuliza Edwin baada ya Rais kukata simu

“Rais amefahamuje kama kuna mtu amevamia idara

yetu? Akaendelea kujiuliza Edwin

“Ngoja nimsubiri yawezekana akanieleza baadae alikopata taarifa za mtu huyo kuvamia idara yetu.Kwa sasa ngoja nijielekeze zaidi katika mipango yetu” akawaza Edwin na kuchukua simu akamtafuta Devotha lakini bado simu yake haikupatikana

“Devotha amekwenda wapi?Kwa nini hapatikani simuni ? Yeye ndiye kiongozi wa mipango yote hatakiwi kukosekana simuni lakini tumekuwa tunamtafuta toka

asubuhi hapatikani na hajatoa maelezo yoyote ya mahala alipo.Anatupa wakati mgumu wa kufanikisha m ipango yetu” akawaza Edwin

****

Mathew alitoka mafichoni baada ya Ruby kuwasili mahala alikokuwa amejficha akaingia garini na Ruby akaliondoa kwa kasi

“Thank you Ruby” akasema Mathew

“Mimi ndiye ninayepaswa kumshukuru Mungu kwa

kukuwezesha kutoka salama ndani ya lile jengo.Niliogopa sana nikalazimika kumpigia simu Austin kumuomba msaada na muda mfupi baadae ukapiga simu” akasema Ruby

“Ahsante sana Ruby kwa kufanya kila jitihada za kuniokoa.Walifahamuje kama nimeingia mle ndani? Akauliza Mathew

“Hata mimi bado ninajiuliza wamefahamuje” akasema Ruby na mara akakumbuka kitu

“Rais alinipigia simu akanitaka niende ikulu usiku

huu tukazungumze kuhusiana na lile suala langu la kuondolewa SNSA nikamwambia haitawezekana kwani tuko katika operesheni muhimu.Akaniuliza ni operesheni gani inaendelea nikamueleza kwamba umekwenda SNSA kuna jambo unakwenda kulichunguza.Rais hakuonekana kufurahi" akasema Ruby

"Ulimueleza Rais kuhusu operesheni hii?akauliza Mathew

"Nilimueleza kwamba kuna jambo unakwenda

kulichunguza SNSA lakini sikumueleza unachokwenda kukifanya pale”

“Basi ni yeye aliyewapa taarifa SNSA ! akasema Mathew kwa hasira

“Hukupaswa kumueleza chochote.Ameharibu sana misheni yetu.Mida hii tulipaswa kuwa na Edwin Mbeko tunamuhoji lakini tumeshindwa kwa sababu yake.From now on hakuna kupokea simu yake yoyote hadi hapo tutakapomaliza operesheni yetu.Forget about

SNSA ! akasema Mathew kwa ukali

“Kwa nini lakini afanye hivi?Kwa nini awaeleze SNSA huku akijua kwamba kwa kufanya hivyo anavuruga misheni yako? Akauliza Ruby

“Rais haniamini hata kidogo.Toka nilipokwenda kuonana naye kumueleza suala la James Kasai hakuonekana kuniamini” akasema Mathew

“Uliwezeje kutoka mle ndani? Ruby akauliza na Mathew akamueleza kila kitu kilichotokea hadi

alivyofankiwa kutoka nje ya jengo lile.

“Ahsante Mungu kwa kumtoa salama huyu mwanaume ninayempenda kuliko wote ndani ya hatari kubwa” akawaza Ruby

“Katika mkoba wa Edwin nimekuta kuna kompyuta lakini sikuweza kuifungua badala yake nikabandika kadi ndogo chini ya kompyuta ambayo itatuwezesha kumfuatilia.Vile vile katika mkoba huo nimekuta makaratasi kadhaa na nilipoyapitia kwa haraka

haraka nilikuta kuna karatasi moja limeandikwa kwa kalamu ya wino ina orodha ya vitu mbali mbali na nilipoipitia haraka haraka nikagundua katika orodha hiyo kuna vitu vinavyotumika katika kutengeneza mlipuko.Nimezipiga picha karatasi zote ili tuweze kuzifanyia uchunguzi” akasema Mathew

“Good Job Mathew.Ilikuwa ni kazi ya hatari sana lakini kwa hiki kdogo ulichokipata ni

mafanikio makubwa kwetu”akasema Ruby

“Sikufanikiwa kumpata Edwin usiku wa leo lakini tayari amekwisha ingia katika rada zetu na saa zake zinahesabika.Hana muda mrefu kabla ya kutua katika mikono yetu” akasema Mathew alipomtazama Ruby michiziri ya machozi ikaonekana machoni pake.

“Ruby let me drive” akasema Mathew na Ruby akasimamisha gari pembeni ya barabara Mathew akashika usukani.

“Nini kinakutoa machozi Ruby?akauliza Mathew

“Najiuliza kama hao makomando wangekataa kukusaidia ungekuwa wapi mida hii? Kinachoniumiza zaidi ni mimi ndiye ambaye ningekuwa nimesababaisha misheni ile kuharibika kwa kumueleza rais” akasema Ruby na kuinamisha kichwa

“Ningeweza kuwaua makomando wale lakini niliwaacha hai kwa kujua lazima wangenisaidia.Endapo wangekataa kushirikiana nami nisingekuwa na kitu kingine

cha kuwafanya zaidi ya kuwaua.Mimi ninapokuwa katika kazi yangu huwa sina huruma hata kdogo.Kikwazo chochote kinachokuja mbele yangu lazima nikiondoe ili niweze kufanikisha misheni yangu.Bahati yao walikubali kushirikiana nami.Niliwaweka katika hatari lakini walifanya kitu sahihi kwa ajili ya nchi yao.Kuhusu Rais usijilaumu kwani hukujua kama angewezakufanya kitu kama kile.Kuanzia sasa kata kabisa mawasiliano naye.Amekwisha

onyesha si mtu tunayeweza kumuamini” akasema Mathew

Safari iliendelea wakielekea katika nyumba waliko akina Gosu Gosu.Mita kadhaa kabla ya kuifikia nyumba waliyokuwamo akina Gosu Gosu likaonekana gari nje ya geti.Mathew akapunguza mwendo wa gari.

“Kuna gari pale nje ya geti.Dr Masawe amerudi na kushindwa kuingia ndani?akauliza Mathew

“Kama angekuwa amerudi na kushindwa kuingia ndani lazima angekupigia simu

halafu ile si gari ya Dr Masawe” akasema Ruby.Mathew akasimamisha gari

“Something is not right.Nimepata wasiwasi kuhusiana na gari lile.Tushuke hapa hapa tutembee kwa miguu” akasema Mathew kisha akavua koti alilokuwa amevaa akampatia Ruby bastora moja kisha wakashuka na kuanza kutembea kwa miguu kuliendea geti la ile nyumba.Walilikaribia lile gari na kulichunguza hakukuwa na mtu yeyote ndani yake.

“Wenye hili gari wako wapi? Akauliza Ruby

Mathew akauparamia ukuta na kuchungulia ndani akastuka baada ya kumuona mtu mmoja akiwa na bunduki amesimama mlangoni huku akivuta sigara akarudi chini bila kutoa ukelele.

“Ruby they’re here ! akasema Mathew

“Akina nani? Akauliza Ruby

“Wale watu wanaotaka kumuua Gosu Gosu” akasema Mathew

“Wamefahamuje kama amehamishiwa hapa? Akauliza Ruby

“Let’s find out.Follow me” akasema Mathew wakazunguka nyuma ya nyumba Mathew akapanda ukuta na kurukia ndani bila kishindo.Bastora ikiwa mkononi akanyata kuelekea upande wa mbele ya nyumba kwenye mlango mkubwa wa kuingilia sebuleni.Yule jamaa mwenye bunduki bado aliendelea kuzunguka zunguka pale mlangoni.Mathew akautikisa mti wa maua na

Yule jamaa akastuka akageuka kutazama kuna nini hakuona kitu,akaanza kutembea kwa tahadhari kuelekea ulipo ule mti ili kujiridhisha kama kweli hakuna kitu Mathew akajiweka tayari.Mara tu Yule jamaa alipokaribia ule mti Mathew akaruka kama kima akamvamia Yule jamaa na kumpiga kichwa kizito kilichompeleka chini akapoteza fahamu.Mathew akachukua pingu ya plastiki akamfunga mikono na kujaza tambara mdomoni kisha akamtupa pembeni sehemu

yenye mwanga hafifu akaenda mlangoni akachungulia ndani kupitia dirisha lililokuwa pembeni ya mlango lakini hakukuwa na mtu yeyote sebuleni akakiminya kitasa cha mlango akaufungua taratibu sana akaingia sebuleni akanyata hadi katika korido akachungulia na kumuona mtu mmoja akiwa amesimama nje ya chumba alimolazwa Gosu Gosu akiwa na bunduki.Mathew akaenda katika runinga akaongeza sauti.Yule jamaa aliposikia sauti imeongezeka akaanza

kupiga hatua kuelekea sebuleni kutazama nani ameongeza sauti ya runinga.Mathew akajiweka tayari na Yule jamaa alipojitokeza akakutana na ngumi nzito iliyompeleka ukutani,kabla hajakaa sawa akavutwa na kupigwa kichwa kizito akaanguka chini.Mathew hakutaka kumtazama tena kwani kwa kichwa kile tayari hakuwa na fahamu.Mathew akapiga hatua ndefu za tahadhari kuelekea katika chumba cha Gosu Gosu.Mlango haukuwa

umefungwa akachungulia ndani akawaona madaktari na wauguzi waliokuwa wanamuhudumia Gosu Gosu wakiwa wamepigishwa magoti chini huku jamaa wawili wakiwaelekezea bunduki

“Natoa nafasi ya mwisho.Nataka mniambie nani aliyewatuma mumtoe huyu mgonjwa hospitali? Akauliza mmoja wa wale jamaa kwa ukali.Mmoja wa wauguzi alikuwa analia na kuwaomba wale jamaa wawasamehe

“Nitahesabu hadi tatu kama hamtanieleza nitawapiga wote risasi ! akasema Yule jamaa mwenye macho ya kikatili akaanza kuhesabu kuanzia tatu.Kabla hajamaliza kuitamka moja Mathew akaizinga bastora yake na kumpiga risasi Yule jamaa katika kiganja cha mkono bunduki ikaanguka chini.Yule mwenzake aliyekuwa naye alistuka baada ya kumuona mwenzake ametoa mguno baada ya risasi kumpiga kiganja cha mkono.Kabla hajajua risasi ile ilikotoka

tayari Mathew alikwisha ingia me chumbani akamtandika tee zito la mbavu Yule jamaa aliyempiga risasi ya mkono akaenda kujibamiza ukutani halafu akamuelekezea bastora Yule jamaa mwingine mwenye bunduki

“Weka silaha yako chini taratibu ! akasema Mathew kwa ukali akimuelekezea Yule jamaa bastora.Taratibu Yule jamaa akaiweka chini bunduki yake.Mathew akampa mmoja wa wale madaktari pingu ya plastiki na kumtaka amfunge Yule jamaa mikono kwa

nyuma halafu akawataka wamsaidie Yule jamaa aliyepigwa risasi kiganja cha mkono kuzuia damu kuendelea kumwagika

“Kuna yeyote ameumizwa?akauliza Mathew

“Hakuna aliyeumizwa wote tuko salama.Umetokea kwa wakati muafaka kabisa kwani ungechelewa kidogo sote tungeuawa.Ahsante sana Mathew kwa kutuokoa bado siamini kama tumenusurika kifo ! akasema mmoja wa wale madaktari huku akilia.

“Wagonjwa wote wanaendeleaje?

“Wote wanaendelea vizuri.Hawa watu ni akina nani?akauliza daktari mwingine

“Hata mimi siwafahamu lakini muda si mrefu tutawafahamu wote” akasema Mathew kisha akawaelekeza madaktari wawakusanye wale jamaa waliopoteza fahamu wawaweke sebuleni akampigia simu Ruby na kumtaka aingie ndani kwani hatari imekwisha na wale jamaa wamedhibitiwa.Yule jamaa

aliyepigwa kiganja cha mkono akapatiwa matibabu halafu naye akafungwa mikono kwa waya na wote wakachukuliwa wakapelekwa sebuleni wakaungana na wenzao wawili ambao hawakuwa na fahamu.

Ruby alikwenda kuchukua gari mahali walikoliacha akafungua geti akaingia ndani.Aliposhuka garini akaingia sebuleni na kupatwa na mstuko mkubwa alipowaona wale jamaa waliokuwa wamedhibitiwa na Mathew

“You ?! akasema Ruby akimshangaa mmoja wa wale jamaa ambaye naye alistuka mno alipomuona Ruby akiingia mle ndani

“Unawafahamu?akauliza Mathew

“Ndiyo.Huyu mmoja ninamfahamu anafanya kazi SNSA ni dereva wa Edwin Mbeko”

“Dereva wa Edwin?! Akauliza Mathew naye akishangaa na kuwatazama wale jamaa kwa hasira

“Ahsante sana Ruby kwa kunijulisha wanakotoka watu hawa”

“Watu wote humu wako salama? Akauliza Ruby

“Wote wako salama.Niliwahi kabla hawajawaumiza” akasema Mathew kisha akawageukia wale jamaa

“Wakati tunawasubiri wenzenu wazinduke nataka mfahamu kwamba hapa mlipoingia ni katika tanuru la moto.Uhakika wa kutoka hai hapa ni mdogo sana labda kama mtakuwa tayari

kunieleza ukweli lakini endapo mtakuwa kiburi huu ndio mwisho wenu ! akasema Mathew na kuwatazama kwa hasira kisha akamnyooshea bastora Yule jamaa aliyetambuliwa na Ruby

“Jina lako nani? Akaulia Mathew Yule jamaa akawa kimya

“Nakuuliza jina lako nani? Akauliza tena

“Tafadhali sema ukweli ukijifanya kiburi utapata taabu sana ! Ruby akamweleza Yule jamaa

“Jina lako nani?akauliza Mathew Yule jamaa bado akawa kimya na kuzidi kumpandisha Mathew hasira.Akamfuata Yule jamaa mwingine aliyepigwa risasi ya kiganja cha mkono akamuinua kisha akachukua kisu na kuzichana chana nguzo zake akabaki mtupu halafu akamgeukia Yule dereva wa Edwin

“Jina lako nani?akauliza Mathew Yule dereva bado akawa kimya.Mathew akageuka kwa kasi na ghafla Yule jamaa aliyepigwa risasi ya

kiganja akatoa ukelele mkubwa wa maumivu makali.Alikuwa amekatwa uume wake.Aligalagala chini kwenye damu.Mathew hakumjali akamfuata Yule dereva na kumchana chana nguo zake kwa kisu naye akabaki mtupu

“Umeona kilichomtokea mwenzako.Nakuuliza kwa mara ya mwisho jina lako nani? Akauliza Mathew

“Naitwa Jackson Kandala” akasema Yule jamaa huku akitetemeka kwa woga.

“Nani kawatuma hapa?

“Tumetumwa na mkuu wetu”

“Mkuu wenu nani?

“Edwin Mbeko ! akasema Jackson halafu Mathew akamgeukia Ruby akamtaka awaite madaktari waje wamshughulikie Yule jamaa aliyekatwa uume wake.Madaktari wakafika na kumchukua Yule jamaa wakampeleka katika chumba kitupu wakaanza kumuhudumia ili kuzuia damu kuendelea kumwagika

“Umeona kilichomtokea mwenzako nawe pia

kitakutokea kama hiki endapo utaendelea kuwa kiburi.Nataka unieleze ukweli Edwin Mbeko amekutuma nini hapa?akauliza Mathew Jackson akawa kimya.Mathew akaushika uume wa Yule jamaa na kuuvuta akainua mkono wenye kisu juu

“Usinikate tafadhali nitakueleza! akasema Jackson

“Edwin amekutuma nini?

“Ametutuma kuja kumuua mgonjwa ambaye amehamishwa kutoka hospitali na kuletwa hapa anaitwa Gosu Gosu”

“Amewaeleza sababu za kutaka kumuua Gosu Gosu?

“Hapana hajatueleza chochote.Katutuma tuje hapa kufanya kazi moja tu ya kuwaua watu wote tutakaowakuta humu ndani” akasema Jackson

“Amefahamuje kama Gosu Gosu yuko hapa?akauliza Mathew Jackson akasita kujibu

“Jackson nitakuharibu sasa hivi kama Yule mwenzako naomba unijibu tafadhali ! akasema Mathew.Jackson akaingiwa hofu baada ya

kuona macho ya Mathew yaliyoonyesha alikuwa tayari kumfanyia ukatili mkubwa.

“Anamshikilia daktari mmoja anaitwa Dr Masawe na familia yake na ndiye aliyemuelekeza mahala alipohamishiwa Gosu Gosu”

“Edwin anamshikilia Dr Masawe?

“Ndiyo.Aliiteka kwanza familia yake kisha akampigia simu na kumpa maelekezo na huyo daktari ndiye aliyemuelekeza Edwin mahala alipo GosuGosu” akasema

Jackson.Mathew na Ruby wakatazamana.

“Dr Masawe yuko wapi hivi sasa?akauliza Mathew

“Yuko SNSA yeye na familia yake.Edwin atamuachia pale tu Gosu Gosu atakapokuwa ameuawa.” akajibu Jackson.Mathew akamtaka Jackson avae suruali yake wakaenda nje sehemu ya kupumzikia kulikokuwa na sofa nzuri akamtaka achukue simu yake

“Mpigie simu Edwin mwambie kwamba tayari mmeimaliza kazi

aliyowatuma.Gosu Gosu na wote mliowakuta hapa mmewaua” akasema Mathew.Jackson akazitafuta namba za simu za Edwin akampigia huku akiguswa na mdomo wa bastora kichwani.

“Jackson” akasema Edwin baada ya kupokea simu

“Edwin kazi tumeimaliza.Gosu Gosu tumemuua pamoja na wote tuliowakuta humu ndani.Tumeua madaktari wawili,wauguzi wawili na wagonjwa wawili Gosu Gosu na mwenzake”

“Good job Jackson.Mmenifurahisha sana.Kabla ya kuwaua mliwahoji madaktari wakasema nani aliyewatuma kumuhamisha Gosu Gosu?akauliza Edwin

“Tuliwahoji lakini hawafahamu chochote tukawaua”akajibu Jackson

“Ahsante Jackson.Rejesheni silaha kisha mkapumzike” akasema Edwin

“Ahsante sana mkuu” akajibu Jackson.Mathew akaichukua simu ile na kuizima kabisa.

“Umefanya vizuri Jackson.Bado kuna mambo ambayo nataka kuendelea kukuuliza kuhusu Edwin Mbeko”akasema Mathew

“Wewe umekuwa ni dereva wa Edwin Mbeko.Unaweza ukaniambia sehemu ulikompeleka kwa siku mbili jana na leo?Wapi ulimpeleka nje ya ofisi?akauliza Mathew

“Kwa wiki nzima sijampeleka Edwin sehemu yoyote.Amekuwa akiendesha gari lake yeye mwenyewe”

“Jackson mimi ni mtu mbaya sana pale mtu

anaponidanganya au kunionyesha kiburi.Umeona nilichomfanyia Yule mwenzako.Nimetoa uanaume wake na hata wewe ninaweza kukufanyia vile vile nilivyomfanya mwenzako.Yawezekana jua la kesho msilione tena kama mtaendelea kunifanyia kiburi.Nieleze ukweli uokoe maisha yako na wenzako ! akasema Mathew

“Nitakueleza ukweli kaka naomba uniamini”

“Nieleze haraka ! akasema Mathew

“Nimekwambia ukweli kwamba kwa wiki nzima sijamuendesha Edwin amekuwa akiendesha gari lake yeye mwenyewe lakini alinituma mara mbili nimpelekee gari lake katika bohari kuu la idara”

“Yeye alikuwa wapi hadi akakutuma umpelekee gari lake huko katika bohari? akauliza Mathew

“Mara ya kwanza alikuwa safarini Kagera akanipigia simu na kunielekeza nimpeleke gari lake bohari.Aliposhuka katika

helkopta akaingia ndani ya gari na kuondoka na wageni wake”

“Alikuwa na wageni?

“Ndiyo alikuwa na wageni”

“Uliwaona wageni hao?

“Ndiyo alikuwa na wageni wawili mwanaume na mwanamke” akasema Jackson Mathew akamgeukia Ruby

“Ulikuwa mkuu wa Edwin.Alikujulisha kuhusu safari hiyo ya Kagera?

“Hakunijulisha chochote kama anasafiri.Nakumbuka kuna siku nilimtafuta nikamkosa na kesho yake

akaniambia kwamba alikuwa safari nje ya mkoa nadhani ndiyo safari hiyo aliyokwenda Kagera”akajibu Ruby

“Jackson mara ya pili alipokuelekeza umpelekee gari katika bohari ilikuwa lini?akauliza Mathew

“Ni leo jioni.Alikwenda Arusha na akanitaka nimpelekee gari bohari.Alikuja na mgeni mmoja mwanaume akaingia garini na kuondoka”akajibu Jackson

“Wageni ambao alikuja nao mara ya kwanza unaweza

ukawafahamu ukiwaona? Mathew akauliza

“Ilikuwa jioni na kiza kilianza kuingia walipotua hivyo siwezi kuzikumbuka vyema sura zao.Mwanamke aliingia haraka haraka ndani ya gari sikumuona vizuri lakini Yule mwanaume ninaweza kumkumbuka alikuwa mrefu alivaa suti ya bluu na kofia ya mduara kichwani.Alivaa miwani mikubwa kuficha macho yake na kidevu chake chote kilijaa ndevu

Maelezo yale yakamstua Mathew.Akamtaka Ruby

akalete picha ya James Kasai.Ruby akaenda katika gari na kurejea na kompyuta yake akaifungua picha ya James Kasai

“Jackson tazama vizuri picha hii” akasema Mathew na Jackson akayaelekeza macho yake katika ile picha ya James Kasai

“Mtu huyo uliyemuona akishuka katika helkopta na Edwin anafanana na huyu katika picha?akauliza Mathew na Edwin akaikazia macho picha ile na kusema

“Huyu jamaa pichani anafanana na Yule niliyemuona lakini kidogo sana hasa maeneo ya kidevuni” akasema Jackson.Ruby akaichukua kompyuta yake na kuuliza

“Uliyemuona alikuwa amevaa kofia ya namna gani?

Jackson akamuelekeza kofia aliyokuwa amevaa Yule jamaa na Ruby akacheza na kompyuta yake akaivisha kofia ile picha ya James Kasai.

“Miwani ya namna gani alikuwa amevaa?akauliza James,Jackson akamuelekeza

kila kitu alichokuwa amekivaa Yule mtu na Ruby akakiweka katika ile picha halafu akamuonyesha Jackson akabaki anashangaa

“Yule mtu alikuwa hivi hivi isipokuwa ndevu zake zimekuwa nyingi kidogo tofaui na hizi katika hii picha” akasema Jackson.Mathew akamtazama kwa makini na kuuliza

“Jackson are you sure?

“Yes I’m sure” akajibu Jackson

“Jackson ahsante sana kwa maelezo haya

uliyotupa.Twende ndani” akasema Mathew na kumchukua Jackson akampeleka katika chumba kitupu akamfunga mikono kwa pingu za plastiki halafu akaenda kuwachukua na wale jamaa wengine wawili ambao bado hawakuwa wamezinduka akawapekua na kuchukua simu zao kisha akawapeleka katika chumba kidogo cha stoo akawafungia humo kisha akamfuata Ruby

“Ruby sina shaka na maelezo ya Jackson kwamba mtu huyo ambaye aliongozana

na Edwin Mbeko katika helkopta kutoka Kagera ni James Kasai” akasema Mathew

“Ninataka sana kumuamini Jackson lakini ninasita” akasema Ruby

“He’s telling the truth ! akasema Mathew

“Edwin Mbeko alikwenda Kagera na helkopta ya idara ya SNSA na akaenda kumchukua James Kasai.Tulifahamu James anakuja nchini lakini hatukujua ataingia vipi.Kila sehemu kulikuwa na picha yake na hakukuwa na sehemu

ambayo angeweza kupita bila kujulikana.Ilihitajika mtandao mkubwa wenye nguvu kuweza kumuingiza James Kasai hapa nchini na SNSA ndio waliotumika.James Kasai alivuka mpaka akaingia Kagera Edwin Mbeko akaruka na helkopta hadi Kagera akaenda kumchukua James Kasai na kumleta hapa Dare s salaam.Mpaka hapa tuna uhakika mkubwa kwamba Edwin Mbeko,Devotha na Melanie Davis ni kitu kimoja na Edwin Mbeko kwa kutumia idara ya SNSA hufanikisha

mipango ya mtandao huu.Mfano mzuri ni namna zoezi la kumfuatilia Khalid Sultan lilivyoshindwa kufanikiwa na jambo hilo lilifanywa ndani ya SNSA. Edwin Mbeko alifahamu jambo hili na ndiye aliyefanikisha huo mpango.Kama haitoshi akamuua pia Yule mwanadada Edina ambaye uligundua kwamba ndiye aliyekata mawasiliano.Naamini Edina alifanya vile kwa maelekezo ya Edwin ndiyo maana akamuua.Hata Yule jamaa

tuliyemuhoji Fidelis naamini aliuawa ili kuendelea kuficha siri.Edwin Mbeko ni shetani wa mguu mmoja ! akasema Mathew kwa hasira

“Dr Fabian alifahamu hiki kinachoendelea katika idara ya SNSA ndiyo maana akanitaka nije kuiongoza? Akauliza Ruby

“Inaumiza sana kwa idara nyeti ya serikali kutumika katika kufanikisha mipango miovu ya magaidi”

“Dah ! akasema Mathew

“Baada ya kufahamu kuhusu Edwin Mbeko nini kinafuata? Ruby akauliza

“Kwanza Edwin hatakiwi kujua kama tumekwisha mgundua lakini tuendelee kumfuatilia kwa karibu sana na ndiye ambaye atatuongoza mahala alipo James Kasai.Alipo James ndipo alipo Melanie Davis na ndipo alipo Khalid.Edwin ni mtu muhimu sana kwa sasa” akasema Mathew

“Kwa nini tusimjulishe Rais kuhusu Edwin itakuwa rahisi kumkamata kumuhoji na kisha kujua mahala alipo James Kasai?akauliza Ruby

“Rais hatakiwi kufahamu chochote kuhusu suala hili kwa sasa.Edwin akikamatwa tutashindwa kuwapata akina James na watu wengine wanaohusiana na mtandao wao hivyo tutamfuatilia kwa siri sana na tutafahamu kila kitu” akasema Mathew na kukumbuka kitu

“Katika zile karatasi nilizozipata katika mkoba wake kuna orodha ya vifaa vya kutengenezea mlipuko.Khalid Sultan ni mtaalamu wa milipuko na ambaye zoezi la kumfuatilia lilivurugwa na

SNSA.Nashawishika kuamini kwamba Khalid akishirikiana na washirika wake ambao ni akina Melanie na James Kasai wanatengeneza mlipuko na wanapanga kufanya shambulio lingine hapa nchini.Ili tufahamu lini na wapi shambulio hilo litafanyika lazima tuendelee kumfuatilia Edwin Mbeko kwa karibu sana” akasema Mathew

“Mathew I’m so scared.Kwa nini tusimjulishe Rais jambo hili mapema ili hatua zianze kuchukuliwa? Tukichelewa hawa jamaa

wanaweza wakatekeleza shambulio lao na watu wengi wakapoteza maisha lakini tukimjulisha angali mapema vyombo vyote vya usalama vitaanza kuchukua tahadhari”

“Hatuwezi kumjulisha Rais kwa sasa kuhusiana na suala hili kwani jamaa wakifahamu tayari wamegundulika wanaweza wakajificha na tukashindwa kuufahamu mtandao wao wote.Tunachopaswa kukifanya ni kuhakikisha tunawatafuta watu hawa na tufahamu kama wanatengeneza bomu na wapi

wamepanga kulitumia hilo bomu.Taarifa ikianza kusambaa sasa hivi itavuruga kila kitu.Hawa jamaa wana mtandao mrefu na wamejipachika katika idara mbali mbali za serikali na wanaweza wakapata taarifa haraka kama wanatafutwa” akasema Mathew na kumtazama Ruby akamshika bega

“Ruby we can do this.We’re going to end them and save our country.Have faith in me” akasema Mathew

“I believe you Mathew”

“Thank you” akasema Mathew

“Niliweka kadi nyuma ya kompyuta ya Edwin.Activate that card now.Tunatakiwa kuanza kumfuatilia kujua anakoelekea” akasema Mathew na kumpa Ruby namba za ile kadi aliyoiweka nyuma ya kompyuta ya Edwin na Ruby akaanza kucheza na kompyuta yake.Baada ya dakika mbili akasema

“Kadi tayari inafanya kazi na mpaka sasa inaonekana kompyuta iko katika jengo la

SNSA.Edwin Mbeko bado yuko pale”akasema Ruby

“Good.Tutaanza kumfuatilia bila yeye kufahamu na kujua kila sehemu anakoelekea na tutafahamu mengi kuhusu mtandao wao.Lakini hata hivyo nina swali najiuliza.Ni vipi kama ataiacha kompyuta yake ofisini? Kama ikiwa hivyo hatutakuwa tumefanya chochote. EdwinMbeko ndiye pekee ambaye tunategemea atuongoze katika kuifanikisha misheni hii hivyo lazima

tumchunguze kwa kutumia kila mbinu.” akasema Mathew

“Mathew umesema kitu kizuri.Anaweza akaiacha kompyuta yake ofisini na sisi tukaendelea kudhani kwamba yuko ofisini kumbe hayupo”

“Kuna kitu nakifikiria.Yule dereva wake anaweza akawa na msaada kwetu.Tunaweza tukamtumia” akasema Mathew

“Unataka kumtumia Yule jamaa?akauliza Ruby

“Ndiyo nataka kuzungumza naye ili aweze kushirikiana nasi”

“Nadhani hilo si wazo zuri Mathew.Yule jamaa ni mtiifu kwa Edwin na anaweza akamueleza kila kitu kuhusu sisi” akasema Ruby

“Yule jamaa ndiye anayemfahamu zaidi Edwin kuliko sisi na vile vile Edwin anamuamini sana hivyo tukiweza kumtumia anaweza akawa na msaada mkubwa sana kwetu.Let’s try talk to him” akasema Mathew na kwenda kumchukua Jackson

“Jackson nimekuleta tena hapa tunataka kuzungumza nawe.Kuwa huru usiogope.Sisi

siyo watu wabaya hadi pale tunapolazimishwa kuwa hivyo.Nataka tuzungumze kirafiki sisi na wewe” akasema Mathew na kumtazama Jackson

“Una watoto wangapi Jackson?

“Nina watoto wawili”

“Wanasoma?

“Ndiyo wanasoma”

“Good.Mimi pia ni baba nina watoto wanne.Nadhani unafahamu majukumu ya baba ni kuhakikisha anailinda familia yake dhidi ya hatari yoyote ile na siku zote baba

atafanya kila lililo ndani ya uwezo wake kuhakikisha familia yake wanakuwa salama.Nasema uongo?akauliza Mathew

“Ni kweli kabisa”akajibu Jackson

“Vizuri sana.Kama ilivyo kwa baba kuhakikisha familia inakuwa salama ndivyo ilivyo serikali ambayo ina jukumu la kuhakikisha wananchi wake wanakuwa salama ndiyo maana kuna majeshi na idara mbalimbali za ulinzi yote hii ni katika kuhakikisha wananchi wanaishi kwa amani na

salama.Serikali ilianzisha idara ya SNSA kwa lengo la kupanua zaidi wigo wa ulinzi na usalama wa nchi.Kwa bahati mbaya idara hii nyeti na muhimu sana kwa nchi imeyumba na haitekelezi tena majukumu yake.Mabeberu tayari wamekwisha otesha mizizi yao katika idara hii na sasa wanaitumia kwa malengo yao.SNSA haifanyitena kazi ya kulinda nchi bali imekuwa ni hatari kwa nchi" akasema Mathew na kunyamaza akaichukua komputa ya Ruby akafungua sehemu ya

kuhifadhi picha akaifungua picha ya Melanie Davis akamuonyesha Jackson

“Huyu mwanamke anaitwa Melanie Davis.Ni mshirika wa James Kasai ambaye alitekeleza shambulio la hivi majuzi na kuua wake za marais.James Kasai ana mashirikiano na kikundi cha kigaidi cha IS na anapokea fedha na silaha kutoka kwa kikundi cha IS ambazo zinapita katika mikono ya huyu mwanamke ambaye ni tajiri hivyo moja kwa moja mwanamke huyu ana

mashirikiano na IS.James Kasai na IS wanapanga kufanya shambulio lingine hapa nchini na kwa bahati mbaya idara ya SNSA inatumika katika kufanikisha mipango hiyo.Bosi wako Edwin Mbeko anashirikiana na mtandao huu hatari na anaitumia idara anayoiongoza kufanikisha mipango ya mtandao huu" akasema Mathew na Jackson ambaye alionyesha kustuka kidogo akasema

"Hii picha ya huyu mwanamke uliyenionyesha

amefanana na Yule mwanamke niliyemuona siku ile jioni Edwin aliporejea kutoka Kagera” akasema Jackson

“Una hakika ulimuona mwanamke kama huyu?akauliza Mathew

“Ninakumbuka alifanana na huyu japo alikuwa amevaa miwani lakini anafanana sana na huyu”

“Kama una hakika mwanamke uliyemuona anafanana na huyu hakuna shaka mwanamke huyo ni Melanie Davis na hii inazidi

kuonyesha ukaribu wa Edwin Mbeko na mtandao huu.Yule mwanaume uliyemuona jioni ile ni James Kasai ambaye kwa sasa anashirikiana na kundi la kigaidi la IS.Baada ya James kuingia nchini tulipata taarifa nyingine kwamba kuna mtu anaitwa Khalid Sultan Khalid anatokea kundi la IS anakuja hapa nchini.Huyu ni mtaalamu wa milipuko.Tuliomba idara ya SNSA isaidie katika kumfuatilia Khalid atakapoingia hapa nchini na ikaandaliwa timu maalum

ikaanza kumfuatilia lakini wakati zoezi la kumfuatilia likiendelea mawasiliano kati ya timu hiyo na ofisi kuu yakakatika na tukampoteza Khalid na hadi sasa hatujui mahala alipo.Baada ya kufanya uchunguzi tukagundua kwamba mawasiliano yalikatwa makusudi na mmoja wa wafanyakazi ndani ya SNSA anaitwa Edina na tulipomfuatilia tukakuta ameuawa kwa kupigwa risasi” Akasema Mathew na kunyamaza akamtazama Jackson

“Jackson nimekupa maelezo haya marefu kidogo kwa lengo la kukupa picha ya kile kinachoendelea hapa nchini na katika idara ya SNSA.Edwin Mbeko mkuu wa idara yenu anashirikiana na magaidi ambao wanapanga kufanya shambulio lingine kubwa hapa nchini.Mimi na wenzangu tunapambana katika kuhakikisha tunazuia shambulio hilo lisitokee pamoja na kuwatia nguvuni wahusika wote wa mtandao wa kigaidi hapa nchini.Tukishindwa kuzuia

shambulio hilo damu nyingine itamwagika na utakuwa ni ushindi kwa magaidi.Hatupaswi kuwaacha wakafanikisha mipango yao miovu.Hakuna anayejua shambulio hilo limepangwa kufanywa wapi na lini.Yawezekana ikawa ni kanisani,shuleni au sehemu zenye mikusanyiko mikubwa ya watu na huwezi ukajua yawezekana mwanao akawepo eneo la shambulio na akapoteza maisha.Kama si mwanao basi ni mtoto wa mtu mwingine ambaye ni sawa na

mwanao.Hatupaswi kuacha hilo likatokea na uwezo wa kuwadhibiti watu hao waovu tunao na ndiyo maana tunakuomba ushirikiane nasi katika harakati zetu za kuwazuia watu hawa wabaya kwa nchi yetu.Hatukulazimishi kwani ni misheni ya hatari sana lakini sisi sote unaotuona hapa tumeyatoa maisha yetu kwa ajili ya nchi na hatuogopi kufa.Ukiwa kama mwajiriwa wa idara ya SNSA ambayo malengo yake ni kuhakikisha nchi inakuwa salama hivyo kushiriki katika misheni hii ni

moja ya wajibu wako.Baada ya haya niliyokueleza nini maamuzi yako?akauliza Mathew

“Kaka samahani naomba niwafahamu ninyi ni akina nani? Akauliza Jackson

“Mimi naitwa Mathew Mulumbi na mwenzanu anaitwa Ruby.Sisi hatufanyi kazi katika idara yoyote ya serikali lakini tumeyatoa maisha yetu kwa ajili ya kuisaidia nchi kupambana na wale wote wanaohatarisha usalama wa nchi” akasema Mathew

“Kaka Mathew naomba nikiri kwamba sijawahi kupata mstuko mkubwa kama nilioupata leo kwa maneno uliyonieleza.Sikujua kama kuna hatari kubwa kiasi hiki hapa nchini.Nimekuwa SNSA toka wakati wa Tamar na sasa Edwin na nimekuwa dereva wake kwa miaka mitatu lakini sikuwahi hata mara moja kufahamu siri zake kama ni mtu mbaya namna hii.Aliponielekeza nipeleke gari lake bohari kuu nilijua kuna jambo linaendelea lakini kwa kuwa nilikuwa mtiifu

kwake sikuweza kuhoji chochote kumbe ni mtu mkatili asiye na huruma hata chembe.Umeniambia silazimishwi kujiunga nanyi lakini kwa hiari yangu mwenyewe nataka kujiunga nanyi kuwadhibiti hawa watu wasifanikishe mipango yao” akasema Jackson

“Tutakuamini vipi kama una nia ya dhati ya kujiunga nasi na si kugeuka msaliti?akauliza Ruby

“Kaka hapa amenipa maelezo marefu kidogo na nimeyaelewa ndiyo maana kwa

hiari yangu mwenyewe ninataka kushirikiana nanyi.Kuhusu kuniamini hilo litakuwa ni juu yenu lakini mimi niko tayari kushirikiana nanyi katika jambo hili.Nipeni kazi yoyote nitaifanya.Nini mnataka niwasaidie?akauliza Jackson

“Nataka usiku huu uchukue silaha zenu zote mlizokuja nazo na uzirejeshe ofisini kwenu ili wasiwe na wasiwasi kuhusu ninyi wakikuuliza kuhusu wenzako waeleze kwamba wamekwenda makwao kupumzika.Kesho

asubuhi utawahi kazini na Edwin atakapofika utaweka kifaa tutakachokupa chini ya gari lake na kazi yako itakuwa imekwisha.Endapo itajitokeza tena kazi nyingine basi tutawasiliana lakini utaendelea kuchunguza nyendo za Edwin hapo ofisini na tutakuwa tunakupa maelekezo nini cha kufanya.Unaweza ukalifanya hilo?akauliza Mathgew

“Ndiyo ninaweza kulifanya hilo”

“Good” akasema Mathew

“Vipi kuhusu wenzangu? Nao mtawaachia?

“Hapana tutaendelea kuwashikilia hadi pale tutakapokuwa tumekamilisha misheni yetu na wahusika wote kutiwa nguvuni ndipo tutawaachia.Yule mmoja mgonjwa ataendelea kuhudumiwa hapa hapa na madaktari”akasema Mathew na kumtazama Jackson

“Jackson niangalie vizuri usoni mimi huwa ni mtu mbaya mno pale ambapo utajaribu kutuchezea na kugeuka msaliti.Ninaapa nitakusaka na nitakuua kwa mateso makali

sana.Umenielewa Jackson? Mathew akauliza

“Nimekuelewa kaka.Ninaelewa ninachotakiwa kufanya na sintajaribu kuwasaliti kwani hii ni kwa faida ya nchi yetu.Nitafuata maelekezo yako” akasema Jackson

“Good” akasema Mathew na kwenda ndani akamletea Jackson nguo za kuvaa halafu akamtaka akachukue silaha za wenzake akapewa kifaa ambacho alielekezwa kukiweka chini ya gari la Edwin wakaagana akaondoka.

“Mathew do you trust that guy?Ruby akauliza

“Yes I do.Ruby hatuna namna lazima tumuamini.Atafanya kama tulivyomuelekeza.Kama akifanya tofauti tutatafuta namna nyingine lakini kwa sasa tuendelee kumuamini” akasema Mathew

“What’s next? Akauliza Ruby

“Umekuwa ni usiku mrefu wenye hatari nyingi na mafanikio pia.Kwa sasa tupumzike hadi kesho asubuhi” akasema Mathew

wakaenda kuwatazama madaktari wakawatoa hofu kuhusu usalama wao

****

Saa kumi na mbili za asubuhi ilimkuta Edwin Mbeko amekwisha wasili nyumbani kwa Melanie Davis.

“Karibu sana Edwin.Habari za huko utokako?

“Habari ni njema lakini jana kuna tukio lilitokea katika idara yetu kuna mtu alivamia kwa lengo la kuiba siri za

usalama wa nchi”akasema Edwin na kumsimulia Melanie kila kitu kilichotokea usiku

“Poleni sana kwa tukio hilo.Unahisi huyo mtu kitu gani alikuwa anakitafuta hapo katika ofisi zenu?

“Hakuna anayejua lakini itakuwa ni siri za usalama wa nchi.Nitazungumza na Rais baadae leo ili anieleze kwa kina kuhusiana na huyo mtu ni nani na namna alivyoweza kupata taarifa za ofisi zetu kuvamiwa.Kwa maelezo ya Rais anaonekana kumfahamu huyo mtu kwani alimtaja kwa

jina lake la Mathew Mulumbi na akadai kwamba huyo mtu alikuwa amefariki na ameibuka hivi karibuni kutoka kusikojulikana.Asubuhi ya leo ninakwenda kuonana na Rais amenitaka niende nadhani ni kwa ajili ya kuzungumza suala hilo hilo" akasema Edwin

"Edwin umesema huyo mtu aliyejaribu kuvamia ofisi zenu anaitwa Mathew Mulumbi?akauliza Melania

"Ndiyo.Unamfahamu?

"Hapana simfahamu lakini nimewahi kulisikia jina hilo.Si

jina geni kwangu” akasema Melanie na kukumbuka kitu

“Devotha ! akasema na kuchukua simu yake akajaribu kumtafuta Devotha lakini hakupatikana

“Kwa nini Devotha hapatikani toka jana? Nakumbuka ni yeye aliyewahi kunitamkia hilo jina.Ndiyo nakumbuka hivyo Devotha amewahi kulitamka hilo jina.Tukimpata yeye anaweza akatupa maelezo kuhusiana na huyo Mathew Mulumbi ni nani” akasema Melanie

“Tuachane na hilo suala Melanie tutapata majibu yake baadae tuzungumze kuhusu mipango yetu.Mambo yanakwendaje hapa? Edwin akauliza

“Mambo yanakwenda vizuri.Usiku kucha Khalid ameendelea na kazi ya kuunda bomu na ilipofika saa kumi za alfajiri amemaliza kazi na sasa bomu liko tayari” akasema Melanie na kutabasamu

“Edwin leo ni siku kubwa sana kwetu.Ni siku ya kuandika historia katika nchi hii.Ni mara ya kwanza Rais wa

jamhuri ya muungano wa Tanzania anakwenda kuuawa.Binafsi nina furaha kubwa kwani ninakwenda kulipiza kisasi kwa watu wawili ambao kwa pamoja walishirikiana katika kuwaua wazazi wangu kikatili.Mimi mwenyewe nilinusurika kifo kwa namna ya ajabu lakini malengo yao yalikuwa ni kuua familia nzima.Kama wao walivyotaka kuimaliza familia yangu yote ndivyo itakavyokuwa kwao.Nilianza na wake zao leo ni zamu yao na baadae watafuata watoto

wao.Nitahakikisha ninazisafisha kabisa familia hizi mbili na kusibaki hata na kumbu kumbu yao.Ahsante sana Edwin kwa kunisaidia hadi tumefikia hatua hii.Tusingeweza kufika hatua hii kama si kwa msaada wako.Nakuahidi baada ya tukio la leo utaishi maisha mazuri kama uko peponi.Yale yote tuliyokuahidi utayapata kweli na hata zaidi" akasema Melanie

"Melanie mimi nakushukuru sana kwa kuwa msikivu na kufuata maelekezo

japokuwa mwanzo kulikuwa na kutoelewana kati yetu lakini yale yamekwisha pita.Nashukuru kwa mipango kwenda vizuri.Ninakwenda ikulu asubuhi hii na nitapata ratiba kamili.Nitakapotoka huko nitakuja hapa na sare za jeshi la polisi ambazo ndizo mtu wetu atakayejitoa mhanga atavaa ili aweze kuingiaa ndani ya uwanja wa ndege.Ninao watu wangu ndani ya jeshi la polisi hivyo hakutakuwa na wasiwasi wowote wa jambo hili kufanikiwa" akasema Edwin

“Edwin tafadhali hakikisha hakuna kitu chochote kitakachoingilia na kuharibu siku ya leo.Huu ni mpango mkubwa sana ambao kwa namna yoyote ile lazima ufanikiwe” akasisitiza Melanie

“Melanie nakuhakikishia kwamba kila kitu kitakwenda kama kilivyopangwa.Hakuna kitakachoweza kuvuruga mipango yetu.Andaa shampeni nzuri kwa ajili ya kujipongeza jioni ya leo wakati nchi nzima wanalia” akasema Edwin na kuagana na Melanie alikuwa

anakwenda kujiandaa kwenda ikulu kuonana na Rais.

“Mathew Mulumbi ! akawaza Melanie baada ya Edwin kuondoka

“Hili si jina geni kulisikia.Devotha aliwahi kulitamka siku moja na sikumbuki alikuwa anazungumza kuhusu nini” akawaza Melanie

“Hili jina la Mathew Mulumbi halina mahusiano na Gosu Gosu au Penielea?akajiuliza

“Nakumbuka kama Devotha alilitaja jina hili

wakati tukizungumza kuhusu aidha Peniela au GosuGosu” akawaza Melanie na kuchukua simu tena akampigia Devotha lakini simu yake haikupatikana.

“Where are you Devotha?Kuanzia jana haupatikani simuni umekwenda wapi?Kwa nini hujatupa taarifa? Akajiuliza Melanie

“Nimepata wazo ngoja nimpigie simu Peniela nimuulize kama anaweza kumfahamu huyu Mathew Mulumbi.Sifahamu kwa nini

nimestuka baada ya kulisikia jina hili” akawaza Melanie na kufungua katika kitabu chake cha kumbukumbu akaziandika namna za simu za Peniela katika simu yake akampigia

“Hallow” ikasema sauti ya upande wa pili

“Hallow Peniela” akasema Melanie

“Nani mwenzangu?akauliza Peniela

“Ni mimi Melanie Davis”

“Oh Melanie habari za Dar es salaam?

“Nzuri kabisa Peniela.Habari za Paris?

“Huku kwema pia.Ni mara ya kanza tunawasiliana toka umefika Dar es salaam”

“Ndiyo Peniela hatujawasiliana tangu nimeondoka Paris”

“Melanie nina hamu sana ya kuzungumza nawe mambo mengi lakini naomba nikupigie baada ya dakika kumi na tano kuna mgeni muhimu niko naye tuna mazungumzo ya kibiashara.Usiende mbali tafadhali” akasema Peniela

“Ahsante Peniela samahani kwa usumbufu”

“Hakuna usumbufu wowote Melanie hata mimi nimefurahi sana kwa kunipigia.Nitakupigia ili tuzungumze mambo mengi.Kuna makampuni mengine ambayo nataka kuyauza.Nisubiri kwa dakika ishirini” akasema Peniela

“Sawa Peniela ukiwa tayari nipigie simu” akasema Melanie na kukata simu

“Shetani jike wewe leo umejileta mwenyewe .Umekwisha ! akasema Peniela baada ya kukata simu na bila kupoteza muda akampigia

simu Peterson ambaye anamiliki kampuni ya wapelelezi wa kujitegema.

“Peniela habari za asubuhi” akasema Peterson

“Peterson habari ni nzuri.Samahani kwa usumbufu wa asubuhi hii”

“Usijali Peniela tayari niko kazini”

“Kuna simu nataka kuifuatilia nchini Tanzania na kujua mtu huyo yuko sehemu gani.Nakuhitaji hapa mara moja uje na vifaa vyako kwa ajili ya kuifuatilia simu hiyo” akasema Peniela

“Sawa Peniela ninakuja hapo nyumbani kwako”

“Hautaweza kuwahi kwa muda ninaoutaka.Ninatuma helkopta ije ikuchukue” akasema Peniela na kumuelekeza Peterson sehemu ya kwenda kupanda helkopta itakayompeleka nyumbani kwa Peniela.

****

Peterson alishuka katika helkopta iliyokwenda kumchukua akiwa na sanduku

jeusi na kuelekea katika jumba la Peniela.

“Karibu sana Peterson” akasema Peniela wakaelekea katika ofisi yake ya nyumbani

“Kama nilivyokueleza simuni kuna mtu nataka kumfuatilia kujua mahala alipo nchini Tanzania”

“Hiyo ni kazi ndogoPeniela” akasema Peterson huku akifungua sanduku lake akatoa kompyuta ndogo na kuweka sawa program zake akaweka kifaa kingine mezani na kumtaka

Peniela ampigie simu mtu anayemfuatilia

“Jitahidi kumuweka kwa muda mrefu katika laini ya simu” akaelekeza Peterson na Peniela akampigia simu Melanie

“Hallo Peniela” akasema Melanie

“Melanie samahani kwa kukukatisha wakati ule”

“Usijali Peniela.Ahsante kwa kupiga”

“Sasa niko huru unaweza ukanieleza kile ulichotaka kunieleza”

“Umewasiliana na Devotha kuanzia jana?akauliza Melanie

“Devotha?! Peniela akauliza

“Ndiyo.Umewasiliana naye ?

“Hapana sijawasiliana naye.Kuna nini?

“Nimejaribu kumtafuta kuanzia jana na hapatikani simuni”

“Nitajaribu kumtafuta nikimpata nitamjulisha kuwa unamtafuta”

“Ahsante sana Peniela.Jambo lingine kuna kitu nataka kuuliza”

“Uliza Melanie usihofu”

“Kuna mtu anaitwa Mathew Mulumbi unamfahamu?

“Mathew Mulumbi?

“Ndiyo unamfahamu?

“Hapana simfahamu huyo mtu.Ni nani ?akauliza Peniela

“Hata mimi simfahamu lakini nimewahi kulisikia mahali hilo jina likitamkwa ndiyo maana nikaona nikuulize kama unamfahamu”

“Hapana simfahamu huyo mtu lakini kama unamuhitaji sana ninaweza kukusaidia

kumtafuta.Ni mfanya biashara? Akauliza Peniela

“Hata mimi sifahamu Peniela kuhusu huyo mtu.Simfahamu na sina taarifa zake”

“Sasa imekuaje ukamuulizia wakati humfahamu? Akauliza Peniela

“Nimesikia watu wakizungumza kama alifariki na ameonekana hai.Niliposikia jina hilo nikakumbuka nimewahi kulisikia mahali lakini sikumbuki wapi ndiyo maana nikakuuliza”

“Jaribu kumuuliza Gosu Gosu yeye anaweza kuwa na taarifa nyingi za watu mbali mbali hapo Dar es salaam”

“Gosu Gosu am…….” Akasema Melanie na kusita

“Amefanya nini Gosu Gosu? Akauliza Peniela

“Alivamiwa na majambazi akapigwa risasi”

“Mungu wangu ! Peniela akaonyesha mstuko kama vile hafahamu chochote

“Vipi hali yake?akauliza

“Hali yake si nzuri nitaendelea kukujulisha

maendeleo yake” akasema Melanie

Peterson akamfanyia ishara Peniela kwamba tayari amekamilisha zoezi

“Melanie taarifa hizi za Gosu Gosu zimenistua sana.Naomba endelea kufuatilia kwa karibu hali yake utanijulisha.Nitakuwa na safari ya Tanzania wiki ijayo tutazungumza masuala ya biashara kuna makampuni yangu mengine nataka kuyauza.Tutazungumza nitakapokuja” akasema Peniela

“Sawa Peniela.Nitafurahi sana kuonana nawe tena.Utakapokuja tafadhali usiondoke bila kuonana nami” akasema Melanie na Peniela akakata simu

“Umepata mahala alipo huyu niliyekuwa nazungumza naye simuni?akauliza Peniela

“Ndiyo tayari nimepata mahala alipo nchini Tanzania” akasema Peterson na kumuonyesha Peniela ramani katika kompyuta yake

“Yuko katika jiji la Dar es salaam mahala hapa kwenye

mduara mwekundu” akasema Peterson

“Ahsante sana Peterson.Naomba unitumie picha hiyo katika simu yangu” akasema Peniela kisha akaagana na Peterson akapanda helkopta kurudishwa mahala alikochukuliwa.Mara tu Peterson alipoondoka Peniela akampigia simu Mathew Mulumbi.

“Peniela” akasema Mathew

“Mathew habari za Dar es salaam?

“Huku kwema.Unaendeleaje na watoto?

“Sisi tuko vizuri.Mathew uko katika nafasi nzuri tuzungumze?

“Ndiyo Peniela”

“Ninakutumia ramani katika simu yako sasa hivi.Ukitazama katika mduara mwekundu ni mahala alipo Melanie Davis” akasema Peniela na kumueleza Mathew kila kitu kilichotokea hadi akafahamu mahala alipo Melanie

“Peniela nakushukuru mno.Sipati maneno mazuri ya kueleza shukrani zangu kwa haya uliyonifanyia” akasema Mathew

“Mathew ni mimi ambaye nina deni kubwa kwako la kulipa kwa mambo uliyonifanyia hivyo kila pale utakapohitaji msaada wangu usisite kunijulisha” akasema Peniela na kuagana na Mathew

“Sikutegemea kama Peniela anaweza akawa na msaada mkubwa namna hii” akawaza Mathew na kuifungua picha aliyotumiwa na Peniela

ilikuwa ni ramani ya jiji la Dar es salaam.

“Melanie Davis ! Hatimaye umeingia katika mikono yangu ! akasema Mathew huku akiuma meno kwa hasira.Akamfuata Ruby chumbani alikokuwa anaoga akafunga maji

“Kuna nini Mathew?

“Ruby tumepata mahala alipo Melanie Davis”akasema Mathew na kumueleza namna Peniela alivyoweza kugundua mahala alipo Melanie.

“Siku njema huonekana asubuhi.Itakuwa siku ndefu na ngumu sana”akasema Ruby

“Kweli ni siku ngumu sana.Leo ni sisi au wao.Mbio zao zimefika ukingoni”

“Nini tunakifanya baada ya kujua mahala alipo Melanie Davis?Ruby akauliza

“Kwanza ni kuchunguza na kujiridhisha kama kweli Melanie Davis anaishi mahala hapo.Tukisha kuwa na uhakika kwamba Melanie Davis Yuko ndani ya nyumba hiyo tutaingia katika hatua ya pili lakini kwanza lazima

tujiridhishe.We’re going there.Tutaweka kambi karibu na nyumba hiyo na kufuatilia kila kinachoendelea ndani ya nyumba hiyo.Ninayo kamera ya siri yenye muundo wa ndege ambayo tutairusha ndani ya nyumba na itatupa picha ya kila kinachoendelea humo ndani.Si rahisi kugundulika kama ni kamera kwani inafanana sana na ndege wa kawaida anayeruka angani” akasema Mathew

“SNSA wana drone kubwa ambazo hurushwa angani kila asubuhi na kuzunguka sehemu

mbali mbali za jiji na huwasaidia kupata picha mbali mbali.I can hack one drone”akasema Ruby

“We’re done with SNSA.Wanaweza wakagundua kwamba tunatumia drone yao na wakavuruga misheni yetu.Hatuhitaji drone ya SNSA.Ninayo pia kamera nyingine ndogo ambayo tutaitumia.Ni aina mpya ya kamera za kijasusi ambayo inafanana sana na nyuki.Kamera hii inaweza ikaingia hadi ndani ya nyumba

na kutupa picha nzuri” akasema Mathew

“Kwa kamera hizo mbili hatuna haja ya kutumia drone ya SNSA” akasema Ruby huku akifuta maji na kutoka bafuni

****

“Jackson jiandae nataka unipeleke ikulu ninakwenda kuonana na Rais” Edwin Mbeko akamwambia Jackson dereva wake mara tu alipowasili katika ofisi za SNSA akitokea nyumbani kwa Melanie Davis.

Jackson akaenda katika gari la Edwin akaanza kulifuta vumbi.Akatazama pande zote hakukuwa na mtu katika maegesho yale ya viongozi akachukua kile kifaa alichopewa na Mathew akakibandika chini ya gari halafu akampigia simu Mathew

“Kaka tayari nimekibandika kile kifaa katika gari la Edwin” akasema Jackson

“Good job Jack.Nini kinaendelea hapo SNSA kwa sasa?

“Edwin anataka nimpeleke ikulu asubuhi hii”

“Sawa Jack endelea kutujulisha kila mahala anakoelekea na sisi tutaendelea kufuatilia kupitia hicho kifaa ulichokiweka katika gari lake” akasema Mathew na kukata simu

“Jackson tayari ameweka kile kifaa katika gari la Edwin” Mathew akamwambia Ruby wakati wakijiandaa kuondoka nyumbani kwao kwenda kwa Melanie.Ruby aliyekuwa pembeni ya Mathew akiwa na

kompyuta yake akakiona kile kifaa alichokiweka Jackson

“Tayari nimekiona.Sikutegemea kama angeweza kufanya tulivyomuelekeza”

“Unatakiwa kujifunza kuwaamini watu.Nitakufundisha namna ya kumtambua mtu ambaye anasema ukweli” akasema Mathew na ujumbe ukaingia katika simu yake akausoma ulitoka kwa Dr Masawe

“*Please stop calling me.I’m done with you !*

“Dr Masawe hatarejea tena.Kitendo cha jana kutekwa na Edwin tayari kimempa uoga mkubwa kuendelea kushirikiana nasi.Hakuna tatizo tutaendelea kuwatumia wale madaktari waliobaki ambao wamekubali kuendelea kumuhudumia Gosu Gosu.Nitawalipa mara mbili zaidi ya tulivyokubaliana” akasema Mathew

****

Edwin Mbeko aliwasili ikulu alikoitwa na Rais.

“Edwin karibu sana.Nashukuru umefika kwa wakati” akaanzisha maongezi Dr Fabian

“Nashukuru sana mheshimiwa Rais”

“Nimetaka uje asubuhi hii tuzungumze kwa sababu nina ratiba ndefu siku ya leo.Nina ugeni wa marais wa Uganda na jamhuri ya kidemokrasia ya Congo.Tutakuwa na kikao muhimu sana hivyo mazungumzo yetu yatakuwa mafupi sana” akasema Dr Fabian

“Edwin nimekuta hapa kuja kukujulisha rasmi kwamba kuanzia sasa wewe utakuwa ndiye mkurugenzi mkuu wa SNSA.Umekaimu nafasi hii kwa miaka mitatu na umefanya kazi nzuri sana hivyo kwa mamlaka yangu nimekuteua kuwa mkurugenzi mkuu na msaidizi wako nitamteua hapo baadae” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais umenistua sana.Sikutegemea kabisa ama ungeweza kuniteua kushika nafasi hiyo” akasema Edwin

“Unastahili nafasi hiyo” akasema Dr Fabian

“Nashukuru mno mheshimiwa Rais kwa kuniona ninafaa”

“Unafaa Edwin.Umekuwa katika nafasi ya ukaimu kwa miaka mitatu na hakujawahi kutokea tatizo lolote.Nilifanya makosa makubwa kuamua kumleta mtu ambaye haijui vyema idara ile na tazama mambo yaliyotokea.Ndani ya siku mbili tu ambazo Annabel amekuwa katika nafasi ya ukurugenzi yametokea mambo ya ajabu sana.Ameingiza watu

wasio watumishi wa idara.Vimetokea vifo vya wafanyakazi wawili n.k.Kama angeendelea kwa mwezi mzima sifahamu nini kingetokea hivyo sitaki tena kumuona katika idara ile.Ulifanya vizuri sana kutumia kanuni kumuondoa katika nafasi yake.”

“Mheshimiwa Rais ninashukuru sana kwa uteuzi huu na ninakuahidi kufanya kazi iliyotukuka kabisa”akasema Edwin

“Edwin nataka ukafanye kazi .Nataka nchi iwe salama” akasema Dr Fabian

“Usiwe na hofu mheshmiwa Rais.Idara yetu hailali watu wanafanya kazi saa ishirini na nne kuhakikisha nchi inakuwa salama”

“Good.Kubwa nililokuitia hapa ni hilo la kukupa hiyo taarifa nzuri” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa rais kwa mara nyingine ninashukuru sana na ninakuahidi kazi nzuri.Hata hivyo nina swali dogo kama utaniruhusu

kuuliza”akasema Edwin na Dr Fabian akaitazama saa yake kisha akasema

“Uliza”

“Ni kuhusiana na tukio la jana usiku.Uliniambia mtu ambaye alivamia ofisi zetu anaitwa Mathew Mulumbi.Ni nani huyo mtu?

“Mathew Mulumbi hata mimi simfahamu vyema lakini wanaomfahamu wanadai aliwahi kufanya kazi katika idara ya ujasusi kabla ya kuanza kujishughulisha na biashara zake binafsi.Licha ya kuacha kazi katika idara ya

ujasusi lakini inadaiwa Mathew ameendelea kufanya kazi za ujasusi kwa kujitegemea na inasemekana miaka mitatu iliyopita alishiriki katika misheni ya kuwakomboa mateka waliotekwa na kundi la IS na mmoja wa mateka hao akiwa ni mtoto wa Rais aliyemaliza muda wake kwa bahati mbaya katika misheni hiyo inadaiwa alifariki dunia lakini kwa mshangao mkubwa Mathew ameibuka wiki hii kutoka kusikojulikana.Mambo anayoyaongea na kuyafanya

yanatia shaka sana kama kweli ni binadamu wa kawaida au ni mzimu unatuchezea.Kwa mfano jana aliwezaje kutoka ndani ya jengo lile bila kuonekana? Akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais hata sisi tumejiuliza alitokaje ndani ya jengo lile bila kuonekana?Lakini mheshimiwa Rais bado kuna kitu kimoja nataka kukifahamu kama itakupendeza “

“Sema Edwin usiogope”

“Nataka kufahamu chanzo cha taarifa ile ya Mathew kuingia ndani ya jengo letu” akasema Edwin

“Ni Annabel”

“Annabel?Edwin akashangaa

“Ndiyo.Yeye ndiye aliyeniambia kwamba anamsaidia Mathew kuingia ndani ya ofisi zenu na ndipo nikakupigia.Hiyo ni moja ya sababu kubwa iliyonifanya nikamuondoa katika nafasi ile ya ukurugenzi”

“Mheshimiwa Rais Annabel alikueleza Mathew

alikuja kutafuta nini katika ofisi zetu?akauliza Edwin

“Hakunieleza sababu za kumsaidia Mathew kuingia SNSA”

“Mheshimiwa rais utaniwia radhi lakini kwa hiki alichokifanya Annabel na Mathew wamekwisha ingia kwenye orodha ya watu hatari kwa usalama wa nchi.Annabel japo amekuwa mkurugenzi wa SNSA kwa siku mbili lakini ameyafahamu mambo mengi ya idara,tayari amezifahamu siri nyingi za usalama wa nchi na kama amemsaidia Mathew

kuingia ndani ya ofisi zetu ni wazi kuna siri wanazitafuta na watajaribu kila njia hadi wafanikiwe lengo lao” akasema Edwin

“Unalolisema Edwin ni la kweli kabisa.Tayari Annabel amekwisha onekana kuwa hatari hivyo tunatakiwa kuanza kummulika na kujua mwenendo wake.Nitakuita tena kesho tutalizungumza hili kwa kirefu zaidi” akasema Dr Fabian huku akinyanyuka kitini

“Kwa heri mheshimiwa rais,jivinjari ikulu mara ya

mwisho kwani kabla ya machweo leo tayari utakuwa umerejea kwa muumba wako” akawaza Edwin wakati akiagana na Rais

****

Mathew na Ruby waliegesha gari lao mita chache kutoka geti la kuingilia jumba la Melanie Davis.Ni mtaa wanaoishi matajiri wakubwa hivyo kulikuwa na ukimya mkubwa.Kulikuwa na magari mawili yameegeshwa kandoni mwa barabara hivyo

gari la akina Mathew likawa la tatu.

“Kwa mujibu wa ramani yetu,Melanie Davis alizungumza na Peniela akiwa katika nyumba ile pale” akasema Ruby huku akiitazama ramani yake

“Tunarusha kwanza kamera ya ndege ichunguze ndani ya nyumba ile kuna nini halafu tutarusha ile kamera ndogo ya nyuki” Akasema Mathew na kufungua boksi lililokuwa na ndege wa bandia aliyefungwa kamera.Kwa kumtazama kwa haraka haraka

isingekuwa rahisi kujua kama ndege ile ni bandia kwani alionekana kama ndege halisi mwenye rangi za kuvutia.Mathew akatazama pande zote kama kuna watu wanaowatilia shaka halafu akaiwasha kamera ile akafungua dirisha na kumrusha Yule ndege huku Ruby akiwa na kifaa cha kumuongozea.Ndege Yule alipaa na kutua juu ya paa la nyumba ya Melanie na eneo lote la nyumba ile likaanza kuonekana.Hakukuwa na mtu yeyote nje.Kulikuwa na

bustani nzuri ilyopandwa maua mazuri na eneo kubwa la nje lilipandwa majani mazuri ya kijani.Ruby akaizungusha kamera ile upande wa nyuma ya nyumba na mwanamke mmoja akaonekana akifanya usafi.Ruby akachukua picha ya mwanamke Yule akaiingiza katika programu na kumtafuta lakini hakuweza kupatikana

“Mwanamke Yule hayupo katika mfumo wowote wa serikali” akasema Ruby

“Tumekuja sehemu husika.Hii ni kazi ya mtandao wa akina Melanie.Watu wao

wengi hawajulikani katika mifumo ya serikali” akasema Mathew.Ruby akampeleka ndege Yule juu ya ukuta akaielekeza kamera katika mlango mkuu wa kuingilia ndani ili waweze kushuhudia kila anayeingia na kutoka kupitia mlango ule mkubwa

“Time to send in our second camera” akasema Mathew na kufungua sanduku lingine dogo akatoa kiboksi kidogo ambacho ndani yake kulikuwa na kamera ndogo yenye muundo sawa na nyuki.

“Teknolojia imekua sana zama hizi hadi vitu kama hivi vinatengenezwa.This is wonderfull” akasema Ruby

“Hizi ni kamera za hali ya juu za kijasusi ambazo zinatumiwa na mataifa makubwa” akasema Mathew na kuiwasha ile kamera ndogo

“Sweet bee go inside and do a nice job” akasema Mathew akamrusha Yule nyuki nje Ruby akaanza kumuongoza kuelekea ndani huku wakipata picha nzuri

“This is amazing.Sikutegemea kama

nyuki Yule anaweza akarusha picha nzuri namna hii” akasema Ruby na kumuongoza nyuki Yule hadi katika mlango mkubwa wa mbele akitafuta nafasi ya kumuingiza ndani lakini hakukuwa na upenyo wowote.Akamzungusha nyuma ya nyumba ambako nako tayari mlango ulikuwa umefungwa.

“Betri ya huyu nyuki inaweza kudumu kwa muda gani? Ruby akauliza

“Saa tatu hadi nne.Tutaendelea kusubiri hadi pale mlango

utakapofunguliwa” akasema Mathew

****

Baada ya kutoka ikulu Edwin Mbeko alimuelekeza Jakson ampeleke katika nyumba za maafisa wa polisi Mikunguni.

“Jackson ahsante kwa kazi nzuri mliyofanya jana usiku” akasema Edwin

“Usijali mkuu.Muda wowote utakaponituma kazi yoyote nitahakikisha inafanyika kikamilifu”

“Nafurahi kusikia hivyo.Ninakuahidi kukuweka sehemu nzuri sana kwani kwa sasa mimi ndiye mkurugenzi.Rais ameniteua leo niwe mkurugenzi wa SNSA” akasema Edwin

“Hongera sana mkuu.Unafaa kuongoza idara ile.Rais hajakosea kukupa nafasi hiyo”

“Ahsante sana Jack” akasema Edwin

“Vipi kuhusu Yule mama tuliyetambulishwa kuwa ndiye mkurugenzi?Atarudi tena SNSA?akauliza Jackson

“Yule habari yake imekwisha.Hatarejea tena SNSA.Ni mwanamke hatari sana yule na ndiye aliyesaidiana na Yule jaama aliyeingia katika ofisi zetu jana usiku.Ni hatari kabisa kwa usalama wa nchi” akasema Edwin

“Nini walikuwa wanakitafuta katika ofisi zetu jana? Akauliza Jackson

“Wanatafuta siri za usalama wa nchi.Kuna mtu anaitwa Mathew Mulumbi nimeambiwa ndiye ambaye alivamia ofisi zetu.Tukimpata

huyo atatueleza alichokuwa anakitafuta katika ofisi zetu” akasema Edwin

“Mathew Mulumbi ni nani? Akauliza Jackson

“Hata mimi simfahamu lakini nimeambiwa aliwahi kufanya kazi katika idara ya ujasusi na baadae akapotea sasa amerudi tena na haijulikani ametoka wapi.Ni mtu hatari sana kwa usalama wa nchi” akasema Edwin na simu yake ikaita akaipokea

“Hallo Melanie” akasema Edwin

“Edwin bado uko ikulu? Huku kila kitu tayari na ni wewe tunayekusubiri hivi sasa” akasema Melanie

“Tayari nimekwisha toka ikulu hivi sasa ninakwenda kuchukua zile sare halafu nitakuja hapo muda si mrefu” akasema Edwin na kukata simu halafu akamtaka Jackson kuongeza mwendo zaidi ili wawahi kufika mahala wanakoelekea

Walifika katika nyumba za maofisa wa polisi Mikunguni Edwin akamuelekeza Jackson kuegesha gari nje ya nyumba

Fulani ya mmoja wa maofisa wa polisi halafu akashuka na kugonga kengele ya geti na ndani ya muda mfupi mlango mdogo wa geti ukafunguliwa akaingia ndani.

Mara tu Edwin alipoingia ndani ya ile nyumba Jackson akatoka nje ya gari akampigia simu Mathew

“Jackson nini kinaendelea kwa upande wako?Mathew akauliza baada ya kupokea simu

“Kaka nimekupigia simu kukujulisha kuwa tayari tumetoka ikulu na Edwin

amenielekeza nimlete hapa Mikunguni katika nyumba za maafisa wa polisi hivi sasa ameingia katika mojawapo ya nyumba hizi.Kuna mambo mawili yametokea kwanza Rais amemteua kuwa mkurugenzi mkuu wa SNSA pili tukiwa garini alipigiwa simu na mtu anaitwa Melanie.Nadhani atakuwa ni Yule Melanie uliyenionyesha picha yake jana unayemtafuta.Sikusikia upande wa Melanie alichokizungumza lakini kwa upande wa Edwin nilimsikia akisema kwamba tayari

ametoka ikulu na sasa anakwenda kuchukua zile sare kisha atamfuata.Kwa sasa ameingia ndani ya nyumba yenye kibao Block D 39”

“Ahsante sana Jackson kwa kazi nzuri endelea kumfuatilia na kutujulisha kila kinachoendelea” akasema Mathew na kukata simu

“Edwin amepewa ukurugenzi wa SNSA na Rais” Mathew akamwambia Ruby

“Hakuna tatizo.Anamuamni ndiyo maana amempa nafasi hiyo lakini bado hajui kama Edwin

ni nyoka wa vichwa viwili.Siku akilijua hilo tayari atakuwa amechelewa sana” akasema Ruby

“Ukiacha hilo Jackson anasema wakiwa garini Edwin alipigiwa simu na Melanie na katika mazungumzo yao Edwin akamwammbia Melanie kwamba anafuatilia sare”

“Sare?Ruby akauliza

“Ndiyo amesema anafuatilia sare na sasa yuko Mikunguni ambako wanakaa maafisa wa polisi.Kuna kitu hapa kinajitokeza.Je huko mikunguni ndiko amefuatilia

hizo sare?Je ni sare zipi hizo? Akauliza Mathew na mara katika kioo cha mashine ya kuongozea ile kamera ya ndege ukaonekana mlango mkubwa wa mbele ya nyumba ukifunguliwa.Mtu mmoja aliyevaa fulana ya kukatwa mikono akiwa na sigara mkononi akatoka.

“James Kasai ! akasema Mathew

Haraka haraka Ruby akacheza na kompyuta yake akaichukua picha ya yule mtu aliyetoka ndani ya ile nyumba akaiingiza katika programu ya

utambuzi na majibu yakaja kwamba kwa asilimia mia moja Yule ni James Kasai

“Oh my God it’s him ! akasema Ruby

James Kasai akiwa na sigara yake alikwenda kuketi katika bustani mahala kulikokuwa na viti vzuri vya kupumzika.Baada ya muda mlango ukafunguliwa akatoka Yule mwanamke ambaye walishindwa kumtambua awali akiwa amebeba sinia lenye chupa kubwa ya mvinyo na glasi akamuwekea James mezani na kummiminia kidogo

katika glasi.James akavuta sigara akapuliza moshi mwingi halafu akainua glasi ya mvinyo akanywa akaendelea kuvuta sigara yake.

“Enjoy life for the last time bastard ! akasema Mathew akimtazama James kwa hasira.Mlango ukafunguliwa akatoka mwanamke ambaye hakukuwa na haja ya kutumia programu ya utambuzi kumtambua.Wote walimtambua haraka haraka alikuwa ni Melanie Davis

“That’s Melanie Davis.Yule ndiye shetani wa kike

anayetusumbua ambaye tumekuwa tukimsaka bila mafanikio” akasema Ruby

“Kwa nini mwanamke mzuri namna hii akavaa roho ya kishetani anaua watu bila ya huruma?akauliza Mathew

“Nani alikwambia shetani ana sura mbaya?Kumbuka shetani aliwahi kuwa malaika kabla ya kufukuzwa kwa hiyo usishangae ukiona mwanamke mzuri kama huyu ana roho ya kishetani” akasema Ruby

“Your days are over Melanie.Leo ni wewe au sisi ! akasema Mathew akiendelea

kumtazama Melanie akitembea kwa kuringa kuelekea mahala alipokuwa James Kasai ambaye aliinuka akavuta kiti Melanie akaketi halafu akammiminia kinywaji katika glasi

“What a gentleman ! akasema Ruby huku akitabasamu.Mathew akageuka akamtazama na wote wakajikuta wakitabasamu

Melanie na James waliendelea na mazungumzo.

“Natamani nisikie kile wanachokizungumza.Tunawez a kumsogeza Yule nyuki karibu

kusikia maongezi yao”
akasema Mathew na Ruby
akairusha kamera ile hadi
karibu na mahala walipokuwa
akina Melanie akaishusha
katika majani halafu nyuki
Yule akaanza taratibu
kutembea katika majani hadi
chini ya meza na sauti za
maongezi ya Melanie na James
Kasai zikaanza kusikika

“Nimependa sana Dar es
salaam ! akasema James Kasai

“Usijali utakuja na
kuondoka Dar es salaam kila
pale utakapohitaji.Unaweza
ukaja kila mwisho wa wiki

ukastarehe kisha ukaondoka kurejea Uganda.Uwezo huo upo kwani tunaweza kufaya chochote ndani ya nchi hii”akasema Melanie

“Ningefurahi sana kama ingekuwa hivyo.Naipenda Tanzania na ninaishambulia kwa kuwa imebidi iwe hivyo lakini sikuwahi kuwa na mpango wa kushambulia” akasema James

“Hata mimi ninaipenda Tanzania.Nimeishi na kusoma hapa,watu wake ni wakarimu,watanzania hawana ugomvi na mtu yeyote.Kwa

ujumla Tanzania ni nchi nzuri wabaya ni viongozi wake ! Lakini baada ya leo mambo yatatulia” akasema Melanie na mmoja watumishi wake akamfuata akamjulisha kwamba anahitajika ndani.

“Melanie anadai ameishi na kusoma hapa.Ni nani huyu mwanamke?Mbona inaonyesha ametokea Ufaransa? Akauliza Ruby

“Kuna jambo kubwa liko nyuma ya huyu mwanamke na leo lazima tulifahamu.Melanie Davis ni zaidi ya tunavyomdhania.Halafu katika

maongezi yao kuna kitu amekiongea Melanie amesema baada ya leo mambo yatatulia.Kauli hii inaashiria kuna kitu kinakwenda kutokea leo.What are they planning today?akauliza Mathew na simu yake ikaita alikuwa ni Jackson

“Jackson nipe habari” akasema Mathew

“Edwin ametoka katika ile nyumba alimoingia akiwa na sanduku dogo.Hakutaka niongozane naye tena amenipa shilingi laki moja nitafute

usafiri nirejee ofisini”akasema Jackson

“Ahsante sana Jack kwa taarifa.Usiondoke maeneo hayo.Fanya utafiti kujua nyumba hiyo ni afisa gani wa polisi anaishi na mwenye cheo gani halafu nijulishe mara moja” akasema Mathew

“Sawa kaka” akasema Jackson na kukata simu

“Edwin amekwisha ondoka katika ile nyumba alimoingia.Hajataka kuongozana na Jack bali amempa shilingi laki moja atafute usafiri

mwingine.Ametoka akiwa na sanduku dogo mfuatilie tujue anaelekea wapi” akasema Mathew na Ruby akaigeukia kompyuta yake akaanza kukifuatilia kile kifaa kilichowekwa katika gari la Edwin.

“Kama utakumbuka Jack alisema wakati wanaelekea Mikunguni Edwin alizungumza na Melanie simuni na akamjulisha kwamba anafuatilia sare.Kwa taarifa ya sasa hivi Jack anadai kwamba Edwin alitoka ndani ya hiyo nyumba alimoingia

akiwa na sanduku dogo.Je humo alimoingia ambamo ni kwa afisa wa polisi ndimo alimokwenda kuchukua hizo sare? Je ni sare zipi hizo? Akauliza Mathew

“Mathew ukiunganisha hilo la sare na yale maneno ya Melanie kwamba “*baada ya leo*” unapata picha kwamba kuna kitu kinaandaliwa leo na hawa watu”akasema Ruby

“Bado kuna mtu mmoja hatujathibtisha kama yuko ndani ya nyumba hii Khalid Sultan Khalid.Je yumo humu ndani au yuko sehemu

nyingine? Lakini taarifa zilionyesha kwamba anakuja Tanzania kuonana na James Kasai hivyo basi kama James yuko humu ndani kuna uwezekano mkubwa Khalid akawa mle ndani.Tuendelee kuvuta subira tutajua kila kitu” akasema Mathew

****

Edwin Mbeko alipotoka Mikunguni akaelekea moja kwa moja nyumbani kwa Melanie Davis.Mathew na Ruby waliendelea kumfuatilia

bila yeye kufahamu na kugundua alikuwa anaelekea maeneo yale.Alipofika katika geti la nyumba ya Melanie gari lake likasimama kwa sekunde kadhaa halafu geti likafunguliwa akaingia ndani.Kamera mbili za akina Mathew zilizokuwa mle ndani zote zikaelekezwa katika mlango mkubwa wa kuingilia sebuleni.Gari likasimama mlango ukafunguliwa akashuka Edwin Mbeko akafungua mlango wa nyuma akachukua sanduku dogo

kisha akaingia ndani haraka haraka

“Sanduku lile dogo ndilo alilotoka nalo kule Mikunguni kwa mujibu wa Jackson.Natamani nikaingie mle ndani nishuhudie kile kinachoendelea lakini tutaharibu mambo” akasema Mathew

“Tuwe wavumilivu na tutajua tu kila kinachoendelea mle ndani” akasema Ruby

Edwin alipoingia mle ndani akasalimiana na James Kasai na Melanie

“Kwema huko utokako?akauliza Melanie

“Kwema kabisa.Kuna habari nzuri.Rais ameniteua kuwa mkurugenzi wa idara ya SNSA”

“Wow ! hongera sana”

“Ahsante.Kwa sasa tuna nguvu kubwa na tunaweza kufanya kila tutakalo”

“Imekuwa vyema amekukabidhi cheo kwa mara ya mwisho”

“Marais wa Uganda na jamhuri ya kidemokrasia ya Congo tayari wamewasili na hivi sasa kikao kinaendelea

ikulu Dar es salaam” akasema Edwin

“Jenerali Akiki alinipigia simu wakati anaondoka Kampala kuja Dar es salaam” akasema Melanie

“Melanie hii ni siku yetu kubwa sana na kizuri ni kwamba mipango yetu yote inakwenda vizuri.Inapendeza sana kama kila mnachokipanga kinakwenda vyema” akasema Edwin na kufungua sanduku alilokuja nalo na kutoa sare za jeshi la polisi kikosi cha kutuliza ghasia.Wakazikagua halafu

wakaelekea katika chumba alimokuwamo Khalid Sultan.Akasalimiana na Edwin halafu akamuonyesha bomu alilolitengeneza ambalo lilifanana na fulana za kuzuia risasi wavaazo jeshi la polisi.

“Bomu ambalo niliitwa kulitengeneza ni hili hapa limekamilika na kazi imebaki upande wenu kulilipua.Hili ni bomu kubwa na madhara yake ni makubwa pia.Nina hakika wale wote waliolengwa kuuawa na bomu hili hawatasalimika.Nimetengeneza pia bomu lingine la akiba

kwa ajili ya siku nyingine” akasema Khalid halafu akaenda kumchukua Abdi kijana wa miaka ishirini na nane kutoka katika kundi la Alshabaab .

“eabdi kl shay’ jahiz wahan alwaqt alan lildhahb” (Abdi kila kitu kimekamilika na muda wa kuingia kazini umewadia) Khalid akamwambia Abdi akitumia lugha ya kiarabu.

“ana mustaeidum” (niko tayari” akajibu Abdi

“eabdi eayilatuk satatrik hayatan fakhiratan libaqiat

hayatihim bsbb ma tafealuh alyawm (Abdi familia yako itaishi maisha ya kifahari kwa maisha yao yote kwa sababu ya hiki unachokwenda kukifanya leo” akasema Khalid

“amiyn ! akasema Abdi halafu akavua mavazi aliyokuwa amevaa akaanza kuvaa mavazi yale ya askari yaliyoletwa na Edwin.Alionekana kama askari halisi wa kikosi cha kutuliza ghasia kwa mavazi yale.Taratibu Khalid akaichukua fulana ile ambayo

ni bomu akamvisha akaifunga vizuri.

Khalid akazungumza na Abdi kwa lugha ya kiarabu halafu akawageukia akina Melanie

“Kila kitu tayari Abdi amekwisha pewa maelekezo nini cha kufanya hivyo msiwe na wasi wasi wowote.Kila kitu kitakwenda kama kilivyopangwa” akasema Khalid

Hakukuwa na kupoteza muda Edwin akaagana na akina Melanie kisha

akamchukua Abdi wakaelekea nje

Mlango mkubwa wa kuingilia sebuleni ukafunguliwa na Ruby akamstua Mathew

“Mlango umefunguliwa” akasema na mara akaonekana Edwin Mbeko na nyumayake akaonekana askari wa kikosi cha kutuliza ghasia.

“What’s going on in there?akauliza Mathew

“Sijaweza kuipata sura ya Yule askari kwani ametoka haraka haraka sana na kuingia garini”akasema Ruby

“Edwin alipozungumza na Melanie alimwambia anakwenda kufuatilia sare na alipotoka katika nyumba ya mmoja wa afisa wa polisi alikuwa na sanduku ambalo alikuja nalo hapa akaingia nalo ndani.Naamini sare alizokuwa anafuatilia ni sare za jeshi la polisi ambazo amevaa Yule jamaa na hii inatoa picha kwamba Yule jamaa yawezekana si askari.Yawezekana wamemvisha sare zile ili aonekane kama askari na wamtumie katika mipango

yao.Ningeweza kumfuatilia kujua wanakoelekea lakini kwa kuwa kuna kifaa katika gari la Edwin tutafahamu anaelekea wapi.Ndani ya nyumba hii kuna watu muhimu sana ambao hatupaswi kuwapoteza” akasema Mathew

Wakati Mathew na Ruby wakiendelea kufuatilia kile kinachoendelea ndani ya nyumba ya Melanie Jackson akapiga simu.

“Kuna taarifa gani Jackson?Mathew akauliza

“Uliniambia nifuatilie ni afisa gani anakaa katika ile nyumba alimoingia Edwin”

“Ndiyo.Umekwisha fahamu ni afisa gani?

“Anaitwa Inspekta Fanuel Mwabukusi au kwa jina lingine anaitwa afande mwarabu”

“Ahsante sana Jackson usiondoke maeneo hayo hadi nitakapokwambia” akasema Mathew

Katika nyumba ya Melanie bado milango iliendelea kufungwa.

“Ruby hatuwezi kuendelea kusubiri namna hii wakati

tayari tumekwisha pata uhakika kwamba ndani ya nyumba ile yupo James Kasai na Melanie Davis.We have to do something ! akasema Mathew

“Unataka kufanya nini Mathew?

“I want to get in there and…….”

“Hapana Mathew sikushauri ufanye hivyo.Kuna mambo mengi tutashindwa kuyafahamu kama tukiwavamia sasa hivi.Tujipe muda kidogo”akasema Ruby

“Ruby hujui ni namna gani ninaumia kuwaona wale watu walivyo huru wakiendelea na mipango yao mle ndani”

“Muda utafika Mathew.Vuta subira kidogo” akasema Ruby

“Kuna mtu mmoja tu ambaye bado hatuna uhakika naye mahala alipo Khalid Sultan.Kama ningekuwa na uhakika yuko mle ndani nisingekuwa na muda wa kusubiri” akasema Mathew

“Subira yavuta heri.Tuendelee kusubiri tunaweza kugundua mambo

mengine mengi zaidi” akasema Ruby na ile kamera ndogo ya nyuki ikaonyesha kuanza kuisha chaji ikalazimu Ruby kuirudisha

“Kamrea hii imetusaidia sana Mathew” akasema Ruby

“Teknolojia imerahisisha sana kazi za ujasusi siku hizi.Kama isingekuwa teknolojia ingetuchukua muda kufahamu kama James Kasai na Melanie wako mle ndani” akasema Mathew

****

Edwin Mbeko alipoondoka kwa Melanie alielekea moja kwa moja Mikunguni.Jackson akiwa katika kibanda cha kuuza juisi kilichotazamana na nyumba ya afande mwarabu aliiona gari ya Edwin ikikata kona kuelekea katika geti la nyumba ile.Akapiga honi na geti likafunguliwa gari likaingia ndani geti likafungwa.Jackson akasogea hadi katika geti akatafuta upenyo na kuchungulia ndani akamuona Edwin akiwa

amesimama na askari mmoja wa kikosi cha kutuliza ghasia pamoja na askari mwingine aliyevaa mavazi ya kiofisa akiwa na fimbo mkononi.Walizungumza kwa dakika kama tano halafu Edwin akaingia peke yake ndani ya gari yule askari akabaki.Geti likafunguliwa gari la Edwin likatoka na kuondoka.Simu ya Jackson ikaita alikuwa ni Edwin Mbeko

“Hallo mkuu” akasema Jackson

“Jackson umekwisha fika ofisini?akauliza Edwin

“Ninakaribia kufika mkuu”

“Fanya hivi.Nataka hapo hapo ulipofika ugeuze.Nataka nikukute katika bohari ili nikuachie gari langu nitakuwa na safari”

“Sawa mkuu ninaelekea huko sasa hivi” akasema Jackson halafu akampigia simu Mathew

“Jackson tumeona hapa Edwin amerejea tena mikunguni” akasema Mathew

“Ndiyo mkuu amerejea katika nyumba ile ile ya afande mwarabu”

“Alipoondoka hapa kwa Melanie alikuwa na mtu aliyevaa sare za jeshi la polisi”

“Nimemuona huyo mtu alikuwa amesimama naye wakizungumza na afande mwenye mavazi ya kiofisa ambaye naamini ni afande Mwarabu.Kwa sasa Edwin ameondoka lakini yuko peke yake garini Yule askari amemuacha hapa kwa Mwarabu.Amenipigia simu na kunitaka niende katika bohari ili anikute kule aniachie gari anadai anataka kusafiri” akasema Jackson

“Anataka kusafiri?!

“Ndiyo.Ameniambia hivyo” akajibu Jackson

“Jackson naomba unisubiri hapo mahala ulipo.Ninakuja sasa hivi nataka twende wote huko katika bohari” akasema Mathew

“Sawa mkuu nakusubiri” akajibu Jackson na Mathew akakata simu

“Mathew unataka kufanya nini?akauliza Ruby

“Sikiliza Ruby.Edwin anataka kusafiri.Ninahisi safari hii ni nje ya mkoa hivyo

lazima kuna kitu.I have to stop him.Ninakwenda huko katika bohari pamoja na Jackson na kumdhibiti Edwin asiweze kuondoka.Wewe utaendelea kukaa hapa hapa ukiendelea kufuatilia kwa karibu kila kinachoendelea na utanijulisha.Usiogope you'll be safe.Kama kutatokea hatari yoyote kuna silaha iko humu utatumia.Nikimaliza huko nitarejea hapa mara moja"akasema Mathew

"Sawa Mathew mimi nitaendelea kufuatilia kila kinachoendelea hapa na

kukujulisha” akasema Ruby.Mathew akashuka ndani ya gari na kuanza kutembea haraka haraka kuelekea barabara kuu kwa ajili ya kuchukua piki piki akamuelekeza Jackson sehemu ya kukutana.

****

Mathew alimchukua Jackson mahala alipomuelekeza wakutane kisha wakaelekea nyumbani kwake.

“Jackson karibu sana hapa ni nyumbani kwangu”

“Hapa ni kwako?akauliza Jackson

“Ndiyo.Mbona umeshangaa?

“Una nyumba nzuri mno.Unaonekana una maisha mazuri kwa nini unafanya kazi hizi za hatari?akauliza Jackson

“Tutazungumza hayo baadae lakini kwa sasa nataka kufahamu ulinzi ulivyo katika bohari”

“Kuna walinzi wanne getini.Wawili wana silaha mmoja ana mbwa na mmoja

kwa ajili ya mawasiliano.Kuna walinzi wengine sita wenye silaha kuzunguka ukuta wa bohari.Ndani huwa kuna wafanyakazi kumi na mbili.Kwa kawaida ni wafanyakzi wa bohari pekee ambao huruhusiwa kuingia.Wewe si mfanyakazi wa bohari hivyo hautaweza kuingia”akasema Jackson

“Nitaingia katika buti ya gari”

“Ikiwa hivyo utaweza kuingia mle ndani” akasema Jackson.

“Jackson kabla ya kuondoka hapa naomba nikuonye kwamba hiki tunachokwenda kukifanya huko ni kitu cha hatari sana hivyo endapo hauko tayari kwenda unaweza ukaniambia na mimi nitakuelewa” akasema Mathew

“Kaka mimi nimejitolea kwa ajili ya nchi yangu hivyo siogopi hata kama nikifa nitakuwa nimekufa nikilinda usalama wa taifa langu” akasema Jackson

“Good ! akasema Mathew kisha akaenda chumbani

kwake akaongeza silaha katika begi lake dogo akachagua gari ambalo lingeweza kuwafaa kwa shughuli ile akaingia katika buti na safari ikaanza

****

Edwin Mbeko alirejea kwa Melanie Davis baada ya kutoka Mikunguni

“Kila kitu kimekamilika na hivi tuongeavyo tayari Abdi anapelekwa uwanja wa ndege kutimiza jukumu lake”

“Huyo mtu anayempeleka Abdi uwanja wa ndege unamuamini?akauliza Melanie

“Ninamuamini .Ni mtu wangu wa karibu na licha ya hayo amechukua tayari milioni mia moja hivyo kila kitu kitakwenda vizuri.Msiwe na wasi wasi wowote kila kitu kimekaa vizuri” akasema Edwin

“Edwin umenifurahisha sana kwa namna unavyofanya kazi zako.Ahsante sana kwa kuukamilisha mpango huu” akasema James Kasai

“James Kasai hata mimi ninafurahi kukutana na kufanya nawe kazi” akasema Edwin

“Nilimwambia Melanie kwamba nitapenda kuja tena Dar es salaam kwa mapumziko ya hata wiki moja na amenihakikishia nisihofu.Ninakubaliana na Melanie kwamba nisihofu kuhusu kuja Tanzania kwani nina hakika wa kuja na kuondoka salama kwa sababu yako.Hongera sana Edwin” akasema James Kasai na

kumpa mkono Edwin kumpongeza

“Nashukuru sana James na ninakuahidi kwamba kwa muda wowote ambao utahitaji kuja nchini Tanzania unakaribishwa na ninakuhakikishia utakuwa salama” akasema Edwin

“Ndugu zangu ninawashukuru sana kwa ushirikiano wenu mkubwa.Tutaendelea kuwasiliana”akasema James Kasai huku akiwapa mikono Melanie na Khalid halafu akaagana na watumishi wawili

wa Melanie kisha wakatoka nje kuelekea garini.

Melanie na James wakakumbatiana wakaagana.James akafunguliwa mlango akaingia garini Edwin akaliondoa taratibu huku Melanie akipunga mkono kisha akarejea ndani.

****

Mathew Mulumbi akiwa ndani ya buti ya gari akielekea bohari kuu la SNSA simu yake ikaita alikuwa ni Ruby

“Hallo Ruby ! akasema Mathew

“Mathew uko wapi mbona unapatikana kwa mbali sana?

“Niko ndani ya buti ya gari ninaelekea bohari kuu SNSA.Vipi maendeleo huko?Kuna chochote umekipata?akauliza Mathew

“Edwin Mbeko ameondoka hapa muda mfupi uliopita akiwa na James Kasai.Inaonekana James Kasai anaondoka nchini”akasema Ruby

“Kama vile nilivyohisi.Thank you

Ruby.Watanikuta kule katika bohari”

“Mathew kuwa makini sana na hawa jamaa” akasema Ruby

“Usihofu Ruby.Endelea kufuatilia kila kinachoendelea hapo katika hiyo nyumba” akasema Mathew na kukata simu.

Taratibu Jackson alianza kupunguza mwendo wa gari alipokaribia kufika geti kuu la bohari ambako mmoja wa walinzi aliwasha taa yenye maandishi yanayomtaka asimame.Taratibu akapunguza

mwendo wa gari na kusimama walinzi wakaanza kulisogelea gari.Akiwa ndani ya buti ya gari Mathew alikuwa amejiweka tayari endapo kungetokea tatizo lolote.Jackson akashusha kioo cha gari na walinzi wakajikuta wakiangua kicheko baada ya kumuona.Hawakulikagua tena gari bali yakaanza maongezi mafupi

“Samahani mkuu hatukujua kama ni wewe.Unabadili magari sana siku hizi” akasema mmoja wa wale walinzi kisha geti

likafunguliwa Jackson akaingia ndani ya bohari.Moja kwa moja akaenda kuegesha gari katika maegesho ya magari.Kulikuwa na magari manne ya wafanyakazi lake likawa la tano.Akafungua mlango akashuka na kuangaza angaza kama kuna mlinzi karibu na eneo lile lakini hakuona mlinzi yeyote akaenda nyuma ya gari na kugonga buti mara mbili.Mathew Mulumbi taratibu akafungua buti na kuchungulia nje

“Kuko shwari kaka hakuna mlinzi yeyote mahala hapa” akasema Edwin huku macho yake yakigeuka kama kinyonga kutazama kila upande.Haraka haraka Mathew akatoka ndani ya buti ya gari na kuingia katika kiti cha nyuma.

“Eneo liko kimya sana hili” akasema Mathew

“Ile pale ni karakana ya kutengenezea magari mabovu ya idara ingawa kwa sasa haitumiki tena kwani magari yote hupelekwa katika gereji binafsi.Lile pale ndilo jengo la bohari.Ndani mle kuna vitu

mbalimbali vya idara” Jackson akamuelekeza Mathew

“Silaha pia mnahifadhi mle?

“Hapana silaha hazihifadhiwi hapa.Hifadhi ya silaha iko kule wanakoishi kikosi cha makomando wa SNSA” akajibu Jackson na mara ukasikika mlio wa helkopta

“Hiyo ndiyo helkopta ya idara ambayo ataondoka nayo Edwin” akasema Jackson na wote wakaishuhudia helkopta ile ikitua katika sehemu yake maalum.

“Sogeza gari karibu” akasema Mathew na Jackson akawasha gari akalisogeza taratibu karibu na helkopta kama alivyoelekezwa na Mathew.Injini ya helkopta ikazimwa

“Nataka ukamtoe Rubani ndani ya helkopta umpeleke ndani ya jengo.Can you do that?akauliza Mathew na Jackson akashuka garini akafungua mlango mkubwa wa helkopta.

“Desmond ! akasema Jackson akisalimiana na Yule rubani

“Jack mambo vipi.Naona umewahi sana”

“Nimefika hapa dakika chache zilizopita.Safari ya wapi?

“Tunaelekea Kagera” akajibu Yule rubani

“Safari ndefu sana.Twende ndani tukapate vitafunwa kabla bosi hajafika.Yuko mbali hataweza kufika sasa hivi” akasema Jackson

“Wazo zuri Jack.Ninahitaji pia kujisaidia” akasema Yule rubani na kushuka ndani ya helkopta

“Gari zuri sana hili”akasema Desmond baada ya kuliona gari lile alilokuwa anaendesha Jackson

“Usafiri wangu mpya huu.Twende ndani utakuja kulijaribu ukirejea kutoka Kagera.Nitakuachia wiki nzima ulitumie” akasema Jackson na kumuondoa Desmond aliyekuwa ameshika kitasa cha mlango akitaka kufungua kuangalia gari lile kwa ndani.

Mara tu walipoondoka Mathew Mulumbi akashuka kutoka ndani ya gari

akaufungua mlango wa helkopta akaingia ndani akafungua begi lake akatoa bomu na kulitega ndani ya helkopta halafu akatoka na kuingia ndani ya gari.Kilikuwa ni kitendo cha haraka sana.

Kwa mbali aliwaona Jackson na Desmond wakirejea.Desmond akafungua mlango wa mbele akaenda kuketi katika kiti chake akiwa ameshika mfuko uliokuwa na vitafunwa mbalimbali walivyovitoa ndani.Jackson akaliondoa gari na kulirejesha sehemu ya maegesho

Zilipita dakika thelathini na nane gari la Edwin Mbeko likawasili kwa kasi na kwenda kusimama mbali kidogo na helkopta.

“Edwin tayari amewasili.Nini kinaendelea?akauliza Jackson.

“Subiri kwanza washuke garini” akasema Mathew.

Rubani wa helkopta akashuka na kwenda katika gari la Edwin akafungua mlango Edwin akashuka.Akazunguka upande wa pili akafungua mlango akashuka James Kasai

wakaanza kutembea kuelekea ilipo helkopta.

“It’s show time” akasema Mathew na kukibonyeza kidude alichokuwa amekishika mkononi na mara ukatokea mlipuko mkubwa helkopta ikalipuka.Edwin,James Kasai na Desmond wote wakaanguka chini.Kama mshale Mathew na Jackson wakachomoka kutoka katika lile gari kuwafuata akina Edwin.James Kasai ndiye aliyekuwa wa kwanza kuinuka kutoka mahala pale walipoangukia akamfuata Edwin Mbeko aliyekuwa

ameanguka na kumsaidia kuinuka.Mara Edwin akachomoa bastora baada ya kuiona sura ya Mathew Mulumbi akikimbia kuelekea mahala walipo

“Run ! Edwin akamwambia James Kasai kisha akaanza kuachia risasi kuelekea upande wa Mathew mara kiganja cha mkono wake kikapigwa risasi bastora ikaanguka.

“Aaaaggghhh ! Edwin akatoa mguno na mara akapigwa tena risasi nyingine ya paja.James Kasai aliinuka

na kuanza kukimbia huku akigeuka nyuma na kuachia risasi lakini Mathew aliendelea kumkimbiza.

“Leo ni mimi au wewe shetani wewe ! akasema Mathew na kuongeza mbio kumfukuza James aliyekuwa anaelekea yalipo magari mabovu.James aligeuka akaachia risasi Mathew akajibanza katika mnazi James alipogeuka ili aendelee kukimbia Mathew akaachia risasi mfululizo na James akaanguka chini.Alipigwa risasi kiunoni.Licha ya

kupigwa risasi bado James aligeuka na kuanza kuachia risasi hovyo na moja ya risasi ikamchubua Mathew shingoni akajibanza nyuma ya mti uliokuwa karibu.

“Shetani Yule angeweza kuniua ! akawaza Mathew huku akiendelea kusikia mivumo ya risasi kutoka kwa James Kasai.

“Siwezi kumuacha huyu muuaji akatoroka” akawaza Mathew na kugeuka haraka akaanza kuachia risasi mfululizo.James Kasai aliyekuwa anajivuta kuelekea

katika mojawapo ya gari akapigwa risasi nyingine katika mguu wa kushoto na katika bega la kushoto akalala sakafuni.Huku akigugumia kwa maumivu James akageuka akiwa ameishika bastora yake akamuona Mathew akimfuata akaizinga bastora ili kuachia risasi lakini bastora yake haikuwa na kitu.Risasi zilikwisha malizika.

“Aaaaghh ! akasema Mathew kwa hasira huku akimimina risasi katika bunduki yake na kifua cha James hakikutazamika

tena.Bunduki ile ya Mathew ilikwisha risasi akaitupa akachukua bastora akamtazama kwa hasira James ambaye tayari alikwisha fariki.

“Edwin weka bastora yako chini.It’s over ! sauti kali ikamuamuru Edwin aliyekuwa anagugumia kwa maumivu ya kupigwa risasi.Edwin alipatwa na mstuko mkubwa akabaki anashangaa asiamini macho yake alipomuona Jackson akiwa na bastora inayofuka moshi.

“Jack ?!! akasema Edwin kwa mshangao

“It’s over Edwin ! akasema Jackson ambaye alifanya kosa kubwa kugeuka kutazama walinzi waliokuwa wakikimbia kuelekea eneo lile.Edwin akaitumia nafasi ile akaiokota bastora yake kwa mkono wa kushoto akamlenga Jackson na kuachia risasi zilizompata Jack akaanguka chini.

Walinzi waliokuwa na vizimia moto walifika na kuanza kuuzima moto ule.

“Kuna jambazi amekimbilia kule karakana.Hakikisheni mnampata ! akaelekeza Edwin

kisha Desmond akamtaka mmoja wa walinzi amsaidie wakamnyanyua Edwin kumpeleka katika bohari.

Baadhi ya walinzi waliokuwa na silaha wakaanza kuelekea eneo lile la karakana kulikokuwa na magari mabovu kwa ajili ya kumsaka jambazi waliyeelekezwa na Edwin.

“Hatimaye nimefanikisha kile nilichokuja kukifanya.Nilikuja Tanzania kukuua na nimefanikiwa kukuua ! akasema Mathew huku akimtazama James Kasai aliyekuwa amechafuliwa kwa

risasi.Mara akasikia sauti ya mbwa akibweka.

“Wananitafuta ! akawaza kisha akazama ndani ya uvungu wa gari na kutokea upande wa pili akajibanza katika moja wapo ya gari.Walinzi wale walioongozwa na mbwa mkubwa wakaukuta mwili wa James Kasai.Mmoja wa walinzi akachukua redio ya mawasiliano na kuibonyeza akawataarifu wenzake

“Jambazi mmoja ameuawa huku katika karakana ya magari” akasema Yule jamaa

akidhani James Kasai ndiye jambazi waliyetumwa wamtafute.Ghafla Mathew Mulumbi akajitokeza akiwa na bastora mbili na kuanza kunyesha mvua ya risasi walinzi wale wakaanguka chini wote.Mbwa Yule mkubwa akatoka mbio na kutaka kumrukia lakini Mathew alikwisha muona na kumpa konde zito la mkono wa kuliwa mbwa akaanguka chini hakuinuka tena

“Zamu ya Edwin Mbeko” akasema Mathew na kutoka eneo lile la karakana akawaona

baadhi ya walinzi na wafanyakazi wakiendelea na zoezi la kuzima moto.

“Lazima nimpate Edwin” akawaza Mathew kisha akachukua bomu la kurusha kwa mkono akang’oa kifuniko na kulirusha mbali kidogo na ule moto uliokuwa unawaka likalipuka na kuzua taharuki kubwa watu wakaacha kuzima moto wakaanza kukimbia kunusuru maisha yao.Mathew akaitumia fursa ile akatoka mbio kuelekea mahala moto ulipokuwa unawaka akastuka

baada ya kumuona Jackson akiwa amelala chini

“Oh no ! akasema Mathew kwa mstuko na kumfuata Jackson akamtingisha

“Jack ! Jack ! akaita Mathew na Jack akafumbua macho

“Edwin alinipiga risasi akadhani ameniua nami nikalazimika kujifanya nimekufa.Ahsante kwa hii fulana ya kuzuia risasi imeokoa maisha yangu” akasema Jackson

“Yuko wapi Edwin?

“Ameingia ndani ya jengo” akasema Jackson Mathew akamshika mkono akamnyanyua

“James Kasai tayari nimemuua.Tunamfuata Edwin” akasema Mathew wakaanza kukimbia kuelekea katika jengo la bohari alikoenda Edwin

Desmond alikwenda katika stoo ya vifaa vya afya akachukua bandeji na kumfunga Edwin jeraha lake la risasi katika kiganga cha mkono ili kuzuia damu kuendelea kuvuja.

“Desmond I need to get out of here before that nataka uende ukamtafute Yule jamaa niliyekuwa naye garini.Chukua walinzi muelekee katika karakana ndiko alikoelekea.Hakikisha unampata” akasema Edwin na kumpa Jackson bastora

“Mkuu kwa nini nisichukue gari nikakuondoa kwanza wewe haraka ili ukapate matibabu?Eneo hili limekwisha kuwa hatarishi na yawezekana wale jamaa wakaja na kukukuta humu

wakakumaliza” akasema Desmond

“Desmond siwezi kuondoka hapa bila Yule mtu niliyekuja naye ! Go find him ! akasema Edwin.Desmond na Yule mlinzi walitoka Edwin akachukua simu yake akampigia Melanie

“Edwin ! akasema Melanie

“Melanie tumevamiwa ! akasema Edwin

“Mmevamiwa?! Melanie akastuka

“Ndiyo.Tumevamiwa na watu siwafahamu.Helkopta yetu imelipuliwa na bomu”

“Mungu wangu.Are you okay?akauliza Melanie kwa sauti iliyojaa wasi wasi

“Nimepigwa risasi lakini James amekimbia nimetuma watu wakamtafute”

“Edwin get out of there now !

“Melanie siwezi kuondoka nikamuacha James Kasai.Lazima nimpate ndipo tuondoke hapa.Melanie sikiliza kama kuna kitu chochote kitanitokea basi usihofu kila kitu kitakwenda kama kilivyopangwa.Tayari Yule kijana wetu aliyebeba bomu

yuko uwanjani akiwasubiri marais wafike” akasema Edwin

“Edwin tafadhali jitahidi uweze kuondoka hapo mara moja” akasema Melanie

“Nitaondoka Melanie.Nimewatuma watu wakamchukue James kisha tutaondoka.Nitakujulisha kinachoendelea” akasema Edwin na kukata simu

“Taratibu wekeni silaha zenu chini na kisha muinue mikono” Sauti kali ikawaamuru Desmond na Yule jamaa aliyekuwa naye mara tu walipojitokeza katika mlango

wa kuingilia katika bohari.Taratibu wakaweka silaha chini.

“Yuko wapi Edwin Mbeko?akauliza Mathew .Desmond akamtazama Jackson kwa hasira

“Sikujua kama u msaliti kiasi hiki Yuda wewe ! akasema kwa ukali

“Shut up ! akafoka Mathew

“Yuko wapi Edwin?akauliza Mathew

“Hatufahamu alip……” Kabla Desmonda hajamaliza sentensi yake tayari Mathew aliizinga bastora na kumchapa

risasi Desmond akabaki Yule mlinzi

“Yuko wapi Edwin?akauliza Mathew

“Yuko ndani ! akajibu Yule mlinzi kwa woga na Mathew akamtaka ampeleke mahala alipo Edwin Mbeko.

“Desmond ! akaita Edwin Mbeko aliposikia hatua za watu wakielekea mahala alipo

“Desmond is that you? Akauliza tena Edwin na Mathew akampiga Yule mlinzi pigo moja kichwani akaanguka chini akaanza kunyata akifuata sauti ile

ilikotokea.Akausukuma mlango wa moja wapo ya chumba na Edwin Mbeko akakutwa akiwa amekaa chini.Wakatazamana kwa sekunde kadhaa.

“Ni wewe uliyeshirikiana na Annabel kumuua Fidelis na mmeshirikiana tena kuvamia bohari yetu na kufanya uharibifu mkubwa.Umekosea sana kwa hiki ulichokifanya”akasema Edwin Mbeko

“Naamini umeniona lakini hunifahamu .Naitwa Mathew Mulumbi”

“Mathew Mulumbi?! Edwin akashangaa

“Wewe ndiye uliyevamia ofisi zetu !

“Ni mimi niliyevamia ofisi zenu na nilikuja kukutafuta wewe ! Sikukupata siku ile lakini leo nimekupata.Edwin nafahamu yote unayoyafanya.Nafahamu umekuwa unashirikiana na Melanie Davis.Ninafahamu kila kitu unachokifanya kushirikiana na magaidi na sitaki kuyasema hapa.Kwa taarifa yako James Kasai amekwisha fariki

dunia.Nimemuua kwa mkono wangu.Fahamu vile vile kwamba hivi tunavyoongea kuna watu wako nje ya nyumba ya Melanie Davis na muda wowote atatiwa nguvuni na mtandao wenu wote utasambaratika.Naweza kukusaidia Edwin na kukuacha hai lakini ni pale utakapoamua kunieleza ukweli”

“Unajidanganya wewe marehemu.Hakuna chochote utakachoweza kukipata.Wewe na hao waliokutuma mmejidanganya” akasema

Edwin.Simu ya Mathew ikaita alikuwa ni Ruby

“Mathew nimemuona Khalid.Yuko ndani ya nyumba hii” akasema Ruby

“Ruby are you sure?

“Ndiyo Mathew.Nimemuona.Ametoka muda si mrefu nje.Yuko na Melanie wamekaa katika sehemu ya kupumzikia bustanini wakijadiliana jambo”

“Ahsante Ruby.Nitafika hapo muda si mrefu” akasema Mathew na kukata simu

“Tayari tunafahamu mahala alipo Khalid Sultan

Khalid na muda si mrefu kutoka sasa naye atauawa.Nitakuacha hai kama utanieleza ni kitu gani mmepanga kukifanya hapa Dar es salaam leo?akauliza Mathew

“Go to hell ! akasema Edwin

“Mara ya mwisho Edwin nakuuliza nini mmepanga kukifanya leo hii?Nijibu na ninakuahidi sintakuua”

“Unadhani ninaogopa kufa? Najua nitakufa lakini mmeshachelewa sana.Hakuna chochote mtakachoweza

kukifanya kwa sasa.Hadi jioni ya leo tayari mtakuwa mmepata salamu” akasema Edwin

“Mara ya mwisho Edwin nakuuliza nini mmepanga kukifanya leo?Wapi mmepanga kushambulia?akauliza Mathew na Edwin akacheka

“Wewe na wapumbavu wenzako nimewaambia tayari mmechelewa sana.Subirini mtapata majibu! Akasema Edwin Mathew akapandwa hasira akaanza kummiminia Edwin risasi na kumuua

akaichukua simu yake haikuwa na laini.Pembeni yake kulionekana vipande vya laini ya simu iliyoharibiwa

“Bazazi huyu ameharibu laini yake ya simu ! akasema Mathew.

“Jackson tuondoke haraka eneo hili” akasema Mathew wakatoka kwa haraka.Hakukuwa tena na watu eneo lilikuwa tupu watu wote walikimbia kuokoa maisha yao.Jackson aliingia katika gari lao Mathew akamuelekeza kulisogeza katika karakana wakasaidiana kuubeba mwili wa James Kasai wakauweka katika buti ya gari

kisha wakaondoka.Katika geti kuu la kuingilia bohari waliwakuta baadhi ya walinzi na wafanyakazi wakiwa wamekusanyika Mathew akatoa bomu la kutupa kwa mkono akang'oa kifuniko na kulirusha likalipuka na watu wote wakalala chini halafu wakainuka na kuanza kukimbia.Mathew akashuka akafungua geti wakaondoka.

"Kilichotokea pale ndani ni kama filamu lakini ni kitu cha kweli.Huyu jamaa ni mtu hatari sana.Sikujua kama ana uwezo mkubwa namna hii wa kupambana.Sikutegemea kama tungeweza kutoka

hai.Nashukuru alinipa fulana ya kuzuia risasi kwani bila ile hivi sasa ningekuwa marehemu” akawaza Jackson

****

Melanie alichanganyikiwa baada ya kupigiwa simu na Edwin akamjulisha kwamba wamevamiwa na watu wasiojulikana.Mara tu Edwin alipokata simu Melanie akamfuata Khalid chumbani kwake akamtaka watoke nje wakazungumze wakaenda kuketi nje bustanini

“Melanie kuna nini?Mbona unaonekana una

wasiwasi mwingi?akauliza Khalid

“Kuna jambo limetokea Khalid”

“Jambo gani Melanie?akauliza Khalid

“Nimepigiwa simu na Edwin ameniambia wamevamiwa na watu wasiojulikana”

“Wamevamiwa?

“Ndiyo”

“Imekuaje wakavamiwa? Ni tukio la ujambazi? akauliza Khalid

“Hajanieleza vizuri kwa undani”

“Wako salama yeye na James Kasai?akauliza Khalid

“Helkopta yao imelipuliwa,Edwin amepigwa risasi na James amekimbia.Nimechanganyikiwa Khalid sina hakika kama watatoka salama”

“Melanie tunatakiwa kutafuta namna ya kuwasaidia wenzetu kabla mambo hayajawa mabaya.Kwanza kama James Kasai amekimbia ni mbaya zaidi kwani anafahamika,picha zake ziko kila mahali hawezi kufika mbali atajulikana.Edwin naye amepigwa risasi na Yule ndiye pekee tuliyekuwa tunamtegemea aweze kumuondoa James Kasai hapa

nchini.Kama helkopta imelipuliwa basi utakuwa ni mlipuko mkubwa na lazima litakuwa ni bomu hivyo basi watu wa karibuna eneo hilo watakuwa wameusikia mlipuko huo na kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama.Polisi wakifika hapo wanaweza wakampata James Kasai na kila kitu kikaharibika.Tunatakiwa kuwaondoa haraka sana eneo la tukio Edwin na James Kasai kabla polisi hawajafika" akasema Khalid

"Hilo unalosema ni la kweli Khalid lakini namna gani tutaweza kuwaondoa James

Kasai na Edwin mahala hapo?Mimi sina kikosi na mtu pekee niliyekuwa namtegemea ni Edwin ambaye naye amepigwa risasi”akasema Melanie

“Usihofu.Sisi tunao vijana wetu hapa Dar es salaam.Ninaomba simu yako nataka kuwasiliana na mtu Fulani ili anipatie vijana wa kwenda kuwakomboa James na Edwin” akasema Khalid na Melanie akampa simu yake.Khalid akaenda ndani na baada ya muda akarejea akiwa na kitabu kidogo akakifungua akaipata namba ya simu ya mtu aliyetaka kumpigia

akapiga.Akazungumza kiarabu na mtu Yule kwa takribani dakika tano halafu akampa simu Melanie akamtaka amuelekeze Yule mtu pale mahala walipo Melanie akamuelekeza Yule mtu kisha akampatia simu Khalid ambaye aliendelea kuzungumza tena na Yule jamaa halafu akakata simu

“Huyu niliyezungumza naye ni mkuu wa kundi la IS hapa nchini na ukanda wote wa Afrka Mashariki anaitwa Sayid Al Noor.Nilitakiwa kuonana naye jioni ya leo baada ya shambulio kutokea lakini kwa hili lililojitokeza

nimelazimika kumuomba msaada na vijana watakuja hapa muda si mrefu ili kupata maelekezo ya mahala walipo Edwin na James Kasai.Kitu cha msingi kabla vijana hao hawajafika tunatakiwa kufahamu mahala walipo akina Edwin” akasema Khalid

“Sifahamu mahala walipo.Alisema wanakwenda katika bohari kuu na sifahamu bohari hilo liko wapi.Ngoja nimpigie simu nimuombe anielekeze” akasema Melanie na kupiga namba za simu za Edwin lakini simu yake haikupatikana.Akajaribu tena

lakini bado simu haikupatikana.

“Simu yake haipatikani tena.Nitawasiliana na nani anisaidie?Simfahamu mtu mwingine yeyote wa idara yake” akawaza Melanie na mara akapata wazo

“Devotha ! Ngoja nimtafute” akawaza na kuzitafuta namba za simu za Devotha akampigia lakini simu ya Devotha haikuwa ikipatikana.

“Mungu wangu nini hiki kinaendelea? Mbona kila ninayempigia kumuomba msaada hakuna anayepatikana?Devotha naye

yuko wapi?Kwa nini hapatikani kuanzia jana?Joyce naye hayupo najuta kwa nini nilimkubalia aondoke asubuhi ya leo kwenda Kigoma.Ngoja nimjaribu pengine anaweza kuwa na msaada” akawaza Melanie akampigia simu Joyce dereva wake lakini naye simu yake haikupatikana

“Aliyesema siku ya kufa nyani miti huteleza hakukosea.Timu ya kwenda kuwaokoa akina Edwin inakuja na sijui mahala Edwin alipo.Nimepata wazo ngoja nimjaribu Peniela yawezekana akawa amepata taarifa za alipo Devotha.Yule ndiye msuka

mipango yote kwa nini ametoweka ghafla wakati kama huu?Hakupaswa kuondoka bila kutujulisha kwani yeye ndiye tunayemtegemea sana kwa kila kitu” akawaza Melanie na kumpigia Peniela simu ikaita akashusha pumzi

“Afadhali huyu simu yake inaita” akawaza Melanie na mara simu ikapokelewa

“Hallo Melanie” akasema Peniela

“Peniela samahani kwa usumbufu”

“Bila samahani Melanie.Nikusaidie nini?

“Nataka kujua kama ulifanikiwa kumpata Devotha”

“Hapana sikufanikiwa kumpata”

“Mungu wangu ! akasema Melanie

“Kwani vipi Melanie?Una shida naye sana?

“Ndiyo Peniela nina shida naye kubwa sana” akasema Melanie

“Sikiliza Melanie kama Devotha hayupo hata mimi ninaweza kukusaidia.Kama kuna kitu kimekwama niambie nina mtandao mkubwa tu hapo Tanzania na mashariki kwa ujumla” akasema Peniela

“Kuna rafiki yangu amevamiwa na majambazi.Amenipigia simu muda si mrefu akaniambia kwamba amevamiwa na amepigwa risasi.Ninataka kufahamu mahala alipo ili nitume watu wakamsaidie.Devotha anafahamiana na watu wa mitandao ya simu ambao wanaweza wakafahamu huyo rafiki yangu alikuwa wapi aliponipigia simu. Hilo ndilo kubwa ninalolihitaji”

“Usiwe na wasiwasi Melanie.Hata kama Devotha hayupo nitakusaidia.Ninao mtandao mkubwa tu hapo

Tanzania.Nielekeze mahala ulipo kuna mtu ambaye ni mtaalamu wa hayo mambo ya mtandao.Nitamuelekeza afike kwako haraka sana akusaidie” akasema Peniela na Melanie akamuelekeza mahala alipo

“Usihofu Melanie.Ninamuelekeza huyo mtu wangu anakuja hapo sasa hivi atakusaidia kujua mahala alipo mtu wako” akasema Melanie

“Nashukuru sana Peniela”

“Usijali Melanie.Muda wowote ukiwa na tatizo nijulishe nitakusaidia”

akasema Peniela na kukata simu

“Umejileta wewe mwenyewe katika mdomo wa Mamba na mimi kazi yangu ni kukutafuna.Pole sana Melanie kwani mbio zako zimefika ukingoni” akasema Peniela na kumpigia simu Mathew

“Peniela ! akasema Mathew

“Mathew nimepigiwa simu na Melanie muda mfupi uliopita anamtafuta Devotha nikamuomba anieleze shida yake nimsaidie akaniambia kwamba anamtafuta rafiki yake ambaye ametekwa na watu wasiojulikana na anataka

atume watu wakamsaidie lakini hafahamu mahala huyo rafiki yake alipo.Anachohitaji ni mtu wa kumsaidia kujua rafiki yake alipiga simu akiwa wapi? Nimemwambia kwamba ninamtumia mtu ambaye ana uwezo huo wa kumsaidia na kujua mahala alipo huyo rafiki yake.Mathew hii nafasi imepatikana ya kummaliza Melanie.Utakwenda nyumbani kwake na utajifanya wewe ndiye huyo mtu ambaye unataka kumsaidia kujua mahala alipo rafiki yake”akasema Peniela

“Peniela sijui nikushukuruje kwa msaada

huu mkubwa ulionisaidia.Sikutegemea kab…."

"Mathew tusipoteze muda.Melanie anakusubiri sasa hivi.Ukifika mwambie umetumwa na Peniela" akasema Peniela

"Ahsante Peniela" akasema Mathew na kukata simu na kumpigia simu Ruby

"Ruby nimepigiwa simu na Peniela muda si mrefu ameniambia kwamba Melanie amempigia simu akamuomba amsaidie kupata mtu ambaye atamsaidia kujua rafiki yake aliyetekwa yuko wapi ili atume watu wakamsaidie.Nadhani

Edwin Mbeko alimpigia simu akamjulisha kilichotokea. Peniela amemwambia kwamba anamtuma mtu nyumbani kwake muda si mrefu ili aweze kumsaidia”

“Mathew this is our chance to finish Khalid Sultan” akasema Ruby

“Ondoka hapo ili tukutane tuweze kujipanga namna ya kuingia mle ndani” akasema Mathew na kumueleza Ruby sehemu ya kukutana.” akasema Mathew na kukata simu akamuelekeza Jackson aongeze mwendo wa gari.

****

Mazungumzo kati ya marais watatu yalimalizika ikulu Dar es salaam na marais wale ambao kwa siku chache zilizopita hawakuwa wakitazamana usoni kufuatia shambulio lililofanywa na James Kasai nchini Tanzani ambaye anatajwa kufadhiliwa na serikali ya Uganda.Katika kikao hicho ambacho mazungumzo yake yalikuwa ya kirafiki sana Jenerali Akiki Rwamirama Rais wa Uganda aliahidi kutoa ushirikiano katika zoezi la kumsaka James Kasai.

Kikao kilimalizika kwa mafanikio makubwa sana na marais wote wakashikana mikono kupongezana kwa mafanikio yale makubwa

“Tulichokifanya leo ni kitu cha kihistoria na kitaingia katika vitabu vya historia.Tumeonyesha mfano kwa mataifa mengine kwamba tunaweza kuzungumza na kumaliza tofauti zetu sisi wenyewe.Tumewaabisha wale waliodhani labda Afrika Mashariki itasambaratika .Ahsante sana Jenerali Akiki kwa kujisusha kwa ajili ya maslahi ya Afrika Mashariki” akasema Dr Fabian

Jenerali Akiki ndiye aliyekuwa wa kwanza kuondoka kurejea Uganda na kuwaacha Rais Patrice Eyenga na Dr Fabian ambao walikuwa na mazungumzo mengine ya faragha.Waziri wa mambo ya nje wa nchi ndiye aliyemsindikiza Rais Akiki uwanja wa ndege wa Julius Nyerere.

****

Mathew akiwa na Ruby ndani ya gari waliwasili nyumbani kwa Melanie.Mathew aliyekuwa katika usukani akapiga honi

mara tatu halafu geti likafunguka

“Are you ready Ruby?akauliza Mathew

“I’m ready” akajibu Ruby kisha gari likaingia ndani taratibu geti likajifunga.Mathew akapeleka gari hadi katika baraza.Mwanamke mmoja akaenda katika kioo cha dirisha akagonga.Ruby akafungua mlango akashuka .Yule mwanamke akampekua kama ana silaha

“Huyu nani ndani ya gari?akauliza Yule mwanamke

“Huyu ni dereva wangu” akasema Ruby na Yule

mwanamke akamtaka Mathew atoe gari pale karibu na mlango mkuu wa kuingilia sebuleni.

“Hakuna haja.Ninachukua muda mfupi sana hapa kisha naondoka” akasema Ruby akionekana kuwa na haraka.Yule mwanadada akamuongoza Ruby kuingia sebuleni akakutana na Melanie

“Karibu sana dada” akasema Melanie

“Melanie Davis?akauliza Ruby

“Ndiyo.Umetumwa na Peniela?

“Ndiyo nimetumwa na Peniela”akasema Ruby

“Karibu sana”

“Ahsante.Wapi tunafanyia kazi yetu?akauliza Ruby

“Hapa hapa sebuleni hakuna tatizo” akajibu Melanie na Ruby akaitoa kompyuta katika mkoba akaanza kazi yake.Ruby alicheza na kompyuta haraka haraka kama vile ana vidole sita kila mkono na hakuna aliyejua kitu alichokuwa anakifanya.Kitu cha kwanza alichokifanya ni kuunganisha kamera ya siri katika kompyuta yake na kompyuta ndogo iliyokuwamo ndani ya gari ili kumuwezesha Mathew kuona kile kinachoendelea mle

ndani.Alipokamilisha hilo akaomba namba za simu za mtu ambaye anamtafuta kisha akaziingiza katika program yake na kuanza kutafuta mahala alipo Yule mtu.

Kupitia ile kompyuta ndogo aliyounganishwa na Ruby,Mathew aliweza kuona namna watu walivyokaa mle ndani.Ruby alikuwa mezani halafu kukawa na wanawake wawili wakiwa nyuma ya Melanie.Mathew akaziweka sawa bastora zake halafu akafungua mlango taratibu na kwa tahadhari akashuka akatembea kuelekea katika mlango mkubwa wa

sebuleni.Akakishika kitasa cha mlango akakinyonga na kufungua mlango kisha kama kima akajitoma ndani.

Kabla hajafanya chochote mmoja wa wale wanawake akamsukuma Melanie akaanguka chini kisha mwingine akachomoa bastora na kuanza kumimina risasi kuelekea kule alikokuwa Mathew ambaye aliruka na kujificha nyuma ya kabati kubwa la vitabu.Yule mwanamke mwingine aliyemuangusha chini Melanie akamuinua na kumuongoza kukimbia pale sebuleni huku Yule mwanamke mwingine

akiendelea kuachia risasi kumzuia Mathew asiweze kujitokeza.Risasi zilimalizika katika bastora ya kwanza na kwa haraka akachukua bastora ya pili na Mathew akautumia mwanya huo akajitokeza na kuanza kuachia risasi.Yule mwanamke akainua stuli akairusha Mathew akayumba kuikwepa na Yule mwanamke akapata upenyo akainuka na kuanza kukimbia kufuata varanda ambalo Melanie na Yule mwanamke mwingine walipita.Macho ya Mathew yalikwisha mng’aza akarukia katika sofa kisha akarukia juu ya meza na kuanza

kuvurumisha risasi Yule mwanadada akaingia katika mojawapo ya chumba Mathew akanyata taratibu hadi katika mlango wa chumba kile akaupiga teke ukafunguka akaingia ndani na kwa kasi ya ajabu mkono wake uliokuwa na bastora ukapigwa teke bastora ikaanguka chini akapigwa teke lingine la mbavu akaanguka chini na Yule mwanadada akamuelekezea bastora.Mara ghafla akatoa mguno na kuanguka.Ruby alisimama mlangoni akiwa na bastora aliyokuwa ameificha katika

sanduku dogo aliloingia nalo mle ndani

“Thank you Ruby uko salama?akauliza Mathew

“Niko salama Mathew.” akaelekeza Ruby

“Ruby unatakiwa uende nje niachie mimi nipambane na hawa watu humu ndani.Mpigie simuJackson aje ndani” akasema Mathew

“Mathew siwezi kukuacha peke yako humu ndani” akasema Ruby

“Ruby nisikilize.Hii sehemu ya hatari nenda nje ! akafoka Mathew na Ruby hakutaka kubishana na Mathew akachukua kompyuta

yake akatoka kwa tahadhari hadi katika gari akaliwasha na kutoka hadi getini akashuka akajaribu kulifungua geti halikufunguka akatoa bastora na kumimina risasi sehemu ambayo inapokea taarifa kutoka kompyuta iliyo ndani akakisambaratisha kiboksi kile halafu akafungua geti na kutoka nje.

Baada ya Ruby kutoka Mathew akaanza kufuata lile varanda kwa tahadhari akiingia katika chumba kimoja kimoja na mara akapigiwa simu na Ruby

“Kuna gari mbili zimefika katika geti.Geti halitaweza

kufunguka kwa kompyuta kwani nimeliharibu” akasema Ruby

Gari zile mbili zikaanza kupiga honi ili geti lifunguliwe.Mathew akasikia mlio wa simu sebuleni akaufuata mlio ule na kuiokota simu iliyokuwa ikiita na mara ujumbe ukaingia akausoma.

“*Vijana tayari wamefika mahala mlipoelekeza.Wapokeeni na muwaelekeze mahala alipo huyo mtu wakamfuatilie haraka*” ukasomeka ule ujumbe. Mathew akatoka mle ndani na kutembea kwa tahadhari kubwa kuelekea

getini alipolikaribia akatoa mabomu mawili ya kutupa kwa mkono akang'oa vifuniko na kuyarusha nje ya geti yaliko magari ya wale jamaa na milipuko kutokea.

Baada ya kuokolewa sebuleni Melanie Davis na Yule msaidizi wake walikimbilia ghorofa ya pili kilipo chumba cha Melanie

"Mfuate Khalid haraka chumbani kwake mwambie tumevamiwa ! akaelekeza Melanie na kuingia chumbani kwake.Akajipekua kutafuta simu yake lakini hakuwa nayo

“Mungu wangu nimeangusha simu ! akasema Melanie kwa mstuko.

“Kitu gani Peniela amenifanyia? Hawa watu aliowatuma ni akina nani?akajiuliza Melanie na kuhisi kuchanganyikiwa.Akafungua dirisha akachungulia nje kama anaweza akaruka akaogopa na kulifunga.Akatazama saa yake na kuvuta pumzi ndefu

“It’s over ! hawa watu wanaonekana tayari wamekwisha tufahamu.Naamini ndio hawa hawa waliomvamia Edwin na sasa wamekuja kwangu.It’s

over” akawaza kisha haraka haraka akaenda mezani akaikunjua kompyuta yake akaanza kujirekodi.

Kupitia kamera zilizo nje ya chumba chake Melanie alimuona Khalid akielekea katika mlango wa chumba chake akiwa ameongozana na Yule mwanamke aliyetumwa kwenda kumjulisha kwamba wamevamiwa.Haraka haraka Melanie akabonyeza sehemu Fulani na mlango wake ukajifunga.Khalid alianza kugonga mlango kisha kwa hasira akampiga risasi Yule mwanamke akaanguka chini.Akaendelea kugonga

mlango kwa nguvu akimtaka Melanie afungue na alipoona hafungui akaanza kumimina risasi katika mlango lakini mlango ule haukuwa ukipenya risasi

Baada ya kurusha yale mabomu nje ya geti,Mathew akakimbia kuelekea ndani na alipofika mlangoni akasikia mlio wa risasi ukitokea ndani ya ile nyumba.Akaanza kutembea kwa tahadhari akifuata ngazi kuelekea ghorofa ya kwanza akasikia tena milio ya risasi mfululizo katika ghorofa ya juu yake.Akapanda kwa tahadhari kubwa.Mara tu Mathew

alipojitokeza katika ghorofa ya pili akakoswa na risasi ikamlazimu kushuka chini kidogo.Akachukua kioo kidogo akakiinua juu na kumuona mtu mmoja akiwa na bastora amesimama katika mlango huku mtu mwingine akiwa ameanguka chini amepigwa risasi.Mathew alipoinua kichwa tu ikasikika milio ya risasi akajificha tena halafu akaambaa na mbao ya ngazi taratibu kisha akaruka na kutokeza katika varanda akaachia risasi na kumpiga Yule jamaa risasi katika bega la kushoto akaanguka chini akaanza kumsogelea

“Khalid ! akasema Mathew baada ya kumgundua mtu Yule alikuwa ni Khalid Sultan Khalid.

“Usinisogelee nina bomu ! akasema Khalid na kumuonyesha Mathew kilipuzi alichokuwa nacho mkononi.Khalid alikuwa amevaa fulana ya mabomu.Jicho la Mathew liliona kama la kinyonga.Aliweza kukiona kidole gumba kikibonyeza kile kilipuzi akageuka na kuruka hatua tatu kubwa na mara ukasikika mlipuko.Khalid akajilipua.Mathew akajikuta amerushwa na kujigonga

ukutani.Baada ya sekunde kadhaa akajiinua mahala alipoangukia.Alikuwa amepasuka juu ya jicho.Varanda lilijaa moshi.Akatoa kopo Fulani katika begi lake alilovaa mgongoni akapuliza hewa iliyokuwamo ili kuondoa ule moshi.

Bomu lile alilolipua Khalid liliusambaratisha mlango wa chumba cha Melanie na sehemu ya chuma ya mlango ule uliosambaratika ilimpiga Melanie kichwani akaanguka chini na kupoteza fahamu.

Moshi ulipungua kufuatia hewa ile aliyoipuliza Mathew

na akaweza kumuona Khalid akiwa amesambaratishwa na bomu.Mlango wa chumba cha Melanie uling'oka,Mathew akapuliza ile hewa toka ndani ya kopo na moshi ukatoka mle chumbani akauona mwili wa mwanamke ukiwa umelala sakafuni akamuendea haraka haraka akamgeuza alikuwa ni Melanie Davis ambaye hakuwa na fahamu.

"I need you Melanie ! akasema Mathew na kumchunguza kama amekufa akagundua hakuwa amekufa bali alipoteza fahamu kwani bado mapigo ya moyo yalikuwepo.Haraka haraka

akatoa simu na kumpigia simu Ruby

“Mathew are you okay? Tumesikia mlipuko mkubwa na moshi ukatoka humo ndani.Nimeogopa”akasema Ruby

“I’m okay Ruby.Nini kinaendelea huko nje? Akauliza Mathew

“Huku nje kuna taharuki kubwa kufuatia milipuko ile ya mabomu”

“Jackson yuko karibu?

“Niko hapa kaka” Jackson akajibu akitokea nje ya kile chumba kile alimo Mathew

“Niliamua kuingia ndani kuhakikisha kama uko salama

baada ya mlipuko kutokea” akasema Jackson

“Niko salama Jackson” akasema Mathew

“Ruby tayari nimemuona Jackson”

“Mathew nasikia ving’ora vya polisi wanaelekea eneo hili”akasema Ruby

“Tayari wamekwisha pata taarifa za milipuko ile ya mabomu” akasema Mathew na kuiokota kompyuta iliyoanguka chini.Programu ya kurekodi ilikuwa inaendelea.Mathew akaisimamisha na kuanza kupitia kile ambacho Melanie alikuwa

anakirekodi.Akasikiliza kile alichokisema Melanie

“Mungu wangu ! akasema Mathew kwa mstuko baada ya kumaliza kusikiliza maelezo yale ya Melanie

“President ! akasema na kumtaka Jackson ambebe Melanie wakatoka na kuanza kushuka chini

Magari mawili ya polisi yaliyojaa askari yakawasili katika jumba la Melanie na askari wakashuka haraka haraka wakalizingira jumba lile na kuzungusha utepe wa njano kuzuia watu kukaribia mahala pale halafu wengine wakaelekezwa kujiandaa kwa

ajili ya kuingia ndani.Geti likasukumwa na kikosi cha askari kumi wakaingia ndani na mara katika mlango mkubwa wa kuingilia sebuleni wakajitokeza Mathew na Jackson aliyekuwa amembeba Melanie wakaamriwa kusimama mahala walipo.

“SNSA” akasema Mathew huku askari wakiwasogelea kwa tahadhari

“SNSA tafadhali ! akasema tena Mathew askari wale walipowakaribia zaidi

“Tunatoka idara ya SNSA ! akasema Mathew

“SNSA ni kitu gani ? akauliza kiongozi wa kikosi kile cha askari

“Secret national security agency” akasema Mathew na Yule kiongozi wa kikosi akachukua kile kitambulisho cha Jackson akakisoma na kumrudishia

“Sijawahi kusikia kitu kama hicho.Ninyi nyote mko chini ya ulinzi kama mmetoka idara ya nini mtajitambulisha huko mbele ya safari” akasema Yule kamanda

“Afande SNSA ni idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi.Sisi tunafanya kazi kama mnayoifanya ninyi lakini sisi

tunafanya kwa siri.Unapoendelea kutuweka hapa afande unatufanya tushindwe kutimiza wajibu wetu” akasema Mathew

“Hata sisi tuko kazini ndugu yangu tusifundishane kazi” akasema Yule kamanda

“Afande kuna shambulio limepangwa kufanyika katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere walengwa ni marais wa Tanzania na jamhuri ya kidemokrasia ya Congo.Kuna bomu liko tayari uwanja wa ndege na tukichelewa marais hao watauawa ! akasema Mathew

“Wapekueni haraka watu hawa kisha muwafunge pingu tunakwenda nao kituoni watajieleza huko mbele ya safari ! akasema kwa ukali Yule kamanda.Mathew na Jackson wakapekuliwa silaha zao zikachukuliwa na Yule kamanda akaomba kukiona kitambulisho cha Jackson.Akakisoma halafu akamtazama Mathew

“Nini kimetokea hapa? Akauliza

“Magaidi wa IS walikuwa wanaitumia nyumba hii kwa ajili ya kuandaa mpango wao wa kuwaua marais wa Tanzania na Congo”

“Nitaamini vipi kama kweli idara hii ipo na…..”

“Afande naomba twende ndani tukazungumze” akasema Mathew na Yule kamanda akaongozana na Mathew hadi ghorofa ya pili

“Huyu ambaye mwili wake umesambaratika anaitwa Khalid Sultan Khalid anatoka kikundi cha IS.Ni mtaalamu wa milipuko na alikuja hapa Tanzania kutengeneza bomu ambalo litatumika kuwaua marais wetu na kila kitu kimefanyika ndani ya nyumba hii.Idara yetu imekuwa ikiwafuatailia hawa watu kwa muda sasa na leo tumewatia

nguvuni.Afande tunavyozidi kukaa hapa maisha ya rais wetu yako mashakani kwani tayari bomu limekwisha ingizwa uwanja wa ndege.Ni jukumu letu sisi tukisaidiana na ninyi kuweza kulizuia hilo lisitokee”

“Bomu hilo unalosema limeingiaje ndani ya uwanja wa ndege?akauliza Yule kamanda

“Kuna askari mmoja mwenye cheo cha mkaguzi wa polisi ndiye amesaidia bomu hilo kuingizwa ndani ya uwanja wa ndege”akasema Mathew na Yule kamanda akaonyesha mshangao

“Ngoja nipige simu kuwajulisha viongozi walioko uwanja wa ndege kulitafuta hilo bomu” akasema Mathew

“Hiyo si njia nzuri na hawataweza kulipata kwani aliyelibeba bomu hilo amevaa sare za askari polisi na endapo akifahamu kuwa amegundulika anaweza akakimbia tukashindwa kumpata”

“Nini unashauri tufanye?

“Nahitaji kuzungumza na Rais kumuomba asiende uwanja wa ndege sasa hivi ili tuweze kumsaka huyo mtu aliye na bomu na kumtia nguvuni” akasema Mathew

“Unataka kuwasiliana na Rais?

“Ndiyo.Nina mawasiliano naye” akasema Mathew na kufunguliwa pingu akampigia simu Ruby akamueleza kuhusiana na mpango ule wa kumuua Rais na kumtaka ampige simu Rais amzuie asiende uwanja wa ndege hadi hapo Yule jamaa mwenye bomu atakapokamatwa.Ruby akampigia simu rais lakini simu hakupatikana.

“Simu ya rais haipatikani.Tunahitaji kuwahi uwanja wa ndege kabla hajafika.Kutoka hapa hadi uwanja wa ndege si umbali

mrefu.Chukua vijana wachache tutumie gari la polisi kuwahi uwanja wa ndege.” akasema Mathew wakatoka kwa haraka kwa ajili ya kuelekea uwanja wa ndege.

Mathew akawaelekeza Jackson na Ruby kumkimbiza Melanie hospitali kisha yeye akaingia katika gari la polisi ambalo liliondoka kwa kasi kuelekea uwanja wa ndege wa Julius Nyerere.

Gari lile la polisi lilikwenda kwa mwendo mkali sana huku likipiga king’ora kuomba kuachiwa njia na baada ya dakika kumi na saba wakawasili katika uwanja wa

ndege wa Julius Nyerere.Kamanda Yule aliyejitambulisha kwa Mathew anaitwa Afande Titus akashuka garini na kupiga simu halafu akamtaka Mathew amfuate wakaelekea katika ofisi Fulani ambako waliwakuta makamanda watatu.Afande Titus akamtambulisha Mathew kwa makamanda wale wakataka kufahamu kuhusiana na taarifa ile ya uwepo wa bomu pale uwanjani lililolenga kuwaua marais.Mathew akawaeleza namna bomu lile lilivyoingizwa uwanjani wote wakabaki wanashangaa.Mathew

akawaelekeza namna watakavyoweza kumpata Yule askari mwenye bomu wakakubaliana kisha akaongozana na afande Titus wakaingia ndani ya uwanja.Titus alikuwa na kitabu na kuanza kumfuata askari mmoja mmoja akimuuliza namba yake akaiandika katika kitabu.Karibu na jukwaa ambalo husimama marais kwa ajili ya nyimbo za taifa walisimama askari wawili.Mathew na afande Titus wakamfuata askari wa kwanza wakamuhoji namba zake na

walipomfuata askari wa pili akababaika

“Askari taja namba zako tafadhali ! akasema afande Titus lakini Yule askari hakuweza kutamka chochote.Mathew taratibu akaupeleka mkono akaishika bastora yake

“Askari taja namba yako tafadhali ! akafoka afande Titus na katika redio ya mawasiliano akasikika mtu aliyeko uwanja wa ndege akiwajulisha askari wachukue nafasi kwani msafara wa marais umekwisha wasili pale uwanjani.

“Askari !! akafoka afande Titus

“Husikii ninachokuuliza? Taja haraka sana namba yako tafadhali ! akafoka afande Titus.

Jicho la Mathew liliuona mkono wa Yule askari ulikokuwa unapelekwa akaruka na kumsukuma afande Titus akaanguka chini kisha akaupiga teke mkono wa Yule jamaa akaaguka chini.

“Titus kimbiaaa !! akapiga kelele Mathew na Titus akainuka akaanza kukimbia.Yule jamaa aligeuka na kukishika kidude chekundu.Kabla hajakishusha

kidole gumba katika kile kilipuzi Mathew akawahi kumrukia na kumtandika kichwa kizito usoni na Yule jamaa akaachia kile kilipuzi.Mathew akakikamata kidole gumba akakivunja,akamtandika ngumi mbili mfululizo usoni.Yule jamaa akaukunja mguu wa kulia akampiga Mathew kichwani kwa kutumia goti na kumsukuma Mathew pembeni.Akainuka na kukishika kilipuzi kwa mkono wake wa kushoto Mathew akamkata mtama akaanguka ksha akaushika mkono wa kushoto akauvunja.Yule jamaa

akalia kwa maumivu.Akaukamata pia mkono wa kulia akauvunja Yule gaidi akaendelea kupiga kelele za maumivu.

Taharuki kubwa ilitanda pale uwanja wa ndege wa Julius Nyerere baada ya taarifa kusambaa kwamba kulikuwa na bomu.Watu waliokuwa ndani ya uwanja kwa ajili ya kuwaaga marais waliondolewa haraka.Marais waliondolewa haraka sana pale uwanja wa ndege na kurejeshwa ikulu.

Baada ya kumdhibiti Yule gaidi Mathew akamvua ile fulana yenye bomu akaiweka pembeni akasimama na kutoa

ishara kwamba askari wasogee.Wataalamu wa mabomu kutoka jeshi la polisi wakaondoka na lile bomu.

Baada ya kuikamilisha kazi yake Mathew akawaachia maafisha wa usalama waendelee na kazi yao kwa ahadi ya kwenda kituoni kutoa maelezo ya kina kuhusiana na suala lile.Mathew akampigia simu Ruby na kutaka kufahamu mahala walipo kisha akaomba kupelekwa hospitali ya Mtodora alikopelekwa Melanie.Gari la polisi lilimpeleka hadi hospitali ya Mtodora ambako aliwakuta Ruby na Jackson.Ruby

alimkumbatia Mathew kwa nguvu huku akibubujikwa na machozi

“We did it Mathew ! We did it ! akasema Ruby huku akimwaga machozi

“We saved our president ! akasema Mathew halafu akamfuata Jackson

“Jackson Ahsante sana.Tusingeweza kufika hapa bila msaada wako.Umeingia katika historia ya nchi hii kwa kufanya kitu cha kizalendo” akasema Mathew akakumbatiana na Jackson

“Madaktari wanasemaje kuhusu Melanie?

“Wanaendelea kumuhudumia.Bado hajapata fahamu mpaka sasa” akasema Ruby

“Tutarejea hapa hospitali lakini kwa sasa wasiliana tena na Rais tukaonane naye.Anapaswa kufahamu kila kilichotokea” akasema Mathew na Ruby akampigia simu rais na simu yake ikapokelewa

“Unasemaje Ruby?

“Mheshimiwa Rais pole sana kwa kilichotokea leo”

“Ahsante”

“Mheshimiwa Rais tunahitaji kukuona”

“Haitakuwa rahisi kuonana nanyi kwa sasa

kutokana na itifaki za kiusalama hasa pale kunapotokea kitisho cha usalama kama kilichotokea leo”

“Mheshimwia rais ni muhimu sana tukaonana nawe.Kuna mengi ambayo unapaswa kuyafahamu.Kwa ufupi tu sisi ndio tuliofanikisha kila kitu kilichotokea leo.Ni mambo mazito ambayo unapaswa kutusikiliza” akasema Ruby ukapita ukimya kidogo na Dr Fabian akakubali kuonana nao.

Wote watatu wakaingia katika lile gari alilokuwa anaendesha Jackson ambalo

lilikuwa na mwili wa James Kasai katika buti ya gari wakaondoka kuelekea ikulu.Njiani bado Ruby aliendelea kutiririkwa na machozi.

“Ruby nini kinakuliza?

“Nimetazama rekodi ile ya Melanie imenisikitisha sana.Kumbe ni binti mdogo tu lakini amegeuka akawa mkatili kiasi hiki.Nimejikuta nikimuonea huruma” akasema Ruby

“Hakuna kumuonea huruma mtu ambaye anashirikiakana na magaidi.Alichokipata anastahili na ana bahati

ameingia katika mikono yangu akiwa hana fahamu nilikuwa na hasira naye sana ! akasema Mathew akaichukua kompyuta ile ya Melanie na kuanza tena kusikiliza ile rekodi .

“Afrika Mashariki iko salama.Njama za mabeberu zimeshindwa kufanikiwa.Mungu anaendelea kusimama na Tanzania” akasema Mathew

“Kwangu mimi naona ni muujiza kumuua James Kasai ambaye ameleta hofu kubwa Afrika mashariki” akasema Ruby kwa hisia kali na kumwaga tena machozi

****

Akina Mathew waliwasili ikulu ambako walinzi wake uliongezeka maradufu.Walipokewa na kupelekwa moja kwa moja katika chumba cha mikutano midogo cha Rais

“Ni mara yangu ya kwanza kufika ikulu” akasema Jackson

“Utaendelea kufika hapa mara kwa mara.Huu ni mwanzo tu” akasema Mathew

Dakika chache baadae mlango ukafunguliwa wakaingia walinzi wa Rais halafu akaingia Rais Dr Fabian Kelelo.Mathew na wenzake

wakasimama na Rais akawataka waketi.Akawatazama kwa muda halafu akasema

“Nimechelewa kufika hapa kuzungumza nanyi nilikuwa katika simu na mkuu wa jeshi la polisi nchini akinijulisha kuhusiana na matukio yaliyotokea leo jijini Dar es alaam.Nimeambiwa kwamba helkopta ya idara ya SNSA imelipuliwa leo katika bohari la idara hiyo na kumefanyika mauaji ya watu huko.Nikaambiwa tena kuna milipuko ya mabomu imetokea katika nyumba moja kwenye kijiji cha mabilionea na huko

watu kadhaa wameuawa na kwa taarifa ambayo mkuu wa jeshi la polisi nchini ameipata ni kwamba mlikutwa eneo hilo na mkajieleza kuwa mnatoka SNSA na mkaeleza kuwa kuna mtu ana bomu katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere na amelenga kutuua mimi na Rais Patrice Eyenga.Amenieleza kile kilichotokea uwanja wa ndege namna ulivyoweza kumdhibiti Yule gaidi.Nataka mnieleze kwa kina kila kitu kilichotokea” akasema Dr Fabian na Mathew akamueleza kila kitu namna walivyoendesha operesheni yao hadi

walivyoikamilisha.Mashavu ya Dr Fabian yalionekana na michirizi ya machozi wakati Mathew akiendelea kumsimulia.Akatoa kitambaa akafuta machozi akashinda kujizuia kulia kwa kwikwi

“Let him cry ! Mathew akawaambia wenzake.Dr Fabian alilia kwa takribani dakika tatu halafu akafuta machozi akavaa miwani yake

“Mtanisamehe nimeshindwa kujizuia kumwaga machozi” akasema Dr Fabian

“Mathew Mulumbi wewe ni halisi au ni mzimu kama

wengi wanavyohisi?akauliza Dr Fabian

“Mimi ni halisi mheshimiwa Rais” akajibu Mathew

“Nashindwa niseme nini.Nilikudharau sana Mathew Mulumbi.Sikujua kama leo hii wewe niliyekudharau ndiye ambaye umeniokoa.Kama si wewe basi hivi sasa mimi na mwenzangu Patrice tungekwisha fariki dunia”

“Ni Mungu anayepaswa kushukuriwa kwanza kwani hakutaka kukuchukua siku ya leo kwani kama ingekuwa ni kwa mipango yake hata mimi

nisingeweza kukuokoa lakini vile vile kuna watu wengine nyuma yangu ambao kwa pamoja tumeshirikiana katika operesheni hii kwa niaba yao ninasema ninapokea ahsante sana” akasema Mathew na Dr Fabian akavua tena miwani akafuta machozi

“Mtanisamehe vijana wangu kwa hali hii nashindwa kujizuia”

“Mheshimiwa rais nadhani ungeitazama rekodi ile ya Melanie” akasema Mathew na kumsogezea Dr Fabian kompyuta ya Melanie akamchezea ile rekodi ya Melanie

“Nafahamika kama Melanie Davis au Melanie Chuma lakini hilo si jina langu halisi.Jina langu halisi ni Theresia Muganza mtoto wa Laurent na Lucy Muganza kutoka jamhuri ya kidemokrasia ya Congo ambao waliuawa nchini Tanzania.Nilikuwa ninasoma hapa Tanzania na niliipenda sana nchi hii lakini mambo yalibadilika pale walipouawa wazazi wangu, mauaji ya kikatili sana ambayo chanzo chake ni sababu za kisiasa.Mama yangu alikuwa bilionea na hakuwahi kufikiri hata mara moja kuingia katika

siasa hadi pale aliposhawishiwa na serikali ya Ufaransa agombee urais kwa manufaa yao.Rais Patrice Eyenga alipoingia madarakani alikata mirija yote ya mabeberu waliokuwa wakinyonya rasilimali za Congo na hilo halikuwapendeza mabeberu hivyo wakaanza kutafuta namna watakavyoweza kurudi tena kufaidika na rasilimali za nchi ya Congo wakamshawishi mama yangu awanie urais.Waliamini atashinda uchaguzi hivyo wakampa kazi nyingine ya kuhakikisha anaisambaratisha jumuiya ya

afrika mashariki .Kwa bahati mbaya aligundulika mapema akauawa na mimi nikanusurika

Nilipelekwa Ufaransa kwa matibabu na Mungu akanijalia nikapona ndipo nilipoelezwa ukweli wa kile kilichotokea kuhusu mauaji ya mama yangu.Nilipandikizwa hasira ambazo zilizaa chuki kubwa dhidi ya nchi za Tanzania Congo na Afrika mashariki kwa ujumla nikaulizwa kama niko tayari kuvaa viatu vya mama yangu nikakubali nikafanyiwa upasuaji bandia kubadili mwonekano wangu halafu nikatumwa kuja

Tanzania kwa lengo la kulipiza kisasi lakini kubwa likiwa ni kuivuruga jumuiya ya afrika Mashariki.Nilibadilishwa jina nikapewa jina la Melanie Davis.Hapa Tanzania nilikutana na mtu anaiwa Edwin Mbeko ambaye ni mkurugenzi wa idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi SNSA ambaye huyu aliwekwa maalum kwa ajili ya kuhakikisha mipango yangu yote inafanikiwa.Nilipewa jina lingine la Melanie Chuma ili wakati mwingne nijulikane kama mtanzania.Nilinunua makampuni hapa Tanzania na fedha nilipewa na serikali ya

Ufaransa ambao ndio wananifadhili.Niliingia hapa nchini kama mwekezaji na mpango wangu wa kwanza ulikuwa ni kuwaua wake za marais wa Tanzania na Congo.Nilikutana na balozi wa Congo hapa nchini nikamshawishi aandae chakula maalum na kuwakaribisha wake za marais wa Congo na Rwanda na lakini kukawa na ugumu wa kumpata mke wa Rais wa Rwanda na ndipo alipomtumia mke wa Rais wa Tanzania ili kumleta mezani mke wa rais wa Rwanda.Niliandaa mpango ule nikishirikiana na James Kasai

ambaye nilikwenda kuonana naye Uganda. Baada ya shambulio lile lililowaua wake za marais nikaelekezwa tena kuandaa shambulio lingine ambalo linalenga kumuua Rais Patrice Eyenga.Nilimfuata James Kasai nikaongea naye suala hili naye akanipeleka kwa Rais wa Uganda Jenerali Akiki ambaye alikubali kushirikiana nasi katika mpango huo na alitaka baada ya Patrice kuuawa James Kasai achukue nchi.Akiki alinieleza kwamba Majenerali wa jeshi la Congo walikuwa wanandaa mpango wa mapinduzi hivyo akamuita mkuu wa majeshi wa

Congo akazungumza naye lakini wakashindwa kuelewana kuhusu James Kasai kushirikishwa katika serikali baada ya mapinduzi ndipo tulipoamua kuendelea na mpango wa kumuua James Kasai bila kushirikiana na wakuu wa jeshi la Congo.Tulipanga Jenerali Akiki aombe kukutana jijini Dar es salaam na marais wa Tanzania na Congo azungumze nao kuhusu kutafuta muafaka wa amani kufuatia mashambulizi yale yaliyofanywa na James Kasai jijini Dar es salaam.James aliwasiliana na IS wakamtuma

mtu anaitwa Khalid Khalid ambaye ni mtaalamu wa mabomu kuja kuandaa bomu ambalo litaweza kuwaua marais wa Tanzania na Congo.Edwin Mbeko kwa kutumia idara ya SNSA aliweza kufanikiwa kuingia nchini kwa James Kasai pamoja na Khalid Khalid.Rais Akiki alimpigia simu Rais wa Tanzania akamtaka aandae mkutano naye akakubali bila kujua ni mtego.Kwa kumtumia Edwin Mbeko pia tuliweza kumuingiza nchini mtu ambaye angejitoa mhanga na kuwaua marais.

Leo hii kumefanyika kikao hicho cha marais watatu na ninaamini muda si mrefu kutoka sasa AfrikaMashariki itaingia katika msiba mkubwa wa kuondokewa na marais wawili kwa wakati mmoja.Shambulio la bomu litakalotokea muda mfupi ujao na kuwaua marais wa Tanzania na Congo tumeliandaa sisi.

Nimeamua kueleza ukweli huu kwani nyumba yangu kwa sasa imezingirwa na watu ambao naamini ni wapelelezi hivyo sintatoka hai ndani ya chumba hiki.Baada ya kumaliza hii rekodi

nitajimaliza mwenyewe kwa risasi,siko tayari kukamatwa.Katika dakika hizi ambazo nyumba yangu imezingirwa na wapelelezi ninakiona kifo changu na ninaumia sana kwa mateso na maumivu niliyowasababishia watu ambao niliwaua ndugu zao, nimejikuta nikijutia kile nilichokifanya.Mimi ni msichana mdogo bado lakini nimeingia katika historia ya watu makatili wakubwa si kwa kupenda bali ni kwa sababu ya maslahi ya mabeberu.Ninajilaumu kwa kukubali kutumika.Nilikubali kuwa kibaraka wao na kuua

waafrika wenzangu.Nimeyasema haya ili waafrika wenzangu wajifunze kwani si mimi peke yangu ninayetumiwa na mataifa makubwa ya nje.Wapo watu wengi katika taasisi za serikali na hasa viongozi wa siasa.Hawa wamekuwa wakitumiwa sana na serikali za mabeberu katika kuleta migongano ndani ya nchi zao.Machafuko mengi yanatokea katika nchi zetu za afrika chanzo chake ni wanasiasa ambao ukiwachunguza wanatumiwa na mabeberu kutuvuruga ili mabeberu hao waweze kupata

mwanya wa kuingia katika nchi zetu na kuchota rasilimali.Wanafanya haya kwa malipo ya fedha ambazo zinawawezesha kuishi maisha ya kifahari kama niliyoishi mimi na kusahau kwamba nchi zetu zinaendelea kuwa masikini na kunyonywa kila uchao.Niliingia katika mtego wao nikanasa na katika dakika zangu za mwisho nimegundua kosa nililolifanya.Kama nisingekubali kutumiwa na mabeberu ningekuwa na maisha marefu na ndoto zangu nyingi zingetimia lakini nimekatisha ndoto zangu katika umri huu mdogo.Huu ni

mfano kwa wale wote wenye kufanya mambo kama niliyoyafanya mimi kuwa mwisho wenu ni mbaya na yawezekana mwisho wenu ukawa mbaya kuliko wa kwangu.Usaliti kwa nchi yako ni dhambi kubwa.Ninat……..”
Rekodi haikuendelea tena kukasikika kishindo na kukawa giza.Ni pale ambapo Khalid alijilipua na kipande cha mlango kikampiga Melanie kichwani

“Nimekosa maneno ya kusema ! akasema Dr Fabian

“Nani mwingine ambaye ameiona rekodi hii? Akauliza Dr Fabian

“Hakuna mwingine zaidi yetu sisi” akajibu Mathew

“Good.Rekodi hii inapaswa kufanyiwa kazi haraka sana na vyombo husika…….”akasema Dr Fabian na Mathew akamkatisha

“Mheshimiwa rais sisi tumekamilisha jukumu letu la kuilinda nchi na hatua zinazofuata tunaiachia serikali.Kwa mfano kuna mtandao wa IS hapa nchini ambao unapaswa kufumuliwa nk.Kama hutajali mheshimiwa Rais ninaomba tukakukabidhi

mwili wa James Kasai ili uthibitishe kwamba kweli ameuawa”akasema Mathew kisha Dr Fabian akaelekeza Rais Patrice Eyenga aitwe ili kwa pamoja wakashuhudie mwili wa James Kasai.

Akina Mathew wakiongozana na marais wale wawili wakaelekea katika gari la Mathew buti likafunguliwa na mwili wa James Kasai ukaonekana.Dr Fabian na Patrice wakathibitisha kuwa ni yeye,akaelekeza liitwe gari la kubebea wagonjwa ili mwili ule ukahifadhiwe hospitali.Wakarejea ndani

katika chumba cha mikutano midogo

“Vijana wangu sijui nizungumze nini kwa hiki mlichokifanya.Ni kitu kikubwa sana ambacho vizazi na vizazi vinapaswa kuusoma ujasiri wenu.Hiki mlichokifanya kinapaswa kuingia katika historia ya nchi ili mkumbukwe na watoto wa watoto wenu kwamba waliwahi kutokea vijana Fulani ambao walionyesa uzalendo wa ajabu kwa nchi hii.Mathew umepambana na gaidi aliyekuwa na bomu.Ni vipi kama gaidi Yule angeweza kulipua bomu lile wakati

ukimdhibiti?Hukulijali hilo lakini ulichokuwa unahitaji ni kuokoa maisha yangu.Sina neno la kusema.Sijui ni tuzo gani upewe itakayolingana na hiki ulichokifanya.Nitalihutubia taifa usiku wa leo na ningependa watanzania wafahamu kitu kikubwa mlichokifanya leo" akasema Dr Fabiana na kuwatazama akina Mathew

"Mheshimiwa Rais tulichokifanya ndicho tulichoapa kukifanya.Tuliapa kuilinda nchi dhidi ya adui wa ndani na wa nje na leo tumetimiza wajibu wetu.Kwa

niaba ya wenzangu tunaomba jambo hili libaki kama lilivyo na tusitambulishwe kwamba sisi ndio tuliomuua James Kasai na kuzima shambulio la kigaidi.Wewe ukitushukuru basi tunaamini watanzania wote wametushukuru hivyo basi hatutapenda kutangazwa” akasema Mathew

Kikao kiliendelea hadi ilipotimu saa kumi na mbili za jioni ndipo Rais Patrice Eyenga akaondoka nchini kurejea nchini kwake jamhuri ya kidemokrasia ya Congo.Mwili wa James Kasai ukachukuliwa na kupelekwa

hospitali kuu ya Mtodora kuhifadhiwa

Mathew na wenzake wakaagana na Rais wakaondoka wakaelekea hospitali ya Mtodora kujua maendeleo ya Melanie.Walijulishwa na madaktari kwamba ubongo wa Melanie umekufa hivyo hataweza kuamka tena.

Kutoka hospitali ya Mtodora wakaelekea katika nyumba walikolazwa Austin na Gosu Gosu.Hali ya Gosu Gosu iliendelea vizuri na aliweza kufumbua macho lakini wakati walipofika akina Mathew alikuwa amelala na

hawakutaka kumuamsha.Walimsimulia Austin kilichotokea

“Nasikitika nimekosa mengi” akasema Austin na wote wakacheka

“Usijali Austin hata uwepo wako hapa hospitalini ni jambo kubwa sana kwani umeokoa maisha ya GosuGosu” akasema Mathew kisha wakamuaga Austin na kurejea nyumbani kwao.Ruby akayaganga majeraha yote aliyoyapata Mathew kisha wakapata chakula halafu wakaelekea sebuleni kutazama hotuba ya Rais

“Ndugu watanzania wenzangu,napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na kuendelea kusimama na nchi yetu

Ndugu watanzania wenzangu siku,chache zilizopita nilisimama hapa nikiwapa taarifa za tukio baya kabisa kutokea hapa nchini ambapo watu wasio na ubinadamu wenye roho za kishetani walivamia nchi yetu na kutekeleza shambulio baya kabisa ambalo lilikatisha kikatili maisha ya wapendwa wetu. Niliposimama hapa

niliwaahidi kwamba mimi na serikali yangu hatutakaa kimya kwa yeyote aliyeshiriki katika shambulio lile baya.Niliahidi kwamba tutawasaka kokote duniani wale wote waliomwaga damu ya watanzania.

Shambulio lile baya kabisa lilifanywa kwa ushirikiano wa James Kasai kiongozi wa kundi la waasi ambaye anashirikiana na kundi la kigaidi la IS.James Kasai alifurushwa nchini Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo baada ya kugoma kushiriki katika mpango wa amani na akakimbilia nchini Uganda ambako amekuwa akiishi na kukijenga kikundi

chake akifadhiliwa na serikali ya Uganda. Wakati dunia nzima ikiamini James Kasai anaishi msituni nchini Uganda lakini James Kasai amekuwa akiishi katika jiji la Kampala maisha ya kifahari sana na hili hata wananchi wengi wa Uganda hawalifahamu.

Kwa kushirikiana na nchi za Rwanda na Congo tuliahidi kumsaka James Kasai kokote aliko duniani na kuhakikisha tunamtia nguvuni.Wakati mipango na mikakati yetu ikiendelea , James Kasai kwa kushirikiana na mtandao wake aliweza kuingia hapa nchini.Vijana wetu wazalendo

kwa nchi yao waliokula kiapo cha kuifia nchi yao walizipata taarifa hizo za James Kasai kuja Tanzania wakamfuatilia.

Ndugu watanzania wenzangu ninasimama hapa kuwajulisha kwamba James Kasai Yule muuaji aliyemwaga damu ya watanzania bila hatia ameuawa leo mchana na vijana wetu wazalendo.Si yeye peke yake bali pia washirika wake wa karibu pia wameuawa na wengine hivi sasa wanatafutwa.

Ndugu watanzania vijana hawa wazalendo ambao wamefanikisha,kumuua katili huyu na genge lake wameokoa

jumuiya ya Afrika mashariki kusambaratika.Ndugu zangu jambo hili ni pana zaidi ya tunavyolifikiri.Ipo nguvu kubwa kutoka mataifa makubwa ambayo inataka kutusambaratisha na kuvuruga umoja wetu lakini Mungu ameendelea kusimama na nchi yetu pamoja na jumuiya ya Afrika mashariki.Tumekwisha zifahamu nchi hizo,tumekwisha wafahamu viongozi wa nchi hizo ambao wanapanga mipango ya kutuvuruga na tutaendelea kuchukua hatua mbali mbali lakini naomba mfahamu kwamba tuko katika vita

mbaya ya kiuchumi na katika vita hii tunapambana na mataifa makubwa yenye nguvu kutushinda sisi.Wanawatumia watu wetu wenyewe kutugawa na kutuvuruga .Wapo viongozi ndani ya serikali,wapo wanasiasa wapo viongozi wa dini ambao wanatumiwa na mataifa makubwa ya nje katika vita hii.Ninawaomba ndugu zangu watanzania tuipende nchi yetu.Kuisaliti nchi yako kwa fedha kidogo kutoka kwa mabeberu ni dhambi kubwa na mwisho wake ni mbaya.

“Mathew my love kuna jambo nataka kuuliza” akasema Ruby wakati

wakiendelea kutazama hotuba ya Rais

“Uliza mpenzi” akasema Mathew

“Hatimaye misheni imekwisha,James Kasai ameuawa,washirika wake pia wameuawa na wengine wa mtandao wa IS wanaendelea kutafutwa na vyombo vya usalama.Baada ya kazi hii ngumu nini kinafuata? Akauliza Ruby

“Kama nilivyokueleza awali kwamba nitaondoka baada ya kukamilisha misheni hii lakini nitarejea tena kwa ajili yako.Narudia tena kukukumbusha kwamba

nitakapoondoka usijaribu kunitafuta kuwa mvumilivu nitarudi” akasema Mathew

BAADA YA SIKU 3

Afya ya Gosu Gosu iliimarika sana na sasa aliweza hata kuinuka na kukaa mwenyewe kitandani.Ni siku ya tatu toka alipouawa James Kasai.

Saa nne za asubuhi gari la wagonjwa liliwasili katika hospitali kuu ya Mtodora kitanda cha wagonjwa kikashushwa garini na kusukumwa kuelekea katika wodi alikolazwa Melanie

Davis.Pembeni yake walikuwepo Mathew na Ruby

Melanie aliwekewa mashine ya kumsaidia kupumua.Gosu Gosu alipomuona sura yake ikabadilika.Mathew akawaomba watu wote watoke mle ndani akabaki Gosu Gosu akimtazama Melanie

“Sikujua kumbe u shetani uliyevaa mwili wa binadamu Melanie.Nilikupenda kwa moyo wangu wote nikiamini wewe ni mwanamke ambaye umeumbwa kwa ajili yangu.Nilikuwa tayari kufanya kila ulichokitaka na kwa sababu yako nilichungulia

kaburi.Ninashukuru nimekuona ukiwa katika hali hii kwani ungekuwa mzima ningekuua kifo kibaya sana” akasema Gosu Gosu kwa sauti ya chini halafu Mathew akaingia

“Gosu Gosu muda umefika.Kamilisha zoezi ukapumzike” akasema Mathew na Gosu Gosu akasogezwa kitufe ili azime mashine ile ya kumsaidia Melanie kupumua.

“Kwa heri Melanie” akawaza Gosu Gosu na kubonyeza kitufe kile akazima mashine ya kupumua na

ukawa mwisho wa Melanie Davis.

****

Ni Ruby pekee aliyefahamu kuhusu kuondoka kwa Mathew Mulumbi kwani ndiye aliyemsindikiza uwanja wa ndege akapanda ndege kuelekea Cairo Misri.

“Nimemaliza misheni ya kwanza.James Kasai ameuawa na Afrika mashariki iko salama.Njama za mabeberu zimeshindwa.Ninamshukuru sana Habiba Jawad ambaye ameniwezesha kwa kiasi kikubwa kufanikisha misheni

hii muhimu sana kwa nchi yangu.Ninakwenda tena katika misheni nyingine ambayo kwa mujibu wa Habiba Jawad ni kubwa kuliko hii niliyoimaliza.Mungu ataendelea kusimama nami” akawaza Mathew akiwa ndegeni

MWISHO WA SIMULIZI YA MAISHA NA KIFO CHA MELANIE CHUMA.USIKOSE SEHEMU YA TATU NA YA MWISHO YA SIMULIZI YA SIRI IITWAYO JASUSI/GAIDI.